# UCHUNGUZI WA SABABU NA ATHARI ZA KUTOFAUTIANA KWA IDADI YA FONIMU NA VIASHIRIA VYAKE KATIKA KISWAHILI SANIFU

**AMOUR ABDALLA KHAMIS**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SHARTI PEKEE YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMIVU (PhD YA KISWAHILI-LUGHAWIYA) IDARA YA TAALUMA ZA ISIMU NA FASIHI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2024**

## UTHIBITISHO

Waliotia saini hapa chini wanathibitisha kwamba, wameisoma tasnifu hii inayohusu; **Uchunguzi wa Sababu na Athari za Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake katika Kiswahili Sanifu**, na wanapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sharti pekee ya kutunukiwa Shahada ya Uzamivu (PhD) ya Kiswahili-Lughawiya ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

..........................

Dkt. Peter Lipembe

(Msimamizi)

..........................

Tarehe:

..........................

Dkt. Dunlop Ochieng

(Msimamizi)

..........................

Tarehe:

## HATIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga, kunakili au kutolewa kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya Tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au kuitoa kwa njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba ya mwandishi wa Tasnifu hii.

## TAMKO

Mimi, **Amour Abdalla Khamis** natoa tamko la kuthibitisha kwamba, Tasnifu hii ya Uchunguzi wa Sababu na Athari za Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake katika Kiswahili Sanifu ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chingine chochote kwa mfanano au kwa kiwango cha kutunukiwa shahada ya uzamivu au shahada nyingine yoyote.

**…………………………………**

**Saini**

**………………………………**

**Tarehe**

## TABARUKU

Kazi hii ni hidaya adhimu kwa wazee wangu bwana Abdalla Khamis Mavua na mama Hidaya Haji Haji walionizaa, kunilea, na kuamua kunisomesha tangu elimu ya msingi na kwa kudura, ihisani na rehema zake ALLAH (SW) hatimaye akaniruzuku kufikia kiwango hiki cha elimu katika somo la Kiswahili-Lughawiya.

# SHUKURANI

Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa kunijaalia uhai na afya pamoja na kunielekeza kwa ihisani na rehema zake katika kuifanya kazi ya kielimu ya kiwango hiki. Nakiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi shukurani zangu kwake kwa kusema: Alhamdulilahi Rabbil’aalamiina.

Pia, natoa shukurani zangu za dhati kwa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa kunifadhili na kuweza kunilipia gharama kubwa ya masomo yangu haya. Kwa hakika, ufadhili nilioupata kutoka katika Mamlaka hii ulinitia ari na kunipa motisha wa kuisoma shahada hii hadi kukamilika kwake.

Shukurani za dhati nyingine ziwaendee Prof. A. S. Nchimbi (marehemu), Dkt. P. Lipembe na Dkt. D. Ochieng kwa usimamizi na miongozo yao mizuri na yenye muwafaka katika utafiti wangu huu. Kwa bidii na upole wao, hawakuacha kunielekeza na kunishauri ipasavyo kwa zile sehemu zilizohitaji marekebisho ya kitaalamu tangu mwanzo wa kuandaa pendekezo hadi kufikia kuiandikia ripoti Tasnifu hii kama ilivyowasilishwa.

Nina wajibu sana wa kutoa shukurani za dhati kabisa kwa Wasailiwa yaani, wanafunzi na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Chuo Kikuu cha Zanzibar, Chuo Kikuu cha Sumait na Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ambao waliteuliwa na kukubali kushiriki kikamilifu katika kujibu usaili wa Hojaji na usaili wa Mahojiano na kunipatia taarifa sahihi zilizoniwezesha kuzichanganua na kuzijadili na hatimaye kuukamilisha utafiti wangu na nikaweza kuiandika ripoti ya Tasnifu hii.

Shukurani nyingine, napenda ziwafike Prof. Dkt. Shk. TSYM Sengo, Prof. Issa H. Ziddy, Dkt. Abdulrahim H. Taib, Dkt. Hamad Kh. Juma, Dkt. Haroun A. Maalim, Dkt. Haji M.

Ussi, Dkt Abdalla I. Kidodi na Mwl. Bakar K. Bakar kwa kunipa ushauri elekezi wa hapa na pale katika kuimarisha kazi yangu hii.

Kadhalika, nawashukuru Dkt. Abdalla A. Shaame, Mwl. Abdurahman M. Nahoda, Seif Gh. Omar na Mudathir K. Haidar kwa ushauri wao wa kitaalamu wa matumizi ya kompyuta wakati wa kuandika ripoti ya Tasnifu hii.

Kwa dhati yangu, natoa shukurani nyingi kwa Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kwa kunivumilia kuifanya kazi hii wakati wa kazi. Aidha, uongozi huo ulinipa moyo wa kuikamilisha kazi pale nilipovunjika moyo na kutokana na kumkosa msimamizi kwa kipindi cha miaka mine aliposafiri nje ya Tanzania na kutoweza kuwasiliana naye kabisa.

Kwa namna ya kipekee, napenda kumshukuru Dkt. Salma O. Hamad, Dkt. Mohamed O. Maguo na Dkt. Zelda. E. kwa kunishawishi na kunitia ari mpya ilionipa nguvu na matumaini mapya ya kuikamilisha kazi hii baada ya kitambo cha miaka mitatu cha kuiacha kuiendeleza.

Ingawa sio kwa umuhimu, nawashukuru mke wangu na watoto wangu kwa stahamala yao na uvumulivu mkubwa waliouonesha kwangu na kunipa moyo wa kuikamilisha kazi hii kwa kipindi chote cha kujiendeleza katika masomo yangu haya.

Mwisho kabisa, sina budi kuwashukuru wale wote ambao sikuwataja majina yao hapa ambao kwa namna moja ama nyingine walichangia katika utafiti huu hadi kufikia kukamilika kwake. Kwa jumla nasema kwamba naithamini sana michango yao yote kwa jumla na insha Allah, Mwenyezi Mungu ndiye atakayewalipa malipo mema yenye thamani zaidi kwa michango yao waliyoitoa katika utafiti huu.

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza sababu na athari za kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu. Uchunguzi huu ulifanyika kutokana na kuwagundua wataalamu zaidi ya 35 waliotofautiana katika uwasilishaji wao wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu. Utafiti una malengo mahsusi ya kubaini sababu, athari na mapendekezo ya tatizo la kuofautiana kwa wataalamu katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu. Utafiti ulitumia nadharia ya Lyons (1968) ya Umbo-Sauti Maumbo Kimatumizi pamoja na kanuni ya Trubetzkoy (1939/1969) *ya* Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili. Data zilikusanywa kutoka maktabani na nyanjani. Sampuli ilikuwa na Wasailiwa 115 walioteuliwa kutoka vyuo vikuu vya SUZA, ZU, SU na MNMA. Data zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya majedwali, grafu na maelezo. Utafti ulibaini kwamba, kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu kuna sababu 14 na athari 15. Utafiti ulibaini sababu kuu ni ile ya wataalamu kutoainisha kanuni inayowasilisha idadi ya fonimu na athari kuu ni ile ya kuibua mgogoro wa kuwachanganya na kuwababaisha wahadhiri, wanataaluma na wasomi wa vyuoni kwa kutojua idadi gani ni sahihi kati ya 27, 28, 29, 30, 31, 32, 33, 34, 35, 36, 37, 38, 40, 41, 42, 45 na 58. Utafiti pia uligundua kuwa kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake, kumetokana na wataaalamu zaidi ya 35 kuwasilisha baadhi ya fonimu ambatano ambazo hazikubaliki kuwa ni fonimu baada ya kupimwa kwa kanuni ya kisayansi inayowasilisha idadi sahihi ya fonimu na viashiria vyake. Utafiti umethibitisha kwamba, kanuni ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili za maneno ni ya kisayansi na ni suluhisho la kuwasilisha idadi ya fonimu za Kiswahili sanifu. Kanuni hii itaweza kuziba pengo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu. Kwa kuondosha tatizo la kutofautiana, Utafiti ulipendekeza wataalamu wa fonolojia ya Kiswahili sanifu wakiongozwa na Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki, wakae pamoja na kukubaliana kuhusu idadi moja ya fonimu na viashiria vyake kulingana na nadharia na kanuni muwafaka. Mabaraza ya Kiswahili yamesisitizwa yasimamie kwa makini sera ya Kiswahili na kuupitia upya usanifishaji wa Kiswahili ili kuweka makubaliano ya pamoja na kuepukana na tatizo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

## YALIYOMO

**UTHIBITISHO** .......... i

**HATIMILIKI** .......... ii

**TAMKO** .......... iii

**TABARUKU** .......... iv

**SHUKURANI** .......... v

**IKISIRI** .......... vii

**YALIYOMO** .......... viii

**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... xivv

**ORODHA YA GRAFU** .......... xv

**ORODHA YA MICHORO** .......... xvi

**ORODHA YA VIAMBATANISHO** .......... xvii

**ORODHA YA VIFUPISHO** .......... xviii

**ORODHA YA ALAMA** .......... xix

**FASILI ZA ISTILAHI ZILIZOTUMIKA** .......... xx

**SURA YA KWANZA** .......... 1

**UTANGULIZI** .......... 1

1.1 Utangulizi .......... 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti .......... 1

1.3 Tatizo la Utafiti .......... 3

**1.3.1 Maswali kuhusu Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake 10**

1.4 Malengo ya Utafiti ... 12

**1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti ... 12**

**1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti ... 12**

**1.4.3 Maswali ya Utafiti ... 12**

1.5 Umuhimu wa Utafiti ... 13

1.6 Mipaka ya Utafiti ... 14

1.7 Vikwazo vya Utafiti ... 15

1.8 Muundo wa Tasnifu ... 16

1.9 Hitimisho ... 17

**SURA YA PILI ... 118**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA ... 18**

2.1 Utangulizi ... 18

2.2 Dhana ya Fonimu ... 18

2.3 Asili ya Fonimu za Lugha ... 21

2.4 Fonimu Kuwa Kijenzi cha Msingi katika Lugha ... 23

2.5 Dhana ya Fonolojia ya Lugha ... 29

2.6 Usanifishaji wa Kiswahili na Athari zake ... 30

2.7 Matatizo ya Kutofautiana katika Fonolojia ya Kiswahili Sanifu ... 35

2.8 Kutofautiana kwa Wataalamu katika Fonimu Ambatano na Mpumuo .......... 37

**2.8.1 Kutofautiana kwa Fonimu Ambatano Ng'ong'o [ mb, nd, ng, nj ] .......... 37**

**2.8.2 Kutofautiana kwa Wataalamu katika Fonimu Konsonanti Ambatano [ kh, nz, zy, mp, nt, nk, mw, chw, ñ, ʤ, nw ] .......... 40**

**2.8.3 Kutofautiana kwa Fonimu Mpumuo [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, ʧh ] .......... 42**

**2.8.4 Kutofautiana kwa Fonimu Irabu refu [ aa, ee, ii, oo, uu ] .......... 44**

**2.9 Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake katika Lugha Sanifu za Kiingereza,** Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania .......... 46

2.10 Pengo la Utafiti .......... 50

2.11 Nadharia ya Utafiti .......... 51

**2.11.1 Nadharia ya (Lyons, (1968) Lugha ni Umbo-Sauti Maumbo Kimatumizi 52**

**2.11.2 Kanuni ya Trubetzkoy (1939/1969) ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili .......... 55**

2.12 Dhana na Sifa ya Jozi Sahili .......... 57

2.13 Sifa Bainifu za Fonimu .......... 58

2.14 Hitimisho .......... 58

**SURA YA TATU .......... 60**

**MBINU ZA UTAFITI .......... 60**

3.1 Utangulizi .......... 60

3.2 Eneo la Utafiti .......... 60

3.3 Mpango wa Utafiti .......... 62

3.4 Sampuli ..... 62

**3.4.1 Usampulishaji ..... 63**

**3.4.2 Taarifa za Wasailiwa ..... 66**

3.5 Mbinu za Ukusanyaji Data ..... 69

**3.5.1 Ukusanyaji Data kwa Usaili wa Hojaji ..... 70**

**3.5.2 Ukusanyaji Data kwa Usaili wa Mahojiano ..... 71**

**3.5.3 Ukusanyaji Data kwa Usomaji wa Nyaraka ..... 71**

3.6 Mbinu za Uchanganuzi wa Data ..... 72

3.7 Uthibitisho wa Data Zilizokusanywa ..... 72

3.8 Maadili ya Utafiti ..... 72

3.9 Hitimisho ..... 74

**SURA YA NNE ..... 75**

**UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA ..... 75**

4.1 Utangulizi ..... 75

4.2 Uwasilishaji na Uchanganuzi wa Data ..... 75

**4.2.1 Swali la 1 la Usaili wa Hojaji na Mahojiano kuhusu Sababu za Wataalamu Kutofautiana katika Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake ..... 77**

4.2.1.1 Swali la 1 la Usaili wa Hojaji kuhusu Sababu za Wataalamu Kutofautiana katika Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake ..... 80

**4.2.2 Swali la 2 la Hojaji kuhusu Isharasauti Ambatano Ng’ong’o na Mpumuo kama ni Fonimu au si Fonimu ..... 84**

4.2.2.1 Hoja za Isharasauti Ambatano Ng’ong’o na Mpumuo kama ni Fonimu

au si Fonimu ........................................................................................ 85

**4.2.3 Swali la 2 la Mahojiano kuhusu Idadi na Aina ya Fonimu za Lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania .......................... 901**

**4.2.4 Uthibitisho wa Kanuni ya Kisayansi ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili Inavyobainisha Idadi ya Fonimu za Kiswahili sanifu ................................ 93**

4.2.4.1 Matokeo ya Matumizi ya Kanuni ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili .......... 102

**4.2.5 Uchunguzi wa Zaida wa Utafiti kuhusu Aina za Fonimu za Kiswahili sanifu.......................................................................................... 108**

**4.2.6 Swali la 3 la Hojaji: Athari za Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na Viashiria Vyake ………………………………………………………… 114**

**4.2.6.1 Swali la 3 la Mahojiano: Athari za Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na Viashiria Vyake ………………………………………………………… 114**

**4.2.7 Swali la 4 la Hojaji na Mahojiano Kuhusu Mapendekezo ya Nini Kifanyike ili Kurekebisha Tatizo la Kuhitalifiana …………………………………… 120**

4.2.7.1 Kulingana kwa Uwasilishaji na Uchanaganuzi wa Data za Hojaji na Majadiliano...................................................................................... 125

4.2.8 Kulingana kwa Uwasilishaji na Uchanaganuzi wa Data za Hojaji na Majadiliano...................................................................................... 125

4.3 Hitimisho.......................................................................................... 125

**SURA YA TANO ........................................................................................ 127**

**MATOKEO, MJADALA NA MCHANGO WA UTAFITI .................................... 127**

5.1 Utangulizi ........................................................................................ 127

5.2 Matokeo ya Utafiti kwa Jumla ........................................................ 128

**5.2.1 Matokeo ya Lengo Mahsusi la Kwanza ....................................... 128**

**5.2.2 Matokeo ya Lengo Mahsusi la Pili ............................................... 131**

**5.2.3 Matokeo ya Lengo Mahsusi la Tatu ............................................ 133**

5.3 Mchango wa Utafiti ......................................................................... 134

5.4 Hitimisho ........................................................................................ 136

**SURA YA SITA ..................................................................................... 137**

**HITIMISHO, MAPENDEKEZO NA MAONI ......................................... 137**

6.1 Utangulizi ........................................................................................ 137

6.2 Hitimisho ........................................................................................ 137

6.3 Mapendekezo .................................................................................. 138

6.4 Maoni ya Mtafiti .............................................................................. 140

**MAREJEO ............................................................................................. 142**

**VIAMBATANISHO ................................................................................ 160**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Nam.1.1: Wataalamu Walivyotofautiana sana katika Kubainisha Idadi ya Fonimu …… …………………………………………………...6

Jedwali Namba 1.2: Wataalamu Walivyotofautiana katika Viashiria vya Fonimu Konsonanti [ ch, mb, nd, ng, nj ] na Fonimu Irabu [ a, e, i, o, u ]....... 9

Jedwali Nam. 2.1: Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake katika Lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania ....................................... 47

Jedwali Nam. 2.2: Viashiria vya Fonimu za Lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na kihispania Kimatumizi .................................................... 49

Jedwali Nam. 3.1: Sampuli ya Wasailiwawa Usaili wa Hojaji....................................... 65

Jedwali Nam.3.2: Wasailia Walioteuliwa kwa Kigezo cha Jinsi.................................... 67

Jedwali Nam. 4.1: Isharasauti Ambatano Ng’ong’o na Mpumuo ni Fonimu au si fonimu .............................................................................................. 84

Jedwali Nam. 4.2: Idadi na Aina ya Fonimu za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania....................................................................... 911

Jedwali Nam. 4.3: Irabu za Kiarabu.................................................................................. 92

Jedwali Nam. 4.4: Fonimu Konsonanti za Kiswahili sanifu........................................ 103

## ORODHA YA GRAFU

Grafu Nam 4.1: Majibu ya Wasailiwa wa Hojaji kuhusu Sababu za Wataalamu Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake........................ 78

Grafu Nam. 4.2: Majibu ya Wasailiwa wa Mahojiano kuhusu Sababu za Wataalamu Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake ..... 81

Grafu Nam. 4.3: Hoja za Wasailiwa Waliokubali Isharasauti Ambatano na Mpumuo ni Fonimu ........................................................................................................ 86

Grafu Nam.4.4: Hoja za Waliokataa kwamba Isharasauti Ambatano na Mpumuo si Fonimu ........................................................................................ 88

Grafu Nam. 4.5: Majibu ya Wasailiwa wa Hojaji kuhusu Athari za Kutofautiana Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake ............................................................ 115

Grafu Nam. 4.6: Majibu ya Wasailiwa wa Mahojiano kuhusu Athari za Kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake ............................................. 118

Grafu Nam. 4.7: Mapendekezo ya Wasailiwa wa Hojaji kuhusu Nini Kifanyike ili Kurekebisha Tatizo la Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na viashiria vyake ........................................................................................ 121

Grafu Nam. 4.8: Mapendekezo ya Wasailiwa wa Mahojiano kuhusu Nini Kifanyike ili Kurekebisha Tatizo la Kutofautiana ................................................. 123

## ORODHA YA MICHORO

Mchoro Nam. 2.1: Alasauti za Kutamkia Fonimu za Lugha ........................................... 22

Mchoro Nam 2.2: Maandishi ya Kikabari ........................................................................ 27

Mchoro Nam. 2.3: Vipashio vya Lugha ni Umbo-Sauti Maumbo .................................. 55

Mchoro Nam. 4.1: Fonimu Irabu za Kiswahili Sanifu.................................................... 104

## ORODHA YA VIAMBATANISHO

Kiambatanisho cha 1: Vipengele vya Kilughawiya Vilivyobainishwa ....................... 160

Kiambatanisho cha 2: Usaili wa Hojaji kwa Wanafunzi na Wahadhiri wa Kiswahili .. 161

Kiambatanisho cha 3: Usaili wa Mahojiano kwa Wahadhiri wa Lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania ................................. 164

Kiambatanisho cha 4: Wataalamu Walivyowasilisha Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake katika Kiswahili Sanifu ............................................................ 166

Kiambatanisho cha 5: Wataalamu Walivyowaslisha Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake Lugha Sanifu za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihipania ....................................................................... 174

Kiambatanisho cha 6: Ramani ya Eneo la Asili ya Lugha ya Kiswahili Sanifu Afrika Mashariki ...................................................................... 191

Kiambatanisho cha 7: Ramani ya Eneo la Utafiti ......................................................... 192

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| AKIKI | : | Alfabeti za Kifonetiki za Kimataifa |
| BAKITA | : | Baraza la Kiswahili la Taifa Tanzania |
| BAKIZA | : | Baraza la Kiswahili la Zanzibar |
| KAKAMA | : | Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki |
| SKILUKI | : | Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni |
| SUZA | : | The State University of Zanzibar |
| ZU | : | Zanzibar University |
| SU | : | Sumait University |
| SW | : | Sub’haanahu wa Taala |
| MNMA | : | Mwalimu Nyerere Memorial Academy |
| Nam. | : | Nambari |
| TATAKI | : | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| TAKIKI | : | Tafsiri ya Kiswahili kutoka Kiingereza |

# OORDHA YA ALAMA

| | | |
|---|---|---|
| Ir | : | Irabu |
| Juz. | : | Juzuu |
| Kn | : | Konsonanti |
| Kn + Ir | : | Konsonanti na Irabu |
| kur | : | Kurasa |
| taz. | : | Tazama |
| uk. | : | Ukurasa |
| $ | : | Silabi |
| ͡ | : | Isharasauti moja kimatamshi ya kifonetiki inayowakilisha herufi mbili za kimaandishi ya kiotografia. Mfano [ ɣ ] na [ g͡h ]. |
| $^h$ | : | Mpumuo |
| [ ] | : | Mabano yanayowakilisha alama za isharasauti kifonetiki |
| / / | : | Mabano yanayowakilisha alama ya fonimu za lugha mahsusi. |
| | : | Kishiria cha irabu ya fat'ha (a) ya Kiarabu hukaa juu ya herufi. |
| | : | Kiashiria cha irabu ya kasra (i) ya Kiarabu hukaa chini ya herufi. |
| | : | Kiashiria cha irabu ya dhuma (u) ya Kiarabu hukaa juu ya herufi. |
| | : | Kiashiria cha irabu ya sukuun (') ya Kiarabu hukaa juu ya herufi. |
| | : | Fat'haten sawa na fat'ha mbili juu ya herufi. |
| | : | Kasraten sawa na kasra mbili chini ya herufi. |
| '' | : | Dhumaten sawa na dhuma mbili juu ya herufi. |

## FASILI ZA ISTILAHI ZILIZOTUMIKA

**Alifu:** Utamkwaji wa irabu **[ a, e, i, o, u ]** kwa kutoa hewa nyepesi yenye sauti kali isiyozuiwa kwa mzuio wowote katika chemba zote za matamshi. Sauti hizi aghlabu hutokea baada ya konsonanti au irabu. Mfano: uz**a**, aj**e**, l**ia**, s**o**m**o**, ut**ii, ai**ng**ie**.

**Athari:** Upungufu unaotokana na kutofautiana kwa wataalamu katika idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonololojia ya Kiswahili sanifu.

**Fonimu Ambatano:** Fonimu yenye umbo la isharasauti mbili kimaandishi ya Kiotografia lakini ni umbo moja kimatamshi ya kifonetiki. Mfano: [ mb, sh, gh, ny, nj, ng, nd, th, dh, ng' ] (kiotografia) na [ ɓ, ʃ, ɣ, ɲ, ή, ɠ, ɗ, θ, ð, ŋ ] (kifonetiki).

**Fonimu Sahili:** Fonimu ya umbo moja tu kimatamshi na kimaandishi ya kiotografia. Mfano: / b, h, g, s, n, y, **j**, z /.

**Hamza:** Utamkwaji wa irabu [ a, e, i, o, u ] zinaposimama kuwa silabi zinazojitegemea kwa kutoa hewa kwa nguvu inayosababisha sauti kali inayozuiwa katika chemba cha glota. Irabu hizi aghlabu hutokea mwanzo wa neno. Mfano: **A**li**,** **e**limu, **i**li, **o**mba na **u**di.

**Idadi ya Fonimu:** Jumla ya fonimu zote zenye umbo la konsonsnti au irabu katika muundo wa fonimu pekee au fonimu ambatano zinazotumika kuunda maneno katika lugha ya Kiswahili.

**Isharasauti:** Ni sauti za lugha zenye kuwakilisha fonimu.

**Kibantu:** Kikundi cha lugha zinazofanana kimuundo, kingeli, na kiviambishi zinazozungumzwa kusini mwa jangwa la Afrika kama Kijaluo, Kibaganda, Kihaya, Kizulu na Kiswahili.

**Uchunguzi:** Uangalizi makini wa tatizo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

**Uchanganuzi:** Uchambuzi yakinifu wa taarifa au data za sababu na athari za Kiswahili sanifu kwa ajili ya kutoa ufafanuzi au tafsiri kubalifu.

**Matamshi Fasaha:** Matamshi ya herufi au silabi au maneno yanayotamkwa kwa usahihi kisarufi bila ya kuwa na makosa au ukaraha au uchukivu kulingana na kanuni za utamkaji zinazokubaliwa na wazawa au wajuzi wa lugha fulani.

**Nitoe Nikutoe:** Kanuni ya kisayansi ya kubainisha fonimu za lugha katika Jozi Sahili ya maneno ya lugha fulani. Mfano wa Jozi Sahili [ zangu: langu ] Katika jozi hii ikitumika kanuni ya Nitoe Nikutoe kuna ishsarasauti hutoana na kubaki isharasauti moja katika kila neno ambazo huwa ni fonimu. Mfano:

| | | | |
|---|---|---|---|
| [ z | a | ng | u ] |
| [ l | a | ng | u ] |
| [ t | a | ng | u ] |

Isharasauti [ a, ng, u ] zimetoana na kubakia isharasauti **[ z, l, t ]** ambazo ni fonimu za Kiswahili sanifu.

**Uswahilini:** Eneo la pwani ya Afrika Mashariki ikijumisha sehemu za Mogadishu, Lamu, Siu, Pate, Mombasa (Kaskazini), Tanga, Kilwa, Mafia Dar es Salaam (kusini), Unguja na Pemba (Mashariki).

**Kutofautiana:** Hali ya kuzuka kwa utata wa kutolingana na kutoelewana katika jambo fulani linaloshindikana utatuzi au utambuzi wake.

**Viashiria:** Viwakilishi vya fonimu kimaandishi ya kifonetiki au kiotografia.

Mfano: [ mv ] kiotografia na [ ɱ ] kifonetiki**.**

**Waswahili:** Wazawa wa Upwa wa Afrika Mashariki ambao lugha yao ya uzawa ni Kiswahili na utamaduni wao ni wa Kiswahili wenye athari ya mfumo wa maisha ya uislamu katika hali za imani upole, unyenyekevu, ukarimu na umoja.

**Wazawa:** Watu waliozaliwa na lugha yao fulani ambao wanaisema au kuizungumza kwa usahihi na ufasaha.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii inahusu ufafanuziwa vipengele vya awali ambavyo hutumika vikiwa ni muongozo wa kufanya utafiti wa kitaaluma. Vipengele hivyo ni usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, pengo la utafiti, vikwazo vya utafiti, muundo wa tasnifu na hitimsho.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Kiswahili ni moja kati ya lugha za asili ya upwa wa Afrika Mashariki kutoka mji wa Barawa nchini Somalia hadi mji wa Sofala nchini Msumbiji, Visiwa vya Lamu, Pate, Siu, nchini Kenya, na Visiwa vya Mafia, Kilwa, Unguja na Pemba nchini Tanzania (Chiraghdin na Mnyampala, 1977:25, Maganga, 1997:31, Kihore na wenzake, 2002:51) pia taz. Kiambatanisho cha 4. Kwa mujibu wa Marco-Polo[1] mchunguzi wa Kiitaliana, Kiswahili kilikuwepo Afrika Mashariki kabla ya ujio wa wageni mnamo karne ya kumi (miaka ya 1100-1166). Ushahidi wa kuwepo kwa Kiswahili katika kipindi hicho ni maandishi yaliyogunduliwa kama *Unguja, kikonde* na *mkono wa tembo*, maneno ambayo hadi leo yanatumika katika Kiswahili. Baadhi ya maneno ya Kiswahili yaliyotumika kusemwa wakati huo, si sawasawa na maneno ya Kiswahili yanayosemwa wakati wa sasa.

[1] Katika https://www.thecollector.marco-polo-discoveries

Bali ni Kiswahili kilichohusiana na lugha za Kibantu ambacho baadhi ya maneno yake kama hayo yaliyobainishwa hapo juu yanatumika hadi sasa.

Utafiti huu uliazimia kuchunguza sababu na athari za kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Usuli hasa ulioibua mada ya utafiti huu, umetokana na kuwagundua wataalamu zaidi ya 35 waliotofautiana katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Wataalamu hao wamewasilisha idadi tafautitafauti za fonimu za Kiswahili sanifu kama vile: 27, 28, 29, 30, 31, 32, 33, 34, 35, 36, 37, 38, 40, 41, 42, 45, 58. Wataalamu hao pia waliwasilisha viashiria tafautitafauti kama vya kiotografia, kifonetiki, herufi kubwa na herufi ndogo. Kutokana na kugundua tatizo hilo, utafiti huu ndipo ulipovumbua nini cha kukichuguza ambacho ndicho kilichoitwa mada ya utafiti huu ambayo ni Uchunguzi wa Sababu na Athari za Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake katika Kiswahili sanifu. Tatizo hili lilitarajiwa kubaini ukweli wa sababu na athari za kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake kutokana na wataalamu zaidi ya 35 waliowasilisha idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu. Tatizo hili linaruhusu kufanyiwa utafiti na kulichunguza kwa umakini na kubaini matokeo halisi ya data zake (Alston na Bowles, 2007:27). Hii ina maana kwamba, suala hili linaweza kuchunguzwa kwa njia ya uchanganuzi wa maandishi tangulizi ya taaluma hii pamoja na majibu ya Wasailiwa na kuyapima kwa njia ya tathmini ya asilimia pamoja na kuyachunguza kwa njia ya ubora wa majibu ya Wasailiwa hao. Utafiti huu ulikusudia utapogundua sababu na athari za kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu, litafutwe suluhisho sahihi na lenye manufaa kwa lengo la wataalamu kuepukana na kuzidi kuendelea na suala la kutofautiana katika idadi

ya fonimu na viashiria vyake katika taaluma ya fonolojia ya Kiswahili sanifu (Williams na wenzake, 2010:1).

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Uzoefu unaonesha kwamba, baada ya mchakato wa usanifishaji wa lugha ya taifa katika nchi au taifa fulani, lugha sanifu hutumiwa na taasisi za serikali, kama mahakama, skuli, viwanda na vyombo vya habari kwa mawasiliano rasmi ya kitaifa na kimataifa. Kwa mkabala huo, Kiswahili sanifu nacho, kikiwa ni lugha ya asili ya Afrika Mashariki kwa sasa imebahatika kuwa lugha maarufu na yenye mawanda mapana ya matumizi yake kijamii, kisiasa, kielimu, kimazingira, kisayansi na ufundi takriban duniani kote.

Umaarufu wa Kiswahili hivi sasa unatokana kuwa, kinazungumzwa kikiwa lugha sanifu, lugha rasmi na lugha ya taifa nchini Tanzania na Kenya. Pia, Kiswahili kinazungumzwa kikiwa lugha rasmi nchini Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi. Aidha, Kiswahili sanifu kinazungumzwa kikiwa lugha ya kimataifa duniani katika nyanja za kufundishia, kufundishwa, kutangazia na mawasiliano rasmi katika vyombo vya habari vikiwemo redio, televisheni, magazeti majarida, vipeperushi na mabango. Zaidi ya matumizi hayo, Kiswahili kimepata umaarufu kwa kupewa siku yake ya kimataifa na Shirika la UNESCO[2] ambayo ni tarehe 7 mwezi wa 7 kila mwaka. UNESCO ilitoa tangazo hilo siku ya Jumatano, tarehe 23 mwezi wa 11 mwaka 2021 katika mkutano wake mkuu kwa nchi wanachama wa kila mwaka huko Paris nchini Ufaransa.

---

[2] Katika *https://news.un.org/sw/story/2021/11/1132522*

Kwa mujibu wa Dafina ya Kiswahili[3], Kiswahili hivi sasa ni moja kati ya lugha za kiasili katika bara la Afrika iliyopata hadhi ya kuwa lugha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na pia ni lugha ya Bunge la Afrika. Ni lugha moja inayozungumzwa na watu wengi wanaokadiriwa kufikia zaidi ya milioni 200 na kupata nafasi ya saba katika lugha za kimataifa ikitanguliwa na Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno, Kihipania na Kichina (Juma na Mushi, 2019).

Pamoja na umaarufu huo wa matumizi ya Kiswahili sanifu kwa Afrika Mashariki hususan na duniani kwa jumla, bado kuna dhana ya kwamba, Kiswahilli sanifu kina matatizo katika baadhi ya maeneo yake mbalimbaali yakiwemo eneo la taaluma ya fonolojia yake hasahasa kwenye taaluma za matamshi na maandishi kwa kutumia fonimu zake zenye matatizo ya kiidadi na aina zake (Kihore na wenzake, 2001:22-25, Mgullu, 2001:66-69, King'ei na Musau, 2002:12, Khamis, 2011:20-21).

Zaidi ya wataalamu hao, Ligami, (2002:36), yeye amebainisha matatizo ya Kiswahili sanifu wakati huu katika maeneo ya matamshi na maandishi ya fonimu zake kwa pale aliposema kwamba, kuna malalamiko kuhusu wanafunzi wengi wanaojiunga na vyuo vikuu kutoweza kuandika lugha sahihi na fasaha kutokana na matatizo ya lugha ya kwanza, makosa ya kimatamshi, mazingira, sarufi, namna ya kufundisha na matatizo ya kijamii.

---

[3] Katika https://sluhwago.blogspot.com/

Pia, Chomsky na Halle (1968) wametanabahisha juu ya kutofautiana kwa Kiswahili sanifu katika matamshi na maandishi sahihi kuwa ni tatizo la kuzingatiwa sana wakati huu, kwani jukumu kuu la lugha sanifu ni kuondoa tofauti za kimatamshi na kimaandishi kwa kuwafanya wazungumzaji wake wawe na njia moja ya kutamka maneno ya lugha hiyo kwa usahihi kulingana na idadi halisi ya fonimu za lugha hiyo.

Naye Joseph (2004:74) alihoji juu ya kutofautiana kwa maandishi ya Kiswahili sanifu kwa kusema kuwa maandishi ya Kiswahili sanifu mara nyingi huwa na matatizo sugu yanayopotosha usahihi na ufasaha wa matamshi yake.

Sambamba na wataalamu hao, kugundua mtatizo ya matamshi na maandishi katika Kiswahili sanifu, bado wataalamu hao hawjazungumzia suala la kutofautiana kwa idadi ya fonimu katika taaluma ya fonolojia ya Kiswahili sanifu. Uchunguzi umewagundua wataalamu zaidi ya 35 waliotofautiana sana katika ubainishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Hali ya kutofautiana kwa ubainishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake miongoni mwa wataalamu mbalimbali wa lugha hii ni kama inavyodhihirika katika majedwali yafuatayo:

**Jedwali Nam.1.1: Wataalamu Walivyotofautiana sana katika Kubainisha Idadi ya Fonimu**

| Namba | Mtaalamu | Idadi ya Fonimu | Konsonanti | Irabu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Akidah (2013:3-4) | 30 | 25 | 5 |
| 2. | Ager (2014)[4] | 38 | 33 | 5 |
| 3. | Angongo katika tuki (1983:62-65) | 42 | 37 | 5 |
| 4. | Ashton (1944:3) | 37 | 32 | 5 |
| 5. | Aswani (1995:43-44) | 34 | 29 | 5 |
| 6. | BAKITA (2017: xiv-xv) | 32 | 27 | 5 |
| 7. | BAKIZA (2010: xi) | 43 | 28 | 15 |
| 8. | Benard (2000:38-44) | 34 | 29 | 5 |
| 9. | Besha (1994:26) | 36 | 31 | 5 |
| 10. | Choge (2009:62-77) | 31 | 26 | 5 |
| 11. | Habwe na Karanja (2004:48-50) | 31 | 26 | 5 |
| 12. | Harris (1951:97-124) | 35 | 30 | 5 |
| 13. | Khamis (2011:19-23) | 58 | 48 | 10 |
| 14. | Kihore (1996:39-40) | 28 | 23 | 5 |
| 15. | Kihore na wenzake (2001:22-25) | 30 | 25 | 5 |
| 16. | King'ei na Musau (2002:3) | 29 | 24 | 5 |
| 17. | Lodhi (1976:1-2) | 44 | 34 | 10 |
| 18. | Maganga (1991:270) | 30 | 25 | 5 |
| 19. | Massamba na wenzake (2004:39-41) | 32 | 27 | 5 |
| 20. | Matinde (2012:53) | 30 | 25 | 5 |
| 21. | Mbaabu (1985:3-8) | 31 | 26 | 5 |
| 22. | Mbunda (1976:129-132) | 41 | 32 | 9 |
| 23. | Mfaume (1985:18-19) | 30 | 25 | 5 |
| 24. | Mgullu (2001:66–69) | 31 | 26 | 5 |
| 25. | Mohammed (1986:2) | 27 | 22 | 5 |
| 26. | Mutahi (1990:44-47) | 33 | 28 | 5 |

[4] Katika https://www.omniglot>presentations

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 27. | Mwinza (2014:8)[5] | 34 | 29 | 5 |
| 28. | Nchimbi (2008:36-38) | 34 | 29 | 5 |
| 29. | Njogu na wenzake (2006:8-10) | 33 | 28 | 5 |
| 30. | Paneli la Kiswahili (1999-2001)[6] | 31 | 26 | 5 |
| 31. | Polome (1967:38-39), | 35 | 30 | 5 |
| 32. | Russell (2003: xiv-xvii) | 36 | 30 | 10 |
| 33. | TATAKI (2013: xvi) | 35 | 25 | 10 |
| 34. | Whiteley (1956:8) | 38 | 33 | 5 |
| 35 | Zawawi (1971:5-7) | 31 | 26 | 5 |

**Chanzo: Data za Wataalamu, 2020**

Jedwali linabainisha wataalamu zaidi ya 35 namna walivyotofautiana katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu za Kiswahili sanifu. Baadhi ya wataalamu kama Akidah, (2013:3-4), Mfaume (1985:18-19), Maganga (1991:270), Matinde (2012:53), King'ei na Musau (2002: 3 & 8) na Massamba na wenzake (2004:39-41) wana jumla moja ya fonimu 30, zikiwemo fonimu konsonanti 25 na fonimu irabu 5. Hata hivyo, bado kunadhihirika kutofautiana kwa wataalamu wengine kwa kutokuwa na idadi moja ya fonimu hizo hususan idadi ya konsonanti. Tofauti za wataalamu hao, kama zilivyojitokeza katika jedwali hilo, ni ushahidi tosha kuwa, kuna kutofautiana kwa idadi ya fonimu katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

[5] Katika http://.blogspot.com. 2014/08/fonetiki-au-utamkwaji-wa-sauti-fonimu.html.

[6] Katika https://swa.gafkosoft.com/

Kwa upande wa ushahidi wa kutofautiana kwa wataalamu hawa katika ubainishaji wa viashiria vya fonimu ni kama inavyobinika katika jedwali lifuatalo:

## Jedwali Namba 1.2: Wataalamu Walivyotofautiana katika Viashiria vya Fonimu Konsonanti [ ch, mb, nd, ng, nj ] na Fonimu Irabu [ a, e, i, o, u ]

| Namba | Wataalamu | Viashiria vya Fonimu Konsonanti |
|---|---|---|
| 1. | Ashton (1944: 3), Kihore (1996: 39-40), Zawawi (1971: 5-7), Benard (2000: 38-44), Mohammed (1986: 2), King'ei na Musau (2002:3), Russell (2003: xiv-xvii), Paneli la Kiswahili (1999-2017), Choge (2009: 62-77) na Whiteley, (1956:8) | [ ch ] |
| 2. | Akina Harris (1951:97-124), Lodhi (1976:1-2), Mbunda (1976:129-132), Mbaabu (1985:3-8), Mutahi (1990:44-47), Mgullu (2001: 66–69), Habwe na Karanja (2004: 48-50), Khamis (2011:19-23), Matinde (2012: 53), Saimon (2014) | [ ʧ ] |
| 3. | Polome (1967:38-39), Mfaume (1985:18-19), Besha (1994:26), Aswani (1995:43-44), Kihore, Massamba na Msanjila (2004: 39-41), Njogu, Mwihaki na Buliba (2006: 8-10), BAKIZA (2010: xi) | [ č ] |
| 4. | Angongo katika TUKI (1983:62-65), Maganga (1991: 270), Kihore, Massamba na Msanjila (2001: 22-25), Nchimbi (2008: 36-38) na Peter (2014:8) | [ c ] |
| 5. | Whiteley (1956: 8), Mbunda (1976: 129-132), Angongo katika TUKI (1983: 62-65),na Benard (2000: 38-44) | [ mb, nd, ng, nj ] |
| 6. | Lodhi (1976: 1-2) | [ ъ, ƌ, ɠ, ʤ ] |
| 7. | Aswani (1995: 43-44) | [ m͡b, n͡d, n͡j, n͡g ] |
| 8. | Khamis (2011: 19-23) na Njogu, Mwihaki na Buliba (2006: 8-10), Ager (2014) | [ mb, ɲd, ŋg, ɲj ] |
| 9. | Nchimbi (2008: 36-38) | [  ] |
| 10. | Volger, (1976) katika Nchimbi (1992) | [ √b, √d, √g, √ɟ ] |
| 11. | Batibo, (1981), Bouquiaux na Cloarec-Heiss, (1975), Maganga, (1979) na Polome, (1967) | [ mb, nd, ng, nɟ ] |
| | Wataalamu | Viashiria vya Fonimu Irabu |
| 1. | Ashton (1944: 3) | [ A, E, I, O, U ] |
| 2. | Harris. (1951: 97-124), Whiteley (1956: 8), Kihore (1996: 39-40), Polome (1967: 38-39), Zawawi (1971: 5-7), Angongo katika TUKI (1983: 62-65), Mbaabu (1985: 3-8), Mfaume (1985: 18-19), Mohammed (1986: 2), Matinde (2012: 53) na Peter (2014: 8) | [ a, e, i, o, u ] |
| 3. | Lodhi (1976: 1-2), Mbunda (1976: 129-132), Mutahi (1990: 44-47), Maganga (1991: 270), Mgullu (2001: 66–69), Habwe na Karanja (2004: 48-50), Khamis (2011: 19-23), na Saimon (2014) | [ a, ɛ, i, ɔ, u ] |
| 4. | Lodhi (2000: ix) | [ ā, ã, ė, ō, ū ]. |
| 5. | Russell (2003: xiv-xvii) | [ aa, ee, ii, oo, uu ] |
| 6. | BAKIZA (2010: xi), Khamis (2011:19-23), Lodhi (1976:1-2), Mbunda (1976:129-132) na TATAKI (2013: xvi) | [ a:, ɛ:, i:, ɔ:, u: ] |

**Chanzo: Data za Wataalamu, 2020**

Jedwali linabainisha namna wataalamu walivyotafautiana katika kuwasilisha viashiria tofaututofauti vya fonimu konsonanti na irabu za Kiswahili sanifu. Kwa jumla majedwali haya yanatuhakikishia ni kwa kiasi gani wataalamu hao walivyotofautiana katika uwasilishaji wao wa fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

### 1.3.1 Maswali kuhusu Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake

Suala la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika lugha moja ya Kiswahili kama ilivyobainiswa lina athari gani kwa wanafunzi, wahadhiri na wasomi wanapopitia marejeo ya wataalamu hao? Hali hii ndio iliyosababisha tujiulize maswali yafuatayo:

i) Sababu gani zilizowafanya wataalamu zaidi ya 35 watofautiane sana katika kubainisha idadi ya fonimu za Kiswahili sanifu kama: 27, 28, 29, 30, 31, 32, 33, 34, 35, 36, 37, 38, 40, 41, 42, 45, 58 na pia watofautiane katika kubainisha viashiria kama: vya kiotografia, vya kifonetiki, vya herufi kubwa na vya herufi ndogo?

ii) Je, wataalamu hao zaidi ya 35 wametumia vigezo gani vya ubainishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake hadi kukazuka kutofautiana kama huko?

iii) Je, wataalamu hao zaidi ya 35 walipoandika kuhusu idadi ya fonimu walibainisha kasoro walizozigundua hadi na wao wakaongeza au kupunguza idadi walizozibainisha?

iv) Je wataalamu hawa zaidi ya 35 walipoandika kuhusu idadi ya fonimu na viashiria vyake walishauriana na wanataaluma wengine ili kupata mawazo yao au walifanya kazi hiyo kipekeepekee?

v) Je, maandishi ya wataalamu hao yalisimamiwa na vyombo vinavyosimamia Kiswahili kama KAKAMA katika uwasilishajii wao wa idadi ya fonimu na viashiria vyake?

Kutokana na maswali haya ambayo hayakupata majibu, utafiti huu ndipo ulipovumbua malengo mahsusi na maswali yake ili kuyafanyia kazi katika utafiti huu. Baadhi ya wataalamu hao kama Akidah (2013:3-4), Maganga (1991:270), Massamba na wenzake (2004:39-41), King'ei na Musau (2002:3-8) na Mfaume (1985:18-19) wana idadi sawa ya jumla ya fonimu 30, zikiwemo fonimu konsonanti 25 na fonimu irabu 5. Hata hivyo, bado kunadhihirika kutofautiana kwa wataalamu wengine kwa kutokuwa na idadi moja ya fonimu na viashiria vyake, hususan idadi ya fonimu konsonanti. Tofauti za wataalamu hao, kama zilivyojitokeza hapo juu, ni ushahidi tosha kuwa wataalamu hawa wametofautiana kwa kiwango kikubwa katika kubainisha idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

Kutokana na tatizo hili la kutofautiana inadhihirika waziwazi kwamba, kuna haja ya kufanya utafiti, kwani hadi sasa, hakuna utafiti mpana[7] na wa kina[8] uliokwishafanywa kuhusu kuchunguza kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili

[7] Tunaposema utafiti mpana tunamaanisha utafiti uliofanywa katika maeneo yote yanayozungumzwa lugha ya Kiswahili, utafiti ambao ungehusisha lugha ya Kiswahili katika vipengele mbalimbali.

[8] Tunapozungumzia utafiti wa kina tunamaanisha utafiti ambao ungejikita katika kuchunguza fonolojia ya Kiswahili kwa undani

sanifu. Kutokana na hali hiyo, kuna umuhimu wa kuendelea kufanya utafiti katika lugha ya Kiswahili ili pamoja na mambo mengine, kuchunguza matokeo na mchango wa utafiti huu ili kuziba pengo hilo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu na malengo mahususi kama ifuatavyo:

### 1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza sababu na athari za kutofautiana kwa wataalamu katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu

### 1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti

Ili kufanikisha lengo kuu la utafiti huu, malengo mahususi yafuatayo yalizingatiwa kufanyiwa kazi:

vi) Kubainisha sababu za kutofautiana kwa wataalamu katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

vii) Kudhihirisha athari za kutofautiana kwa wataalamu katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

viii) Kupendekeza njia za kurekebisha tatizo la kutofautiana kwa wataalamu katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

### 1.4.3 Maswali ya Utafiti

Ili kuyafikia malengo hayo, utafiti huu ulibuni na kuyafanyia kazi maswali yafuatayo:

ix) Kuna sababu gani za kutofautiana kwa wataalamu katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu?

x) Kuna athari gani za kutofautiana kwa wataalamu katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu?

xi) Kuna njia gani za kurekebisha tatizo la kutofautiana kwa wataalamu katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Kutokana na utafiti kuwa ni nyenzo ya kutatua matatizo katika jamii, inadhihirika kuwa matokeo ya utafiti huu yatakuwa ni taaluma mpya miongoni mwa jumla ya tafiti zitakazoazimia kudhihirisha sababu na athari za kutofautiana kwa wataalamu katika vipengele vya fonolojia ya Kiswahili sanifu. Pili, ni umuhimu wa kuwadhihirishia wanafunzi na wahadhiri wa vyuoni kwamba, Kiswahili sanifu kinaweza kuwasilisha idadi ya fonimu na viashiria vyake kwa kutumia kanuni ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili. Tatu, kuonesha namna taaluma ya fonolojia ya Kiswahili sanifu inavyopingana na lugha maarufu za kimataifa katika uwasilishwaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake. Nne, kuweka muwafaka wa tatizo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Tano, Kuibua marejeo kwa wanafunzi, wahadhiri, wataalamu na wasomi wa taaluma za lughawiya ya Kiswahili sanifu. Sita, kuwakumbusha watunga sera ya lugha serikalini, Mabaraza ya Kiswahili pamoja na Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki kuzingatia sheria na kanuni za kuwepo kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu kama zilivyo lugha za kimataifa za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihipania. Saba, inatarajiwa sana

kuwa matokeo ya utafiti huu yatawawezesha wasomaji kumaizi umuhimu wa kutotafautiana kwa idadi ya idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Nane, Utafiti huu utaiweka taaluma ya fonolojia ya Kiswahili sanifu katika ramani ya fonolojia ya lugha za kimataifa ulimwenguni.

Umuhimu uliobainishwa hapo, unakipa Kiswahili sanifu hadhi na nafasi yake ya kuwa ni lugha maarufu kwa watu wote kuliko lugha za kiasili katika ukanda wa Afrika Mashariki, Afrika Kati na Afrika Kusini. Katika ufahamu huo, wanafunzi, wahadhiri, wataalamu na wasomi wa lughawiya ya Kiswahili vyuoni, wataweza kuwa makini katika kuandika machapisho ya makamusi, vitabu na makala katika majarida mbalimbali katika nyanja za sarufi na lughawiya kwa kuzitumia kikamilifu idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza suala la kutofautiana katika idadi ya fonimu na viashiria vyake. Kipengele hiki kilichaguliwa kwa sababu kinakabiliwa na tatizo la wataalamu zaidi ya 35 waliochangia kubainisha idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu na kubainika kutofautiana kiidadi na aina za viashiria taz. Jedwali 1.1. Pia utafiti huu ulichunguza kwa kutumia sampuli ya wahadhiri na wanafunzi wa fonolojia ya Kiswahili sanifu pamoja na wahadhiri wa fonolojia za lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihipania kutoka vyuo vikuu vine vya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU), Chuo Kikuu cha Sumait (SU) na Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere Memorial Academy (MNMA) ambamo ndimo mlitoka sampuli ya jumla ya Wasailiwa 115. Mawanda ya utafiti huu

yamebanika kuwa madogo kutokana na kwamba mada yake ni ya kitaalamu katika vyuo vikuu vine tu vilivyoteuliwa kutoka Unguja, Zanzibar.

## 1.7 Vikwazo vya Utafiti

Uzoefu unaonesha kuwa vikwazo katika utafiti ni yale matatizo yaliyojitokeza katika mchakato mzima wa utafiti. Mfano katika hali ya kumpata msimamizi atakayekwenda sambamba na mtafiti katika muda uliopangwa. Kuwapata Wasailiwa wote waliokusudiwa na kuweza kuyajibu maswali yote yaliyowekwa katika usaili wa Hojaji na usaili wa Mahojiano ili kupata taarifa au data kamili. Suala la kuweza kukamilisha kazi kwa muda uliopangwa na hata kupatikana kwa fedha za kutosha za kusafiri Makao makuu ya Chuo huko Dar es Salaam pamoja na kukidhi mahitaji ya utafiti huu kwa mujibu wa bajeti yake. Kwa mujibu wa hali halisi ya utafiti huu, vikwazo vilijitokeza katika muda wa kufanya utafiti huu ni kama vifuatavyo:

Wasailiwa hawakupatikana kwa idadi iliyokusudiwa ya 130 ingawa walipatikana kwa wingi yaani, 115. Mtafiti aliweza kutatua kikwazo cha kuwapata Wasailiwa kwa kuwachagua wahadhiri maalumu katika vyuo vinne na kuwaomba msaada wa kuusambaza usaili wa Hojaji kwa Wasailiwa teule waliokusudiwa na kuzisimamia katika kujazwa na baadae kuukabidhi kwa mtafiti kwa kazi ya uchanganuzi. Utafiti huu ulichukua muda mrefu mno kutokana na suala la kumkosa msimamizi wa kwanza kwa muda wa miaka mine aliposafiri nje ya nchi na akawa hana taaluma ya kutumia kompyuta. Suala la kubadilishiwa wasimamizi kwa kila baada ya muda ambapo kila msimamizi alibainika kuwa na msimamo wake binafsi juu taaluma ya kazi hii nacho kilikuwa kikwazo kikubwa kwa mtafiti. Mikabala ya wasimamizi nalo lilisababisha usumbufu wa kuirejea kazi hii kila mara ili iendane na mitazamo yao. Kupata baadhi ya vitabu rejea, hasa vile

vya wataalamu wa taaluma ya fonolojia ya Kiswahili sanifu wa karibuni mnamo miaka ya 2000 ilikuwa ni shida. Pia suala la kutafsiri kwa Kiswahili vitabu, majarida, mitandao na makala zilizoandikwa kwa Kiingereza ili kupata taarifa sahihi zilizohusiana na utafiti huu ilikuwa ni kikwazo kikubwa. Mtafiti alitumia makamusi ya Kiingereza pamoja na programu ya *translation* katika kompyuta ili kutafsiri kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili (TAKIKI). Kikwazo cha mwisho ni cha kutoonana kwa ukaribu kati ya mtafiti na wasimamizi wake ambao walikuwa mbali naye. Wasimamizi walikuwa wanaishi Dar es Salaam na mtafiti alikuwa anaishi Unguja. Mtafiti ilimlazimu kutumia njia ya kuwasiliana kwa whatsapp katika simu na baruapepe katika kompyuta na kukosa mawasiliano ya ana kwa ana kwa takriban muda wote wa mchakato wa utafiti huu.

## 1.8 Muundo wa Tasnifu

Tasnifu hii ina jumla ya sura sita kuu ambazo kila sura imeundwa na mada pamoja na vipengele vyake mahsusi. Sura ya kwanza inahusu utangulizi. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia cha utafiti huu. Kazi tangulizi za wataalamu mbalimbali pamoja na nadharia ya Lyons (1968) isemayo: Lugha ni Sauti-umbo Maumbo Kimatumizi na Kanuni ya Trubetzkoy (1939/1969) isemayo: Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili ziliwasilishwa. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti. Sura ya nne inahusu uchanganuzi na uwasilishaji wa data za utafiti. Sura hii imechambua data kwa kuchunguza maswali manne ya usaili wa Hojaji na maswali manne ya usaili wa Mahojiano. Sura ya tano imebainisha matokeo na michango ya majibu ya uchanganuzi wa hoja kuhusu kutofautiana kwa wataalamu zaidi ya 35 waliowasilisha idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Pia, sura hii ilichambua majibu ya Wasailiwa

wa usaili wa Hojaji na usaili wa Mahojiano ya ili kuyathibitisha malengo na maswali ya utafiti huu. Sura ya sita inahusu hitimisho, mapendekezo na maoni ya mtafiti.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii kwa ufupi, imedhihirisha kwa uwazi namna wataalamu walivyotofautiana katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Kutokana na kutofautiana huko, imedhaniwa kuwa lazima kuna sababu pia pengine kuna athari za kutofautiana huko kulikozuka. Pamoja hayo sura imonesha malengo mahsusi matatu yaliyochunguzwa kulingana na tatizo la utafiti huu. Umuhimu wa utafiti huu uliobainishwa katika sura hii unatoa matumaini na muelekeo kwa jamii yaani, watumizi wake kutotosheka na usanifu wa lugha uliofanywa tangu mwaka wa 1930 na Wazungu ambao ni wageni wa lugha hii. Wasanifishaji hao walikazia kutokiimarisha, kutokiendeleza, kutokihifadhi na kutokienzi, Kiswahili sanifu katika upungufu na kasoro ya idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu. Kasoro hizo zimeibuliwa kwa ushahidi wa mifano halisi kama ilivyodhihirishwa katika kipengele cha 1.2 cha usuli wa utafiti katika sura hii. Sasa tuangalie sura ijayo yenye ufafanuzi wa kazi tangulizi zinazohusiana na matatizo ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura ya hii inahusu mapitio ya kazi tangulizi juu ya taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Mada ndogo zilizopitiwa ni Dhana ya fonimu, Asili ya fonimu za lugha, Fonimu kuwa kijenzi cha msingi katika lugha, Dhana ya Fonolojia ya Lugha, Usanifishaji wa Kiswahili na kasoro zake, Kutofautiana katika fonolojia ya Kiswahili sanifu, Pengo la utafiti pamoja na nadharia zilizotumika kuongoza uchanganuzi wa data za utafiti huu. Mapitio na uhakiki wa kazi tangulizi za wataalamu wa taaluma ya fonolojia ya Kiswahili sanifu waliogundua suala linalohusiana na kutofautiana katika vipengele mbalimbali vya fonolojia ya Kiswahili sanifu kupitia vitabu, nyaraka na mitandao ni kama ifuatavyo:

## 2.2 Dhana ya Fonimu

Pamoja na maendeleo ambayo mwanadamu ameyafikia kwa sasa katika uandishi na uwasilishaji wa taarifa kwa kutumia lugha, fonimu ndio msingi wa lugha na maandishi ni kiwakilishi tu cha matamshi ya kusemwa. Inaaminika kuwa, lugha ni isharasauti nasibu zenye maana ambazo hutolewa na mwanaadamu tu, peke yake kutokana na maumbile yake na si kiumbe kinginechochote (Mario na Frank, 1954 & Mmallavi, 1977).

Kihistoria, kwa mujibu wa Massamba (2012:25), wazo la istilahi ya fonimu ilibuniwa na Dufriche-Desgenettes mnamo mwaka 1873 kwa maana ya *sauti ya usemaji* bila ya kutumia neno *fonimu.* Neno *fonimu* liliasisiwa na mtaalamu Kruszewiski aliloliita *fonema* neno la Kirusi. Kruszewiski ni mwanafunzi wa de Courtenay ambaye naye pia aliiazima

istilahi ya *fonema* na akaitumia katika insha yake ya "*Athari ya Mkazo katika Ubadilishanaji wa Irabu katika Rig-Veda*" katika mwaka 1879. Kwa kuwa fonimu, ni kijenzi chenye sifa ya kupambanua umbo na maana katika maneno ya lugha fulani, fonimu kwa upande mwingine ina sifa ya kuibua alofoni za maumbo na matamshi tofauti ambayo huwa na sifa ya kutobadilisha maana. Kwa mfano katika Kiswahili kuna maneno **[ t ]** aa na **[ $t^h$ ]** aa. Maneno haya katika Kiswahili sanifu yana maana moja ya ama kifaa kinachotoa muangaza au samaki mwenye umbo bapa na mkia mrefu. Hapa isharasauti **[ t ]** na **[ $t^h$ ]** katika Kiswahili sanifu ni alofoni za fonimu **/ t /** kwa vile isharasauti hizi hazibadilishi matamshi wala maana.

Lakini maneno hayahaya **[t**aa**]** na [ **$t^h$**aa] katika lahaja ya Kiunguja Mjini kila moja yanatamkwa na kutoa maana tafauti yaani neno **taa** kwa matamshi ya bila mpumuo ni kifaa kinachotoa mwangaza, na neno **$t^h$aa** kwa matamshi ya mpumuo ni samaki mwenye umbo bapa na mkia mrefu. Hivyo, isharasauti **[ t ]** na **[ $t^h$ ]** kwa lahaja ya Kiunguja Mjini (lahaja iliyosanifiwa) ni fonimu mbili tofauti kwa kuwa zina sifa tofauti zamaumbo yao, matamshi yao na maana zao. Kwa kuwa Kiswahili sanifu asili yake ni Kiunuja Mjini, ndio maana inakubalika kwa kiasi kikubwa kuwa isharasauti mbili zinazokubali matamshi ya mpumuo na bila mpumuo na kutafautisha maana, huwa ni fonimu mbili tofauti katika Kiswahili sanifu. Kwa mujibu wa Martinent (1973) kama alivyoelezewa na Mgullu (2001:64), dhana ya mpishano huru ni maneno mawili yanayoweza kuwa na tofauti ya fonimu moja tu katika kila neno lakini fonimu hizo zenye tofauti ya kifonetiki haziwezi kuwa ni alofoni za fonimu moja. Pia fonimu hizo zilizotofauti kifonetiki hazipo katika ule uhusiano wa kimtoano, yaani zote zinaweza kutumika katika mazingira ya aina moja bila ya kusababisha tofauti. Kila fonimu moja inaweza kutumiwa badala ya nyingine katika

maneno maalumu bila kubadili maana katika maneno hayo. Mifano ifuatayo inathibitisha mfumo wa mpishano huru:

Baibui - Buibui: Isharasauti [ a ] na [ u ] ni fonimu za Kiswahili.

B**e**nua - B**i**nua: Isharasauti **[ e ]** na **[ i ]** ni fonimu za Kiswahili.

-**i**ngine - **e**ngine: Isharasauti **[ i ]** na **[ e ]** ni fonimu za Kiswahili.

**Kh**eri - **H**eri: isharasauti **[ kh ]** na **[ h ]** ni fonimu za Kiswahili.

Mith**a**li - Mith**i**li: Isharasauti **[ a ]** na **[ I ]** ni fonimu za Kiswahili.

**Sh**ikio - **S**ikio: Isharasauti **[ sh ]** na **[ s ]** ni fonimu za Kiswahili.

Tofauti - T**a**fauti: Isharasauti **[ o ]** na **[ a ]** ni fonimu za Kiswahili.

O**ny**esha-O**n**esha: Isharasauti **[ ny ]** na **[ n ]** ni fonimu za Kiswahili.

Kwa mujibu wa Jones (1957) kama alivyoelezewa na Mgullu (2001:61) anafafanua kwamba, fonimu mbili au zaidi za lugha fulani, zinaweza kufanana sana katika sifa zake bainifu kifonetiki lakini zikatofautiana hata kwa sifa bainifu moja tu basi fonimu hizo huwa ni tofauti katika lugha hiyo. Kwa mfano tukizichunguza sifa bainifu za kimatamshi za fonimu irabu / **ɪ** / na / **ʊ** / za Kiswahili sanifu tutabaini matokeo yafuatayo:

Fonimu irabu / **ɪ** / na / **ʊ** / zinafanana katika sifa mbili tu ambapo zote ni irabu fupi na zote ni irabu za juu. Irabu hizi kwa upande wa pili zinatofautiana katika sifa tatu ambazo ni:

| / **ɪ** / | | / **ʊ** / |
|---|---|---|
| Umbo la msimamo wima | - | Umbo la upinde |

Pahali ni irabu ya juu mbele - Pahali ni irabu ya juu nyuma

Mkao wa Mdomo ni mtandazo - Mkao wa Mdomo ni mviringo

Hivyo basi, fonimu irabu **/ ɪ /** na **/ ʊ /** hatuwezi kusema kuwa ni fonimu moja kwa sababu irabu hizi zina sifa pambanuzi na zinatofautiana sana kiumbo na kisifa za kifonetiki. Kwa hiyo, hizi ni fonimu mbili tofauti katika lugha ya Kiswahili sanifu.

Katika mitazamo hiyo tofauti ya dhana ya fonimu, utafiti huu unabaini kuwa suala la kutofautiana kwa wataalamu limejitokeza hata katika dhana ya fonimu kwa wataalamu tofauti na kila mtaalamu mmoja anakubalika kwa kanuni ya kisayansi aliyoitoa pamoja na mifano inayokidhi matumizi ya fonimu hizo katika Kiswahili sanifu. Lakini ikumbukwe kwamba, kutofautiana kwa wataalamu hao sio kwa kiasi kikubwa bali ni kwa kiasi kidogo tu ambapo hakusababishi athari hadi kufikia kujiuliza mswali yasiyo na jawabu.

## 2.3 Asili ya Fonimu za Lugha

Kwa mujibu wa Massamba, (2012: 24-25, istilahi ya fonimu iliasisiwa na Boudouin de Courtenay ambaye aliungwa mkono na Robins, (1967:204). Boudouin de Courtenay alitumia neno la Kirusi *fonema* ingawa kwa mujibu wa Firth, (1957:1) anahoji kuwa, Boudouin de Courtenay aliiazima istilahi hiyo kutoka kwa mwanafunzi wake Kruszewiski aliyoitunga mnamo mwaka 1879 huko Kazan (Kruszewiski, 1879).

Aidha, Boudouin de Courtenay alibuni neno *anthropofoniki* kuwa ni taaluma ya fonetiki na *Saikofonetiki* kuwa ni taaluma ya fonolojia kwa kuziangalia isharasauti zinazotamkwa na msemaji wa lugha (Anderson, 1985:65). Zaidi ya hayo, Boudouin de Courtenay aliamini kuwa, fonimu za lugha fulani zilikuwa na dhima pambanuzi lakini hazikuwa zinawakilisha maana yoyote zikiwa peke yao bila ya kutumika katika lugha mahsusi.

Asili hii ya fonimu inakubalika kwani isharasauti za lugha nyingi huhusiana na taaluma ya fonetiki na isharasauti za lugha mahsusi huhusiana na taaluma ya fonolojia (Massamba, 2004:12). Pia fonimu ndio msingi wa lugha zinapoteuliwa kinasibu katika lugha mahsusi. Fonimu hizi zinapounganishwa kwa kufuata sheria, au kanuni au utaratibu wa lugha ya mwanadamu huzuka katika viwango viwili vya kushirikiana na kukamilishana. Fonimu hizo katika lugha zikisimama peke yake bila ya kuunganishwa hazitowi maana yoyote. Hali hii ni sawa na milio ya wanaadamu, wanyama, ndege au honi ya gari. Fonimu za lugha kama / a, b, g, ε, t, θ, ʧ, ɣ, ʄ, ɱ, ɖ, ɪ, n, m, ʊ /, huwa na utaratibu maalumu wa utamkwaji wake kwa kutumia alasauti au alamatamshi mbalimbali katika chemba cha kinywa cha mwanadamu. Alasauti za mwanaadamu zinazotumika kutamkia fonimu ni kama zinavyobainika hapa chini.




**Chanzo: Nchimbi, *(*1992)**

**Mchoro Nam. 2.1: Alasauti za Kutamkia Fonimu za Lugha**

Mchoro wa hapo juu unabainisha alasauti za mwanaadamu zenye dhima ya kutamkia fonimu za lugha zikijumuisha fonimu konsonanti na fonimu irabu.

### 2.4 Fonimu Kuwa Kijenzi cha Msingi katika Lugha

Kwa mujibu wa Mario na Frank (1954:294) wanaamini kuwa lugha ni isharasauti zenye maana ambazo hutolewa na mwanaadamu tu kwa pale walipohoji:

> Lugha ni mfumo wa mawasiliano kwa njia ya sauti, yaani kwa kutumia alasauti na kusikika miongoni mwa binaadamu wa kundi fulani au jumuia kwa kutumia sauti ambazo maana zake hueleweka kwa unasibu tu.

Mario na Frank kwa lugha ya kilughawiya, wanazungumzia sauti kwa maana ya fonimu kuwa ni msingi wa lugha ya mwanaadamu katika mawasiliano ya kutumia maneno **(**Trubetzkoy, 1939) & Chomsky, 1957). Kwa mkabala huo, Mario na Frank inabainika kuwa, sifa kuu ya lugha ni kutumia fonimu ambazo hutengenezwa na ala za sauti. Pamoja na maendeleo ambayo mwanadamu ameyafikia kwa sasa katika uandishi na uwasilishaji wa taarifa kwa kutumia lugha, kama ilivyokwishasemwa hapo awali, fonimu ndio msingi wa lugha na maandishi ni uwakilishi tu cha matamshi ya kusemwa kwa kutumia idadi mahsusi ya fonimu za lugha inayohusika. Kwa mawazo haya ya Mario na Frank, utafiti huu unakubaliana na wataalamu hao kuwa, chanzo cha lugha ni isharasauti kwa maana ya fonimu.

Kwa mujibu wa Massamba (2004:12) fonimu ni: kipande kidogo kabisa katika mfumo wa isharasauti za lugha ambacho kina sifa pambanuzi za kuweza kuvitofautisha vipande vingine vya aina yake. Katika fasili hii ya fonimu, Massamba ametumia maneno *sifa pambanuzi* kwa maana ya sifa inayoweza kuvitofautisha vipande vingine vya maneno. Hii ina maana ya kuwa utamkaji wa kila fonimu moja na kiashiria chake katika lugha

hujitofautisha na fonimu nyingine kimaana, kiumbo na kiviashiria vyao. Mfano wa fonimu **/ t /** na **/ d /** katika Kiswahili sanifu kila moja kati ya fonimu hizi ina kiashiria chake na utamkaji wake na ndipo inapopatikana tofauti ya fonimu hizo kimaana katika maneno **t**aka (kuhitaji kitu) na **d**aka (kupokea kilichorushwa au au kikonyo cha nazi) au maneno **t**aka (kuhitaji kitu) na **t**$^{\mathbf{h}}$aka (uchafu).

Dhana hii ya fonimu inakubalika kwani isharasauti za lugha nyingi huhusiana na taaluma ya fonetiki na isharasauti za lugha mahsusi huhusiana na taaluma ya fonolojia (Massamba, 2004:12). Pia fonimu ndio msingi wa lugha zinapoteuliwa kinasibu katika lugha mahsusi. Fonimu hizi zinapounganishwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za lugha fulani ya mwanadamu huzuka katika viwango viwili ambavyo vinashirikiana na kukamilishana.

Kiwango cha kwanza ni cha utamkaji wa fonimu zenyewe kama: / b, g, ɛ, t, θ, ʧ, ɣ ɠ, ɱ, ɖ, ɪ, n, m, ʊ / kwa kutumia ala za matamshi mbalimbali katika chemba cha kinywa cha mwanadamu. Fonimu hizo katika lugha zikisimama peke yake bila ya kuunganishwa na fonimu nyingine hazitoi maana yoyote. Hali hii ni sawa na milio ya vitu vyenye uhai kama wanaadamu, wanyama, ndege, au vitu visivyo na uhai kama honi ya gari, kengele ya baskeli, mvumo wa pangaboi, mburuzo wa meza na kadhalika. Kiwango cha pili ni cha maana yaani, pale fonimu hizo zinapounganishwa kwa utaratibu na kanuni za lugha inayohusika. Hii ina maana msemaji wa lugha hutamka fonimu kwa mara moja pamoja na maana ikiwa imechukuana ndani kwa ndani. Simile katika blog "*Utangulizi wa Lugha na Isimu*" ameliona hili aliposema kwamba, msemaji au mzungumzaji wa lugha fulani hutamka maneno yaliyounganishwa fonimu zenye maana katika lugha inayohusika. Kutokana na utaratibu huu, ni wazi kuwa fonimu maalumu za lugha mahsusi kama Kiswahili, zikiunganishwa hujenga maneno yenye matamshi fasaha na maana sahihi

inayokubalika kwa wazawa na wajuzi wa lugha hiyo. Mfano, neno *lugha* katika Kiswahili neno hili lina matamshi ya / l ʊ ɤ a / lenye maana ya mawasiliano ya jamii fulani kwa kutumia maneno ya kusemwa au kuandikwa. Neno hilihili kwa Kiingereza ni *language* lenye matamshi ya / l æ ŋg w ɪ ʤ / lenye maana ya lugha. Neno hilihili kwa Kiarabu ni **[ لغة ]** lenye matamshi ya / l ʊ ɤ a t ʊn / lenye maana ya lugha.

Daniel Jones (1881-1967)[9] ametofautiana na Massamba alipodai kuwa fonimu kwa mtazamo wa kifonetiki ni umbo halisi la kitajwa na kinachosikiwa na msikilizaji wa isharasauti za lugha fulani. Naye, Chomsky, (1957) amefafanua juu ya maana ya fonimu aliposema:

> Katika lugha ya mwanaadamu, fonimu (kutoka Kigiriki: [φώνημα] [phōnēma], sauti iliyotamkwa ni kijenzi kidogo kabisa cha kimuundo kinachobadilisha maana. Fonimu si vipande halisi lakini kinadharia vinafahamika kidhahania au kimgawanyo. Mfano wa fonimu kutoka lugha ya Kiingereza ni sauti **/** t **/** katika maneno **t**ip (ncha au bahashishi), s**t**and (steni au simama), wa**t**er (maji), na cat (p’aka). (TAKIKI).

Maana hii ya fonimu ya Chomsky ina uhusiano wa moja kwa moja na ile maana ya Trubetzkoy iliyotafsiriwa na Baltaxe na Boudouin de Courtenay (1969) kwamba fonimu ni kijenzi cha hisia pambanuzi na si kijenzi halisia. Maana hii inakubalika na itakuwa ndio kanuni ya kufuatwa katika utafiti huu.

---

[9] Katika https://en.wikipedia.org/wiki/Daniel_Jones_(phonetician)

Kwa mujibu wa ‘Old World Book Encyclopedia’ (2020)[10] matamshi ndio msingi wa lugha na kuthibitika kuwa maandishi ni kiwakilishi cha matamshi. Hali hii inaonesha kuwa, lugha ilanza na matamshi na maandishi yakafuatia baadaye. Hadi sasa hakuna uhakika wa maandishi ya lugha yalianza lini na wapi duniani. Wataalamu wengi waliona ya kwamba, Sumeria katika Mesopotamia ilikuwa na maandishi ya kwanza duniani. Wengine wameona ya kwamba sanaa ya uandishi ilianzishwa na watu mbalimbali kwa nyakati tofauti katika pande tofauti za dunia. Kihistoria tuna ushahidi wa maandishi ya mapema hasa, yaliyotoka nchi za Mesopotamia, Misri, Bara Hindi na China[11] Si rahisi kuwa na uhakika wa maandishi ya kwanza yalianza wapi kwa sababu maandishi yenyewe yalidumu kwa muda tu kutegemeana na maumbile ya vifaa vilivyotumiwa. Maandishi ya mwanzo yaliandikwa juu ya miamba, kuta za mapango, majabali, matofali ya udongo, vitambaa, mbao au mabati ya metali na karatasi zilizokosa kuhifadhiwa. Mtandao wa Kikabari[12] [12]umehoji kwamba maandishi yalianza mnamo miaka ya 3000 K.K. katika nchi ya Mesopotamia ya kale. Kwa sasa nchi hiyo ni Iraq. Wasumeria wa Mesopotamia walikuwa wakitumia maandishi ya kale yaliyojuilikana kwa jina la Maandishi ya Kikabari. Maandishi haya chanzo chake yalikuwa ni maadishi ya picha zilizotumiwa kuandika habari fulani. Hapakuwa na karatasi kwa wakati huo. Watu iliwabidi waandike kwenye mbao, kuta, magome ya miti na vitu vyengine.

[10] Katika https://en.wikipedia.org/wiki/Daniel_Jones_(phonetician)

[11] Katika http//sw.waikipedia.org/wiki/china

[12] Katika https://sw.wikipedia.org/wiki/Mwandiko_wa_kikabari#

Mfano wa maandishi ya Kikabari yaliyoandikwa ukutani kwa kutumia picha ni kama yafuatayo:




**Chanzo: Mtandao wa Kikabari, 2020**

**Mchoro Nam 2.2: Maandishi ya Kikabari**

Tafiti zinathibitisha kuwa mfumo wa maandishi ya lugha umekuja baadaye sana katika maendeleo ya binadamu na kwamba, hutumika tu kuwasilisha yale yanayosemwa kwa kutumia kinywa cha msemaji. Vilevile inathibitika kwamba, binadamu anapozaliwa tu, huanza kusema lugha ya pahali anapokuwapo yaani, pahali anapoishi kabla ya kufahamu kuandika. Utaratibu huu ndio unaotuthibitishia kuwa msingi wa lugha ni fonimu. Habwe na Karanja (2004:15) wanaunga mkono kuwa lugha huanza na matamshi yaani fonimu pale walipotoa sababu sita zinazotuwezesha kukubaliana kuwa msingi wa lugha ni isharasauti za kutamkwa yaani, fonimu. Sababu hizo ni:

xii) Mtoto hujifunza kuzungumza kabla hajajifunza kusoma na kuandika.

xiii) Mtoto hujifunza lugha moja kwa moja bila kufikiri kadiri anavyokuwa.

xiv) Maandishi yalikuja baada ya kusema au kuzungumza.

xv) Maandishi huwasilisha yale yanayosemwa au yanayozungumzwa.

xvi) Watu kwa kawaida hutumia muda mwingi kusema au kuzungumza kuliko kuandika.

xvii) Kuna mambo mengi ya muhimu katika sauti za lugha ambayo hayawezi kuwasilishwa vyema kwa kutumia maandishi kwa baadhi ya lugha.

Mambo hayo ni zile sifa za kiarudhi kama, kiimbo, toni, mkazo na kidatu. Mambo haya ni muhimu katika mawasiliano lakini hayawezi kuwasilishwa kisawasawa kwa kutumia maandishi hususan katika lugha ya Kiswahili. Utaratibu huu uliogunduliwa na Habwe na Karanja kwamba, lugha ni ya kusemwa na maandishi ni kiwakilishi tu unakubalika na una uhusiano wa moja kwa moja na utafiti huu, kwamba kila lugha ikiwemo lugha ya

Kiswahili sanifu, lazima iwe na idadi mahsusi ya fonimu zake zenye kujenga maneno ya lugha hiyo kimatamshi na hatimaye kimaandishi.

## 2.5 Dhana ya Fonolojia ya Lugha

Kwa kuwa utafiti huu unahusu taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu, ni vyema pia tukapitia na kudokeza kuhusu dhana ya fonolojia katika lugha. Kwa mujibu wa Lekule katika Chomboz (2013)[13] neno fonolojia, linatokana na maneno mawili ya Kigiriki *phone* kwa maana ya isharasauti za kusemwa na *logos* kwa maana ya taaluma. Lekule anaendelea kueleza kuwa masimulizi pia yanadai kuwa taaluma hii ya fonolojia ilianza zamani sana katika karne ya tano katika mwaka 460 kabla ya Masihia huko India ya kale. Inaaminika kwamba, mwanalughawiya aliyeitwa Panin, na ambaye aliaminika kuwa ni baba wa taaluma ya lughawiya, aliandika kuhusu fonolojia ya Kisansikriti katika matini aliyoita *Shiva Sutras*. Katika maandishi haya ndipo Panin alipobainisha kuwepo kwa dhana za fonimu katika taaluma ya fonolojia za lugha mahsusi mbalimbali.

Kwa mujibu wa maelezo hayo ya Lekule, fonolojia ni tawi la lughawiya fafanuzi linalofafanua uchunguzi, uchanganuzi na uchanganuzi wa fonimu za lugha mahsusi. Uchunguzi, uchanganuzi na uchanganuzi huo ni wa isharasauti katika nyanja za kimatamshi, kimasikizi na uwakilishi wake kimaandishi ya kiotografia na kifonetiki (Khamis, 2011:15). Naye Massamba (1996:3) amehoji kuwa neno fonolojia ni tawi la lughawiya linaloshughulikia taaluma ya mfumo wa isharasauti za lugha asilia. Dhana hii

[13] Katika http://chomboz.blogspot.com/2013/11/#

kwa Massamba inabainisha kuwa, kila lugha asilia ina mfumo wa fonimu zake za kipekee ambazo huwa na kazi ya kujenga maneno yenye maana katika lugha hiyo. Kwa dhana hii ya fonolojia, inabainika kuwa kila lugha asilia ikiwemo lugha ya Kiswahili ina idadi mahsusi ya fonimu zake zikiwemo (fonimu konsonsanati na fonimu irabu) ambazo hutofautiana na lugha nyingine. Aidha, inabainika kuwa kuna isharasauti zinazotumika katika lugha anuwaai. Kwa mfano isharasauti [ s ] inatumika katika Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno, Kihispania na nyinginezo. Kwa upande wa pili kuna isharasauti zilizomo katika lugha moja lakini hazimo katika lugha nyingine. Mfano lugha ya Kiarabu ina isharasauti [ ع ] ambayo katika Kiswahili na Kiingereza haiko. Lugha ya Kiingereza ina isharasauti [ ʤ ] ambayo katika Kiarabu na Kiswahili haiko. Aidha, lugha ya Kiswahili ina isharasauti [ mb ] ambayo katika Kiarabu na Kiingereza haiko. Katika utaratibu kama huo ndipo panapotokea lugha kufanana na kutofautiana katika idadi ya fonimu zao na viashiria vyao.

## 2.6 Usanifishaji wa Kiswahili na Athari zake

Usanifishaji wa Kiswahili, kwa mujibu wa maelezo ya Mbaabu (2007:vi) na Whiteley (1969) kama walivyonukuliwa na Maganga (1991:4) mnamo tarehe 1 Januari 1930, iliundwa Kamati ya Usanifishaji wa Kiswahili ya Afrika Mashariki, Kamati hiyo ilijuilikana kwa jina la: *Inter Territorial Language (Swahili) Committee* yaani, Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ambayo wajumbe wake walikuwa wazungu watupu bila ya kuwemo mswahili hata mmoja. Kamati hiyo iliunda Sera iliyoelekeza kwamba, miswada yote ya Kiswahili sanifu lazima ichunguzwe kwanza na Kamati hiyo kabla ya kuchapishwa. Lengo la sera hiyo lilikuwa ni kuhakikisha kuwa wataalamu wote wa kazi za Kiswahili sanifu wanafuata taratibu na miongozo iliyowekwa na kukubalika kulingana

na matamshi sahihi ya fonimu zinazojenga maneno ya Kiswahili sanifu. Sera hii ilitaka maandishi ya vitabu, magazeti, matangazo ya redio na vipeperushi yaandikwe au yazungumzwe kwa Kiswahili sanifu kama yanavyotamkwa kwa kuzingatia maneno yanayoundwa kwa idadi mahsusi ya fonimu za Kiswahili sanifu.

Sera hiyo ilikuwa ni sahihi lakini katika muendelezo wa usanifishaji wa Kiswahili ilibainika kuwa wasanifishaji kwa kudharau au kwa kusahau kazi yao ya usimamizi, waliziepuka baadhi ya kanuni hizi. Kutokana na baadhi ya wataalamu kudharau au kwa kusahau walisababisha suala la kutofautiana katika baadhi ya vipengele vya taaluma ya Kiswahili sanifu tangu zama hizo hadi hivi sasa. Zaidi ya hayo, baada ya uhuru wa nchi za Afrika Mashariki katika miaka ya 1960, lahaja ya Kiunguja Mjini ndiyo iliyochaguliwa na kusanifiwa na hatimaye kuwa Kiswahili sanifu na kikatangazwa kuwa ni Lugha ya Taifa kwa Tanzania. Hatua hii ilionekana kuwa ni chachu kwa wataalamu kwani, uzoefu unaonesha kuwa, Kiswahili sanifu chenye asili ya lahaja ya Kiunguja Mjini kilipata athari ya kuingiliwa na wataalamu wengi wa ndani na nje ya Tanzania katika taaluma za fasihi, mashairi, sarufi pamoja na lughawiya. Lakini kwa bahati mbaya katika kipindi hicho cha baada ya uhuru wa nchi za Afrika Mashariki, hali iligeuka sana kwani kulitokea athari wa baadhi ya wataalamu wa Kiswahili walioandika vitabu vyao na kuvichapisha bila ya usimamizi wa Kamati au chombo chochote cha usanifishaji wa Kiswahili (Khamisi, 2005:).

Naye Gromova (2008: 115-120*)* anahoji kuhusu usanifu wa lugha aliposema:

> Usanifishaji wa lugha ni jambo la lazima kwani lugha katika maisha yake hubadilika badilika na kupitia hatua mbali mbali. Mabadiliko ya kimsamiati na ya kisarufi pia ni mambo ya kuwekwa maanani hasa kwa walimu na wanafunzi. Wataalamu wa lugha hujaribu kukisanifisha

> Kiswahili na kukisahihisha, kwa sababu ukuaji wa lugha kwa kiasi kikubwa namna hiyo unahitaji mwongozo wa vitabu vya rejea vya kuaminika na vinavyokidhi mahitaji ya wakati uliopo, kuanzia kamusi, vitabu vya sarufi, na vitabu vingine vya matumizi bora. La sivyo, mwalimu wa Kiswahili shuleni atapotea njia na kupotosha wanafunzi wake, ambao ndilo taifa la kesho, na mwandishi wa Kiswahili anakuwa mbabaishaji anayedhuru nchi nzima kwa maandishi yake, badala ya kuboresha lugha na kuendeleza lugha yake. (TAKIKI).

Gromova hapa anatoa ushahidi kuwa vitabu vya sarufi vya Kiswahili sanifu vinatofautiana kutokana na lugha ya Kiswahili kusanifishwa kimakosa na muelekeo wa vitabu hivyo ni kupotosha maandishi yao badala ya kuyaimarisha.

Hapa napo kwa kisi, panachangia kutofautiana kwa taaluma za Kiswahili sanifu kwa kuingiliwa na wataalamu wageni na wenyeji wa Kiswahili ambao kila mmoja aliandika bila ya kufuata sera ya Kiswahili sanifu. Uandishi huo, inawezekana kuwa pia ni chanzo cha waandishi wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu kutofautiana. Inawezekana waandishi wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu waliandika bila ya kufanya utafiti wa kina kuhusu uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Inawezekana pia uandishi huo, ulifanywa bila ya kuzingatia kanuni ya kisayansi ya kubainisha idadi ya fonimu za Kiswahili sanifu. Aidha, inadhaniwa kuwa usanifishaji wa Kiswahili uliletwa pengine kuharibu ule usahihi na ufasaha wa Kiswahili cha Waswahili wenyewe kulingana na utamaduni wao katika eneo lao la upwa wa Afrika Mashariki. Dhana hii imeungwa mkono na Khalid, (1977:163) pale alipohoji:

> Lakini kipindi cha ukoloni kinafikia kikomo hata katika uwanja wa utamaduni na muda wa mwanzo mpya umeshawadia. Tuliona kwamba

> wakoloni hawakukisanifu Kiswahili lakini walionesha mahitaji ya kukisanifu kama kisingizio katika mtindo wa kukitenga. Lugha ya Kiswahili bado ipo katika mfumo wa lahaja anuwai. Usanifishaji wake ambao ulikuwepo zamani lakini baadae ukachafuliwa na wakoloni, sasa unahitaji kufanywa upya.

Kwa maoni hayo ya Khalid, usanifishaji wa Kiswahili uliofanywa na wageni wa Kiswahili pengine umekiharibu Kiswahili badala ya kukitengeneza kwa ajili ya matumizi muwafaka. Utafiti huu kwa kiasi kikubwa ulihitaji kuthibitisha ukweli wa hoja hiyo. Lengo likiwa je kuna ukweli kama Kiswahili sanifu kina kasoro ya kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake kama zilivyobainishwa na wataalamu zaidi ya 35 katika kifungu cha (2.7) huko mbele Maneno ya Kiswahili yanayojengwa kwa fonimu zake mahsusi, yana maumbo, miundo, mitindo, matumizi na matamshi ya kipekee kwa wajuzi na Waswahili wazawa wenyewe. Upekee wa Kiswahili unaungwa mkono na Mayoka (2007:3) pale aliposema:

> Kiswahili kama zilivyo lugha nyingine kina mpango wa matumizi maalumu wa maneno ambao ukikosewa Mswahili hushtuka na kuona kuwa hayo si matumizi sahihi ya mpangilio wa Kiswahili sahihi . . . na hayo hutokea kwa sababu ya athari za lugha nyingine ama kutokipenda Kiswahili au kwa namna nyingine yoyote ile. Kwa mfano, tunaposema bei ya kitu twatanguliza pesa au senti, twasema ‘’shilingi moja’’ hatusemi ’moja shilingi” ‘kama ilivyo katika lugha nyingine ambazo ndio usahihi wake.

Mayoka hapa anatuthibitishia kuwa Kiswahili kina matumizi yake sahihi kwa Waswahili wenyewe kulingana na matamshi saihhi ya fonimu zake kama zilivyo lugha nyingine kwa wenyewe lugha hizo. Wasanifu walipoyabadilisha matamshi ya maneno mengine inabainika kuwa sababu kubwa ni kuwa maneno hayo hayakupata kusanifiwa na

Waswahili wenyewe ambao, wangeweza kuyatamka kwa usahihi na kwa ufasaha na pia wangeweza kuyawakilsha kwa maandishi sahihi.

Kwa upande wa pili, uzoefu unaonesha kuwa, ikiwa maneno yatatamkwa kimakosa, basi matamshi hayo yatasababisha kutokea makosa ya maana. Kauli hii inaungwa mkono na Maro (2013:2) katika *''Jungu Letu''*, alipotanabahisha:

> Matamshi ni namna ya kutamka; utamkaji wa maneno katika lugha. Kwa hiyo, maneno yasipotamkwa vizuri au kuandikwa tofauti ni rahisi kupotosha maana. Katika miaka ya karibuni kumekuwa na matumizi mabaya ya maneno yafanywayo na wazungumzaji, wataalamu na watangazaji wa radio na runinga. Tatizo lingine ni wataalamu kuandika vichwa vya habari vinavyotofautiana na habari husika.

Hoja ya Maro ni sahihi lakini kwa mujibu wa utafiti huu, uchunguzi unagundua kuwa hata yeye Maro mwenyewe amefanya makosa katika baadhi ya maneno katika hoja yake hiyo. Maneno *runinga*, *lingine*, na *husika*. Kwa Waswahili wazalia wenyewe maneno hayo hayatamkwi wala hayaandikwi hivyo bali hutamkwa na kuandikwa hivi: televisheni au tivii badala ya *runinga*, jengine badala ya *lengine* na inayohusika badala ya *husika.*

Maneno haya yamekosa matamshi sahihi kwa kutolingana na yanavyotamkwa na Waswahili wazawa wenyewe. Hali hiyo imetokana na kubadilishwa lafudhi, na miundo ya lugha yenyewe.  Kwa hivyo, husababisha kuharibu ladha ya matamshi na hata maana. Hivyo basi, matamshi hayo hupelekea kuwa na lugha mbovu isiyokuwa fasaha (Mohammed, 1976:109). Uzoefu unaonesha kuwa mara nyingi makosa ya utamkaji wa fonimu katika maneno ya Kiswahili sanifu, hufanywa na Watanzania wasiowazalia wa Kiswahili, vijana na pia watu wasio wajuzi wa taaluma ya matamshi. Hawa ndio wanaopotosha matamshi hayo na kutamka visivyosahihi kama yalivyobainishwa hapo juu.

Hatima yake, matamshi hayo yasiyosahihi na fasaha huwaambukiza na kuwaathiri vijana, watoto na hata watu wazima wazawa wa Kiswahili. Wanaoambukizwa nao hutamka visivyosahihi na visivyofasaha kwa nia ya ama kuwaiga na kuwahusudu wanaotamka maneno hayo kimakosa au kwa kuona kuwa hayo matamshi yasiyosahihi ndio sahihi na fasaha kwa kutokuwa na taaluma ya kuwa lugha ni matamshi sahihi na fasaha.

## 2.7 Matatizo ya Kutofautiana katika Fonolojia ya Kiswahili Sanifu

Matatizo ya kutofautiana katika fonolojia ya Kiswahili Sanifu kwa jumla yamezungumziwa na wataalamu mbalimbali. Gromova, (2008:118) kwa kuchangia juu ya suala la kutofautiana katika fonolojia ya Kiswahili sanifu, anakumbusha juu ya makosa ya Kiswahili sanifu yanayofanywa na wataalamu, walimu, wanafunzi na wazungumzaji wa kawaida kwa kusema:

> Ikumbukwe miaka ya themanini ya karne iliyopita ambapo wataalamu wa lugha walieleza magazetini na redioni makosa yanayofanywa mara kwa mara katika matumizi ya Kiswahili. Inawezekana kusema kwamba, kiwango kipya cha usanifishaji wa sarufi na msamiati wa Kiswahili kimefikiriwa baada ya TUKI ilipotoa toleo la SAMAKISA (2001) na toleo la pili la Kamusi ya Kiswahili sanifu KKS (2004) . . . sote tunajua kuwa lugha si kitu kilichoganda, lugha inaendelea na kukua bila ya kusita. Kile kilichoelezwa kama kosa, kinaweza kuwa sahihi baada ya muda kupita. Kwa mfano: matumizi ya neno mkupuo kuwa na maana ya hatua, yalielezwa kama tafsiri isiyosahihi ya neno la Kiingereza phase (Idarus, 1983:178). Lakini katika Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili (TUKI 1996) neno phase lilitafsiriwa kama awamu au mkupuo (TAKIKI).

Gromova anatanabahisha kuwa lugha ni kitu cha mabadiliko kutegemea mabadiliko ya jamii lakini usahihi wa lugha sanifu kimatumizi ni jambo la msingi na linahitaji usimamizi na makubaliano ya pamoja. Hivyo, ujumbe huo wa Gromova unahitaji pia kuzingatiwa

katika suala la usanifu wa lugha kama Kiswahili katika idadi ya fonimu na viashiria vyake pamoja na matamshi sahihi ya maneno yake yote.

Ingawa katika baadhi ya lugha, matamshi huandikwa lakini suala la kuzingatiwa hapa ni matamshi ambayo ndio msingi wa lugha yoyote ile ikiwemo lugha ya Kiswahili. Maandishi katika lugha, kwa kawaida huchukuliwa kuwa ni kiwakilishi tu cha matamshi kwa zile lugha chache zenye maandishi. Asili ya lugha nyingi ni za kusemwa yaani matamshi (Mmallavi, 1977:84 na Nchimbi, 1996:3). Kwa mantiki ya kuwa matamshi ndio asili ya lugha, ni wazi kuwa, kimsingi matamshi nayo asili yake ni fonimu za lugha yoyote ile iwayo. Kwa sababu mfuatano wa fonimu ndio unaojenga maneno ya lugha ambayo huhitaji kutamkwa kwa usahihi na kwa ufasaha ili yatoe maana inayokusudiwa. Kwa hoja hii, idadi ya fonimu katika lugha ya Kiswahili sanifu ndizo zinazojenga maneno yenye kuhitaji kutamkwa kwa usahihi na kwa ufasaha kwa nia ya kupata maana sahihi ya maneno yake kimatumizi (King'eu & Musau, 2002, Ligami, 2002 na Joseph, 2004). Hali hii ya kuwepo kwa matatizo na masahihisho ya Kiswahili pia inathibitishwa na kutolewa muongozo na Simala, (2004:39) aliposema:

> Wazalendo wa lugha ya Kiswahili wanadai kuwa matatizo yanayoikumba lugha hii ni lazima kutazamwa na kueleweka kuwa ni masuala ya kijamii . . . Hivyo basi, pana haja ya dharura kuhakikisha kwamba Kiswahili kinapewa hadhi yake katika jukwaa la lugha za Kiafrika na zile za ulimwengu.

Simala anasisitiza kuwa, Kiswahili ni chombo cha jamii basi hakikosi matatizo. Lakini kila yanapogundulikana matatizo basi yasiachiwe ila yahakikishwe kuwa, yanachunguzwa na yanafanyiwa usahihi wake, ili Kiswahili kiendelee kuwa na hadhi ya kitaifa na kimataifa.

## 2.8 Kutofautiana kwa Wataalamu katika Fonimu Ambatano na Mpumuo

Sehemu hii inawasilisha na kujadili suala la kutofautiana kwa wataalamu zaidi ya 35 katika kubainisha isharasauti ambatano ng'ong'o na isharasauti mpumuo kama ni fonimu au si fonimu katika Kiswahili sanifu.

### 2.8.1 Kutofautiana kwa Fonimu Ambatano Ng'ong'o [ mb, nd, ng, nj ]

Wataalamu wametofautiana katika uwasilishaji wa isharasauti ambatano ng'ong'o

[ mb, nd, ng, nj ] kama ni fonimu au si fonimu katika Kiswahili sanifu.

Kwa mujibu wa Nchimbi (1991:14) kuhusu suala la isharasauti ambatano ng'ong'o

[ mb, nd, ng, nj ] kama ni fonimu au si fonimu katika lugha ya Kiswahili, amesema:

> Suala la kujua kama mang'ong'o ni fonimu, au si fonimu zipo skuli mbili. Skuli ya kwanza ambayo ninaiita Skuli ya Mang'ong'o inadai kwamba baadhi ya mifungamano ya kimaandishi ya king'ong'o-konsonanti ni fonimu moja ambayo nimeipa istilshi maalumu ya Mang'ong'o. Baadhi nyingine ya mifungamano hiyo imefanyizwa kwa zaidi ya fonimu moja ambayo baadhi ya wanaisimu huiita Mifungamano ya Mkururo.

Nchimbi amewasilisha kuwa, kuambatana kwa isharasauti mbili au zaidi zenye mfuatano wa kutanguliwa na king'ong'o **[ m ]** au **[ n ]** na kufuatiwa na konsonanti za vipasuo au vikwamizi, isharasauti hizo ni fonimu na yeye ameziita fonimu mang'ong'o. Fonimu hizohizo Nchimbi amewasilisha kuwa, baadhi ya wanalughawiya wengine wameziita mifungamano ya mkururo. Mfano wa fonimu hizo ni kama:

xviii) Fonimu / mb / kwa maneno kama mbuzi, sambaa, embe, kimbia, pamba, umba na tumba.

xix) Fonimu / nd / kwa maneno kama ndege, winda, andika, bindo, ndugu, bandika na bendera.

xx) Fonimu / ng / kwa maneno kama ngao, tengua, ingia, tongo, unga na ungua.

xxi) Fonimu / nj / kwa maneno kama njozi, vunja, njegere, injika, njia na njugu.

Isharasauti **[ mb, nd, ng, nj ]** kwa mujibu wa Nchimbi, (1992) zina kambi mbili katika kuitwa kwao ama fonimu au si fonimu. Kambi ya kwanza ya wanaoziita fonimu mang'ong'o ni akina Angongo katika TUKI (1983), Ashton 1994, Halle & Chomsky 1968), Khamis (2011), Lodhi (1976), Nchimbi (1992) na Whiteley 1956. Kambi ya pili ni ya wale wanaoziita mifungamano ya mkururo ambao ni pamoja na Aswani (1995), Batibo (1981), Maganga (1967), Polome (1967), Steere (1970) na Volger (1976).

Khamis (2011:19) kwa mkabala wake amewasilisha isharasauti hizi za [ mb, nd, ng, nj ] kuwa ni fonimu na ameziita vipasuo ng'ong'o na ameziwasilisha kwa viashiria vya kifonetiki vya [ ŋb, ŋd, ŋg, ŋj ].

Batibo (1981), Bouquiaux na Cloarec-Heiss (1975), Maganga (1979) na Polome (1967) nao wamewasilisha isharasauti [ mb, nd, ng, nj ] kuwa ni fonimu na wamezibainisha kwa viashiria vya kifonetiki vya [ $^{m}$b, $^{n}$d, $^{n}$g, $^{n}$ɟ ].

Nchimbi (1979:628, 2008: 36-38) yeye amependekeza isharasauti hizi [mb, nd, ng, nj] kuwa ni fonimu mang'ong'o na amezibainisha kwa viashiria vya kifonetiki vya [ ɗb, N̲, Ɲ, ʼN ].

Lodhi (1976:1-2) amewasilisha isharasauti [mb, nd, ng, nj] ni fonimu na ameziita fonimu ving'ong'o na amezibainisha kwa viashiria vya kifonetiki vya [ Ъ, d̄, ɠ, ʤ ].

Ashton (1944:3) pia amewasilisha isharasauti [ mb, nd, ng, nj ] kuwa ni fonimu na amezibainisha kwa viashiria vya kiotografia vya [ mb, nd, ng, nj ].

Volger (1976) katika Nchimbi (1992) amewasilisha isharasauti hizi [ mb, nd, ng, nj ]. kuwa ni fonimu na amezibainisha kwa viashiria vya kifonetiki vya [ √b, √d, √g, √ɟ ].

Aswani (1995:43-44) amewasilisha isharasauti hizi za [ mb, nd, ng, nj ] kuwa ni fonimuna amevibainisha kwa viashiria vya kifonetiki vya [ m͡b, n͡d, n͡j, n͡g ].

Angongo katika TUKI (1983:62-65) amewasilisha isharasauti hizi tatu tu za [mb, nd, ŋg ] kuwa ni fonimu bila kubainisha isharasauti [ nj ] na amezibainisha kwa viashiria vya kiotografia vya [ mb, nd, ng ].

Besha (1994), Mbaabu (1985), Habwe na Karanj (2004), Kihore na wenzake (2001), Massamba na wenzake (2004), Mfaume (1985), Mgullu (2001), Mohammed (1986) na Zawawi (1971) wao hawakuzibainisha isharasauti ambatano ng'ong'o [ mb, nd, ng, nj ] kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

Steere (1970:5) kama alivyonukuliwa na Mbaabu (2007:32) alihoji kwamba, Waswahili huko mwanzo, walikuwa wakitumia fonimu [ b ] badala ya [ mb ], [ g ] badala ya [ ng ], [ d ] badala ya [ nd ], [ y ] badala ya [ ny ], [ f ] badala ya [ mv ] na [ nz ] badala ya [ ch ] na [ sh ]. Hali hii ilikuwa mwanzo wa usanifishaji wa Kiswahili wakati Steere (1870) alipohoji kuwa, hati za Kiarabu hazifai kuandikia lugha ya Kiswahili. Badala yake zitumike hati za Kirumi kwa vile isharasauti hizo za Kiswahili haziko katika lugha ya Kiarabu lakini ziko katika lugha nyingi zinazotumia hati za Kirumi na hati hizo zinatumika kama isharasauti za kifonetiki. Matatizo haya pia yamezungumziwa na Mgullu (2001:69) aliposema:

> Lipo tatizo ambalo bado halijapatiwa ufumbuzi linalohusiana na fonimu za konsonanti za Kiswahili sanifu. Tatizo hili linahusu hasa sauti ambatano za nazali na fonimu nyingine. Wapo watu wanaodhani kuwa wakati mwingine nazali zinapofuatiwa na konsonanti fulani huungana na kuwa fonimu moja na wakati mwingine haziungani.

Mawazo ya Mgullu hapa ni sawa lakini pamoja na kuliona tatizo hili yeye bado hakuzianisha hizo isharasauti ambatano ng'ong'o za nazali na vipasuo au vikwamizi katika orodha yake ya fonimu za Kiswahili sanifu. Kwa bahati, utafiti huu uliyafikiria yote haya na ikaamua kuyachunguza ili kubaini ukweli wake.

### 2.8.2 Kutofautiana kwa Wataalamu katika Fonimu Konsonanti Ambatano [ kh, nz, zy, mp, nt, nk, mw, chw, ñ, ʤ, nw ]

Ashton (1944:3), Khamis (2011:19), Lodhi (1976:1-2), Mbaabu (1985:3-8), Mbunda (1976:132), Mgullu (2001:66-69), Mohamed (1986:2), Russell (2003: xiv-xvii) na Zawawi (1971:7) wamewasilisha isharasauti ambatano **[ kh ]** kuwa ni fonimu katika Kiswahili sanifu kwa maneno kama **kh**eri, **kh**abari, **kh**iyari, **kh**ulka, **kh**utba na **kh**atibu.Wataalamu hao wamechukua kanuni ya baadhi ya wasemaji yaani Waswahili wazawa wanapotofautisha isharasauti hizo katika maneno kama Hatibu kwa maana ya jina la mtu na Khatibu kwa maana ya mtoa hotuba msikitini. Kwa maana hizo, isharasauti hizo ni fonimu mbili tofauti na si alofoni (Nchimbi 1996:23). Wataalamu wengine wote hawakuibainisha isharasauti ambatano **[ kh ]** kuwa ni fonimu. Wataalamu hao wamechukua kanuni ya kuwa baadhi ya isharasauti huibua alofoni za fonimu moja pale wazungumzaji wake wasipotofautisha maana ya isharasauti hizo kama **[ h ]** na **[ kh ]** kwa maneno kama **h**asara na **kh**asara, **h**ati na **kh**ati, **h**abari na **kh**abari (Nchimbi 1996:23).

Ashton (1944:3), Khamis (2011:19-23), Mbunda (1976:129-132) na Ager (2014) wao wamewasilisha isharasauti ambatano **[ nz ]** kuwa ni fonimu katika maneno **nz**uri, **nz**io, che**nz**a, mwe**nz**angu na mwanafu**nz**i. Wataalamu hao wamesahau kuwa isharasauti **[ n ]** katika **[ nz ]** ni fonimu silabi funge ambayo hutamkwa peke yake haiambatani na **[ z ].** Wataalamu wengine wote hawakuibainisha isharasauti hiyo kuwa ni fonimu.

Lodhi (1976:1-2), Mbaabu (1985:3-8) na Polome (1967:38-39) wamewasilisha isharasauti ambatano **[ zy ]** kuwa ni fonimu kwa maneno kama **zy**uma (jina la mtu), **zy**imwi (jina la kiumbe kisichoonekana mithili ya shetani). Wataalamu wengine wote hawakuibainisha isharasauti hiyo kuwa ni fonimu.

Whiteley (1956:8) amewasilisha isharasautiambatano [ **mp, nt, nk** ] kuwa ni fonimu katika maneno **mp**ira, **nt**a, **nk**e. Kiuhalisia hapa isharasauti **[ m ]** na **[ n ]** hutamkwa peke yao kisilabi funge na haziambatani na isharasauti **[ p, t, k ].** Kwa sababu hii labda ndio maana wataalamu wengine wote hawakuzibainisha isharasauti hizo kuwa ni fonimu.

Polome (1967:38-39), Lodhi (1976:1-2), Mbaabu (1985:3-8) wamewasilisha

isharasauti ambatano **[ ʤ ]** kuwa ni fonimu kwa maneno **j**imbo, ma**j**imbi, ha**j**i lakini wataalamu wengine wote hawakuibainisha isharasauti hiyo kuwa ni fonimu.

Khamis (2011:19), Mbunda (1976:129) na Ager (2014), wamewasilisha isharasauti ambatano **[ mw ]** kuwa ni fonimu katika maneno **mw**ani, ali**mw**ita, kutu**mw**a lakini wataalamu wengine wote hawakubainisha isharasauti hiyo kuwa ni fonimu.

Khamis (2011:19-23) na Mbunda (1976:129-132) wamewasilisha isharasauti ambatano **[chw]** kuwa ni fonimu katika maneno **chw**ale, ma**chw**eo, m**chw**a, lakini wataalamu wengine wote hawakuwakuiwasilisha isharasauti hiyo kuwa ni fonimu.

Khamis (2011:19-23) amewasilisha isharasauti ambatano [$v_y$, $m_y$, $p_w$, $p_y$, $g_w$, $k_w$, $s_w$, $t_w$, $sh_w$, $mb_w$, $nd_w$, $ng_w$, $nj_w$, $ny_w$] kuwa ni fonimu katika maneno, **vy**akula**,** ali**vyo,** ki**my**a, **my**ayo, **pw**eza, kupwam**py**a, pi**gw**a, **gw**iji, **kw**ao, andi**kw**a, **swali**, Ki**sw**ahili, **tw**aa, **mtw**iko, ku**tw**a, **shw**uari, am**shw**a, lakini wataalamu wengine wote hawakubainisha isharasauti hizo kuwa ni fonimu. Besha (1994:26), Kihore na wenzake (2001:22-25), Massamba na wenzake (2004:39-4) wamewasilisha isharasauti **[ ñ ]** kuwa ni fonimu katika maneno kama a**n**a, ki**n**engo, po**n**o lakini wataalamu wengine wote hawakuiwasilisha isharasauti hiyo kuwa ni fonimu.

### 2.8.3 Kutofautiana kwa Fonimu Mpumuo [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, ʧh ]

Wataalamu wametofautiana katika kuonesha isharasauti mpumuo [$p^h$, $t^h$, $k^h$, $ʧ^h$] kama ni fonimu au si fonimu kama ifuatavyo:

BAKIZA (2010: xi), Lodhi (1976:1-2), Massamba na wenzake (2004:40-41), Mwinza (2014), Myachina (198:4-7), Polome (1967:38-39), Whiteley (1956:8), wanadai kuwa isharasauti [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ʧ^h$ ] ni fonimu katika Kiswahili sanifu na matamshi yake ni ya mpumuo. Hoja zao kwa jumla ni kuwa, isharasauti hizi zinatofautisha maana na isharasauti zisizo na mpumuo za [ p, t, k, ʧ ] zinapokutana katika maneno yaliyowekwa katika Jozi Sahili. Mfano: **[ $p^h$ ]** aka (mnyama) na **[ p ]** aka (tia rangi), **[ $t^h$ ]** aka (uchafu) na **[ t ]** aka (hitaji), **[ $k^h$ ]** ucha (za kidole) na **[ k ]** ucha (usiku wote), **[ $ʧ^h$ ]** ana (kikanda cha ndizi) na **[ ʧ ]**ana (kupasua karatasi au kitambaa). Hivyo wanahoji kuwa tofauti ya matamshi yaani toni inasababisha tofauti ya maana na kwa hiyo isharasauti [ p, t, k, ʧ ] bila mpumuo na [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ʧ^h$ ] za mpumuo ni fonimu tofauti kwa sababu zina maumbo, matamshi na maana tofauti.

Ashton (1944:3), Aswani (1995: 43-44), BAKITA (2017: xiv-xv), Besha (1994:35-36), Habwe na Karanja (2004:49-50), King'ei na Musau (2002:3&8), Massamba (1996:5), Mbaabu (1985:3-8), Mbunda (1976:129-132), Mfaume (1985:16-19), Mgullu (2001:66-69), Mohammed (1986:2), Mutahi (1990:44-45), Njogu na wenzake (2006:8-10) na Zawawi (1971:5-7) kwao wao, isharasauti mpumuo [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ʧ^h$ ] hazina tofauti kimatamshi bali ni alofoni za fonimu moja. Hoja zao ni kuwa isharasauti hizo hazina tofauti ya matamshi na isharasauti [ p, t, k, ch ] yaani, mtu akitamka **[ p ]** au **[ $p^h$ ]** ni sawa tu kwani, hapo kuna mpishano huru wa isharasauti tu lakini hazina tofauti kimatamshi na pia hazibadilishi maana.

Whiteley (1956:8), hakubaliani na kuwa isharasauti **[ p ]** na **[ $p^h$ ]** kuwa ni alofoni za fonimu **/ p /**. Yeye anaunga mkono kuwa isharasauti mbili za lugha fulani, zinaweza kufanana katika sifa bainifu zake lakini zikatofautiana kimatamshi na kimaana, basi ikitokea hivyo isharasauti hizo huhesabika kuwa ni fonimu mbili tofauti. Mfano: isharasauti **[ p ]** katika neno ***paa*** la nyumba au ***paa*** moto hutamkwa bila ya mpumuo lakini isharasauti **[ $p^h$ ]** katika neno paa mnyama hutamkwa kwa mpumuo na Waswahili wazawa. Kwa kuwa matamshi hayo husababisha tofauti ya umbo na maana, hivyo isharasauti za **[ p ]** na **[ $p^h$ ]** ni fonimu mbili tofauti katika Kiswahili sanifu.

Kwa upande wa wasemaji yaani, Waswahili wazawa isharasauti hizo huzitamka kwa mpumuo na bila ya mpumuo kulingana na muktadha wa maana zao katika maneno ukiachilia mbali matamshi ya lahaja zao. Hivyo isharasauti [ p, t, k, ch ] hutamkwa kwa mpumuo na bila ya mpumuo na ndio sababu ya kutofautisha maana ya neno **[ p ]** aka kwa maana ya kutia rangi na **[ $p^h$ ]** aka kwa maana ya mnyama (Trubetzkoy katika Massamba, 1996:23).

Khamisi (2005:5) ametanabahisha juu ya hali ya kuziepuka baadhi ya fonimu za Kiswahili aliposema:

> Inaonekana wazi kuwa idadi ya sauti ambazo zinapatikana katika lahaja zenye asili moja na Kiswahili sanifu zinahitaji juhudi kubwa zaidi kujifunza kuzitamka ama zimeepukwa katika Kiswahili sanifu cha leo au zimerahisishwa kwa namna fulani fulani. Mathalan, toni ambayo ni tabia moja ya lugha nyingi zenye asili moja na lugha ya Kiswahili sanifu na ambayo bado inapatikana katika lahaja kadha za Kiswahili sanifu, imetolewa katika Kiswahili sanifu cha sasa.

Khamisi anatuthibitishia kuwa baadhi ya fonimu za Kiswahili sanifu zimeepukwa kuoneshwa na baadhi ya wataalamu ama kwa makusudi au kwa kutofanya utafiti wa kina. Hali ya kuziepuka baadhi ya fonimu hapa, ni kwa sababu ya kuwarahisishia watu wengine kujifunza Kiswahili sanifu lakini kila fonimu katika maneno ya lugha lazima ieleze jinsi inavyotamkwa na wenyeji wake. Khamisi anathibitisha kuwa Kiswahili sanifu hakikuzingatia mlingano wa fonimu za lahaja za Kiswahili bali zimeepukwa na matokeo yake ni kulazimishwa kuepuka toni za Kiswahili sanifu kipya ambacho yeye amekiita Kiswahili sanifu cha sasa. Hivyo utafiti huu ulichunguza hali hiyo kwa Waswahili wenyewe na kupata toni sahihi kulingana na lugha yao kama itakavyobainika huko mbele katika sura ya nne.

### 2.8.4 Kutofautiana kwa Fonimu Irabu refu [ aa, ee, ii, oo, uu ]

BAKIZA (2010: xi), Khamis (2011:19-23), Lodhi (1976:1-2), Mbunda (1976:129:132), Russell (2000: xiv-xvii), na TATAKI (2013: xvi) wameisha isharasauti irabu **[ aa, ee, ii, oo, uu ]** kuwa ni fonimu irabu refu za Kiswahili sanifu, katika maneno kama dag**aa**, mz**ee**, mt**ii**, jong**oo** na mg**uu.** Hoja yao ni kuwa isharasauti hizi zinatofautisha

maana katika maneno kama: dag**a** na dag**aa,** mremb**e** na mremb**ee,** hapik**i** na hapik**ii,** jong**o** na jong**oo,** m**u**nda na m**uu**nda lakini wataalamu wengine wote waliobaki hawakubainisha irabu hizo kuwa ni fonimu za Kiswahili.

Aswani (1995:43-44), Mohammed (1986:2), Myachina (1981:7), Polome (1967:38), Zawawi (1971:6), Mfaume (1985:19), Nchimbi (1992:13), Besha (1994:29), Mbaabu (1985:3-8), Benard (2000:38-44), Whiteley (1956:8), Njogu na wenzake (2006:8-10) na King'ei & Musau (2002:3&8) wao wamewasilisha irabu za Kiswahill sanifu kwa viashiria vya kiotografia yaani, **[ a, e, i, o, u ]** lakini Maganga (1991:270), Kihore na Wenzake (2001:22), Mgullu (2001:29), Massamba na Wenzake (2004:41), Habwe & Karanja (2004:50) na Mutahi (1990:47) wao wamewasilisha irabu za Kiswahili kwa viashiria vya kifonetiki yaani, **[ a, ɛ, ɪ, ɔ, u ]**. Mbunda (1976:132), Russell (2003: xvii), Lodhi (1976:1-2) Khamis (2011:21) na Ager (2014) wao wamewasilisha irabu za Kiswahili kwa alama mchanganyiko wa makundi hayo mawili na kuzidisha kuwa irabu 10 badala ya 5, nazo ni: **[ a, aa, e, ee, i, ii, o, oo, u, uu ]** kiotografia na **[ a, aː, ɛ, ɛː, ɪ, ɪː, ɔ, ɔː, ʊ, ʊː ]** kifonetiki. Ashton (1944:3) yeye amewasilisha kwa alama za herufi kubwa za kiotografia yaani, **[ A, E, I, O, U ]**. Lodhi (2000: ix) yeye amewasilisha irabu kwa alama za kipekee za kifonetiki zenye vialama juu ambazo ni **[ ā, ã, ė, ō, ū ]**. Kimtazamo ni vyema irabu hizi zikapata kuainishwa kwa viashiria vya namna moja na idadi sawa kwa vile lugha yenye irabu hizo ni moja yaani, Kiswahili sanifu (Khamis, (2011:19-23). Utafiti huu ulikuwa na lengo la kusawazisha tatizo hilo la kutofautiana na kuondoa hizo tofauti zilizotawala kwa waandishi hao (Lodhi, 1976:5).

Uzoefu unaonesha kuwa sababu za wataalamu hao 35 kutofautiana katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu za Kiswahili, labda kwa sababu zifuatazo:

xxii) Kila mtaalamu alikuwa na haraka ya kutaka kuibua maandishi yake kwa jamii pengine kwa kutaka kuchangia kuhusu idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

xxiii) Kutokitumia chombo kimoja cha jopo la wahariri wataalamu wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

xxiv) Sababu ya tatu ni kutowatumia Waswahili wazalia katika tafiti zao kwa hivyo kutopata idadi halisi ya fonimu kutoka kwa wazawa wa Kiswahili.

### 2.1.1 Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake katika Lugha Sanifu za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania

Tuliangalie idadi ya fonimu na viashiria vyake katika lugha sanifu maarufu za kimataifa za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na kihispania. Tunaangalia suala hili katika lugha hizo ili kutathmini kama tatizo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake ni la kawaida hata kwa lugha sanifu za kimataifa au ni kwa lugha ya Kiswahili tu? Jedwali lifuatalo linabainisha idadi ya fonimu na viashiria vya lugha hizo kama ifuatavyo:

**Jedwali Nam. 2.1: Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake katika Lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania**

| Lugha | Idadi ya Fonimu | Idadi ya Konsonanti | Idadi ya Irabu |
|---|---|---|---|
| **Wataalamu wa Kiingereza** | | | |
| British Council[14], David (2005:29), Kadeghe (2005:26-32), Katamba (1989:30-33), Michael (2013-2020)[15] O'Connor (1980:142-143), Rough (2006:22) na Yavas (2011: 65-78) | 44 | 24 | 20 |
| Finch (2003:67) na La Pho (2007)[16] | 45 | 25 | 20 |
| **Wataalamu wa Kifaransa** | | | |
| Abry na Veldeman (2007:28-33), Charliac na Motron (2006:124-125), Cappelle (2009:141), Brandão de Carvalho na wenzake (2010:104-107), Menand na Cappelle (2009:129) na Menand na Johnson (2010:172) | 33 | 20 | 13 |
| Akyüz na wenzake (2002), Hélène (2001:5), Menand (2009:141), Charliac na Motron (2004:23&113) | 36 | 20 | 16 |
| **Wataalamu wa Kiarabu** | | | |
| Abdulhamid, (2003:51), 'Ali, (2009:13-14) na Jama Masjid (1950:21-23), | 28 | 28 | - |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Abdutawaab (1997:16), Darwesh (2009:16-17), Juzuu ya Amma (125:2), Karim (2004:19), Kess (2014:25), Sibawayhi (432:30-41) na Watson (2002:2) | 30 | 30 | - |
| **Wataalamu wa Kireno** | | | |
| Azevedo (2005:37), Black (2016:57), Cardoso, Baxter na Nunes (2012:26), Comrie (1990)[17] Manuela, (1989:2), Maria, Mira na Andrea de, (2000:11) na Oliveira Jose na Luisa, (1988:12) | 31 | 23 | 8 |
| Delgado, (1988:23), Espada, (2006:115), Wikipedia, the free enclopedia[18] . | 35 | 23 | 12 |
| **Wataalamu wa Kihispania** | | | |
| Anderson (1956:57), Confied (1981:11-13), Easy Spanish Phrase Book (1994), Spanish Staff [19], Torrego (2002:384-385) na Willey (2012:93). | 23 | 18 | 5 |
| Borobio (2002:146), Duhne na wenzake, (1997:296-297), Macpherson, (1975:4-5) na Moya, (2005:122). | 24 | 19 | 5 |

**Chanzo: Data za Wataalamu 2020**

[14] Katika https://www.britishcouncil.or.tz/

[15] Katika https://www.amazon.fr/Micha%C3%ABl-

[16] Katika https://www.amateurgoument.com/2007/12/my phirst pho. htm

[17] Katika https://www.routledge.com/

[18] Katika https://en.wikipedia.org/wiki/Main_Page

[19] Katika http://www.fahs.surrey.ac.uk/languages/spanish-phonetics

Jedwali linabainisha namna wataalamu hawa walivyotafautiana kwa kiwango kidogo sana yaani, kwa fonimu mojamoja tu kwa kila lugha. Kutofautiana huku ni kwa kawaida tu kinyume na kutofautiana kwa wataalamu wa Kiswahili sanifu ambapo pameonekana kuwa lipo tatizo linalohitaji kuchunguzwa sababu na athari zake kwa jamii wa wanataaluma na wasomi wa lughawiya ya Kiswahili sanifu. Tukiangalia kuhusu viashiria vya lugha hizi inadhihirika pia kuwa wataalamu hao wamewasilisha viashiria vya aina moja bila ya kutofautiana kama inavyobainika katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Nam. 2.2: Viashiria vya Fonimu za Lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na kihispania**

| Wataalamu wa Kiingereza | Viashiri vya Fonimu Konsonanti | Viashiri vya Fonimu Irabu |
|---|---|---|
| | / p, f , t, θ, ʧ, s, ʃ, k, b, v, d, ð, ʤ, z, ʒ, g, j, w, h, m, n, x, ŋ, r, l / | / i:, ɪ, ʊ, u:, iə, eə, e, ə, ɜ:, ɔi, əʊ, aʊ, æ, ʌ, a, a:, ɒ, ai, ei, ɔ: /. |
| Wataalamu wa Kifaransa | / s, z, t, d, n, l, ʃ, ʒ, k, g, f, v, ɲ, p, b, m, R, j, ɥ, w / | / i, y, u, e, ø, ɛ, œ, o, ɔ, a, ɛ~, ɑ~, ɔ~ / |
| Wataalamu wa Kiarabu | / ا ب ت ث ج ح خ د ذ ر ز س ش ص ض ط ظ ع غ ف ق ك ل م ن و ه لا ء ي | - |
| Wataalamu wa Kireno | / p, b, t, d, k, g, ɣ, s, ʃ, ʒ, ʤ, ɹ, f, v, l, ʎ, r, w, j, ʁ, m, n, ɲ / | / i, e, ɛ, a, ɐ, o, ɔ, u, ã, ɨ, õ, ũ / |
| Wataalamu wa Kihisapania | / b, k, ʧ, d, f, g, x, l, m, n, ñ, p, r, s, t, w, j, ks, θ / | / a, e, i, o, u / |

**Chanzo: Data za Wataalamu, 2020**

Jedwali linaonesha kuwa katika uwasilishaji wa viashiria vya fonimu za lugha hizi wataalamu wa kila lugha hawakutofautiana kabisa bali wameainisha viashiria vya aina moja kwa kila lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na kihispania.

Kutokana na ushahidi wa hapo juu wa wataalamu wa lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania kutofautiana katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake lipo tatizo la wataalamu kutofautiana lakini ni la kiwango kidogo mno tofauti na kiwango kikubwa kilichobainika kwa wataalamu wa Kiswahili sanifu. Kwa ushahidi huo ilionekana ni vyema kufanya uchunguzi na kugundua ni kitu gani kilichwafanya wataalamu wa Kiswahili sanifu kutofautiana kwa kiwango kikubwa katika uwasilishaji wao wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Uchanganuzi wa idadi ya fonimu na viashiria vyake kwa kila mtaalamu wa lugha hizo za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania taz. Kiambatanisho cha 4.

## 2.10 Pengo la Utafiti

Baada ya Mtafiti kupitia kazi tangulizi amepata ufahamu mpana zaidi kuhusu matatizo ya taaluma ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Ameweza kufahamu kwamba ukiachilia mbali tatizo la utafiti huu, Kiswahili sanifu kina matatizo mbalimbali kulingana na walivyoyabaini baadhi ya wataalamu kama:

i) Khalid, (1977:163) amezungumzia kuhusu tatizo la taathira za wakoloni katika kukisanifisha Kiswahili.

ii) Nchimbi (1991:14) amezungumzia kuhusu tatizo la isharasauti mang’ong’o kama ni fonimu au si fonimu.

iii) Mbaabu, (1995) amezungumzia kuhusu tatizo la usanifishaji wa lugha na mabadiliko ya msamiati katika sarufi ya Kiswahili.

iv) Mgullu, (2001: 69) amezungumzia kuhusu tatizo la sauti ambatano ng’ong’o au nazali.

v) Simala, (2004:39) amezungumzia kuhusu matatizo yanayoikumba lugha ya Kiswahili lazima yachunguzwe na kueleweka kwamba hayo ni masuala ya kijamii.

vi) Khamisi, (2005:11) amezungumzia kuhusu tatizo la kuepukwa kwa baadhi ya sauti za Kiswahili sanifu zinazotokana na lahaja za Kiswahili.

vii) Mayoka (2007:3) amezungumzia kuhusu tatizo lugha nyingine katika matumizi ya maneno ya Kiswahili.

viii) Gromova, (2008:118) amezungumzi kuhusu makosa yanayofanywa mara kwa mara katika matumizi ya Kiswahili sanifu

Wataalamu hao katika kazi zao hizo hakuna aliyechunguza kuhusu kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Pia, hadi sasa sikupata kuona kufanywa utafiti wa mada hii kwa Tanzania na ndio sababu utafiti huu ukaamua kuliziba pengo hilo la kutofanywa kwa utafiti wa mada hii na kwa kiwango hiki cha taaluma. Ushahidi wa hili ulijitokeza katika tahakiki za upitiaji wa kazi tangulizi kama zilivyowasilishwa hapo awali. Matatizo mengi yaliyowasilishwa katika kazi hizo ndio yaliyotoa nguvu na raghaba ya kufanyika utafiti huu kwa mada hiyo ya utafiti kwa nia ya kuliziba pengo lilioachwa na wataalamu hao.

## 2.11 Nadharia ya Utafiti

Juma, (2017:2) amehoji juu ya lengo na umuhimu wa nadharia kuwa ni muongozo kwa jambo lolote la kujifunza na kupata taaluma kwa kusema:

> Kila linalofanywa na binadamu ili liwe ni lenye kufanikiwa linahitaji mwongozo ambao utakuwa dira kwa jambo hilo. Mwongozo wa jambo lolote sharti uwe na vigezo ambavyo vitawawezesha watu wengine

kujifunza na kulifahamu jambo hilo. Kutokana na vigezo hivyo, nadharia huwajengea utaratibu maalumu unaowawezesha na kuainisha ubora na athari unaojitokea katika jambo hilo.

Maelezo haya ya Juma yana mnasaba wa moja kwa moja na utafiti huu kuhusu taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Hivyo utafiti huu nao lazima uwe na nadharia ya muongozo au kanuni ya kufuatwa. Nadharia ilizoongoza utafiti huu ni nadhari ya Lyons (1968) ya Umbo-Sauti Maumbo Kimatumizi. Pamoja na nadharia hiyo, nayo kanuni ya Trubetzkoy, (1939/1969) ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili imejumuika katika kuongoza na kuelekeza ufumbuzi wa uwasilishaji wa fonimu za Kiswahili sanifu.

### 2.11.1 Nadharia ya (Lyons, (1968) Lugha ni Umbo-Sauti Maumbo Kimatumizi

Nadharia ya Lugha ni Umbo-Sauti Maumbo Kimatumizi ndio iliyoongoza katika utafiti huu. Lyons (1968) ni muasisi wa nadharia hii inayodai kuwa maneno ya lugha sanifu yapimwe kwa kazi zao katika sentensi na sio kwa muundo wa ujenzi wa sentensi. Nadharia hii kama ilivyonukuliwa na Massamba na waenzake (2001:54) kwa ujumla wake inahoji kuwa neno linaweza kufafanuliwa kwa kuchunguza isharasauti zinazounda umbo zima kiotografia zinazotumika katika kuliandika neno lake na matumizi yake kwa kuchunguza kile kinachowakilishwa kimaana na neno linalohusika katika lugha mahsusi. Lyons anatoa hoja kuwa, lugha kama Kiswahili sanifu imejengwa kwa fonimu zenye kutoa maana kulingana na matumizi yake mahsusi. Hii ina maana kwamba, neno la lugha kama ya Kiswahili sanifu msingi wake huanzia na fonimu katika muundo wa neno lenye mfuatano wa konsonanti (kontoidi) na irabu (vokoidi) (Maganga 1984:12). Mfano wa neno [ b - a - h - a - t - i ] au mfuatano wa konsonanti, konsonanti na irabu, mfano neno [ m - t - o ] au mfuatano wa irabu, konsonanti na irabu, mfano wa neno [a - m - a] au mfuatano wa irabu,

irabu, konsonanti na irabu, mfano wa neno [ a - i - b - u ] au mfuatano wa konsonanti, irabu, irabu, mfano wa neno [ w - a - o ] au [ y- a - o ].

Nadharia hii ina uhusiano mkubwa na utafiti huu kwa sababu katika maneno ya lugha ya Kiswahili sanifu kila fonimu moja huwa na maana pambanuzi au kazi tofauti kulingana na nafasi zao katika neno (Massamba, 2004). Mfano manano **[ p ]** ika (ivisha chakula kwa kutumia moto) na **[ t ]** ika (tikisika kwa kitu). Maneno hayo nayo yanatofautiana kiimaana kwa sababu ya tofauti ya sifa bainifu za fonimu **/ p /** ya midomo na fonimu **/ t** / ya ufizi. Mfano mwengine ni wa isharasauti: **[ k ]** na **[** $k^h$ **]** huwa na maana tofauti kikazi katika umbo moja. Tofauti ya maana husababishwa na matamshi ya **[ k ]** bila mpumuo na **[** $k^h$ **]** ya mpumuo. Mfano wa neno **[ k ]** aa (la moto) na **[** $k^h$ **]** aa (samaki) katika lugha ya Kiswahili sanifu yanatofautiana kimaana kwa sababu ya tofauti ya matamshi na maumbo ya isharasauti zao tu (Ferdinand de Saussure)[13].

Nadharia hii inathibitisha kuwa lugha ni mfumo wa kanuni zinazoundwa na wana lugha wenyewe katika maeneo ya fonimu na matamshi yake. Kwa mtazamo wa nadharia hii, ndio maana fonimu za lugha ya Kiswahili sanifu hutambulikana kwa kutofautisha maana kupitia mtoano katika Jozi Sahili za maneno ya lugha hiyo. Mfano, maneno ***salio*** (kwa maana ya kilichobakia) na ***kalio*** (kwa maana ya kifaa cha kukalia). Kwa mujibu wa Nchimbi (1992:2), maneno haya yanatofautiana kimaana kwa isharasauti **[ s ]** na **[ k ]** katika Kiswahili sanifu kwa kutumia njia ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili ya maneno kama:

[ **s** a l i o ]

[ k a l i o ]

Katika jozi hii isharasauti **[ a ]** imeitoa isharasauti **[ a ]**, isharasauti **[ l ]** imeitoa isharasauti **[ l ],** isharasauti **[ i ]** imeitoa isharasauti **[ i ]** na isharasauti **[ o ]** imeitoa isharasauti **[ o ].** Hivyo isharasauti **[ s ]** na **[ k ]** zilizobakia bila ya kutoana ni fonimu za Kiswahili sanifu na ndizo sauti zilizobadilisha maumbo na maana ya maneno hayo. Nadharia hii inaungwa mkono na Ager (2014) pale alipohoji:

> Utumiaji wa matamshi sahihi ni namna ya kutamka maneno katika hali inayozingatia kanuni zote za kisarufi za maneno hayo. Njia hiyo inayawezesha maneno kutoa maana inayoeleweka. Neno linapotamkwa katika hali isiyo sahihi, husababisha moja ya mambo mawili yafuatayo kutokea: i) Kutokea kwa maana inayotofautiana na ile inayokusudiwa. Mfano: Tafadhali niletee huo mlago badala ya Tafadhali niletee huo mlango. ii). Kutokea kwa maneno ambayo hayaeleweki. Mfano: Mzee Masoud ameshinda hapu leo badala ya Mzee Masoud ameshinda hapa leo.

Maelezo haya ni sahihi kabisa na yanathibitisha juu ya umuhimu wa matamshi sahihi ya fonimu za maneno katika lugha. Matamshi ndio msingi wa kufahamika kinachokusudiwa kimaana kwani msingi wa matamshi ya fonimu za lugha ni kupata maana inayoeleweka na wanalugha wenyewe. Katika mkabala huu, tunagundua kuwa lugha msingi wake ni vipashio vya fonimu zinazojenga silabi nazo hujenga maneno nayo hujenga tungo nazo hujenga sentensi na hatimaye sentensi hujenga lugha. Kwa mkabala huo tunaweza kusema kuwa lugha hujengwa kwa idadi ya fonimu zake mahsusi na bila ya idadi ya fonimu mahsusi hakuna lugha. Utaratibu huu wa fonimu kuwa ni sababu ya lugha unawakilishwa kwa mchoro ufuatao:




**Chanzo: Data za utafiti 2020**

**Mchoro Nam. 2.3: Vipashio vya Lugha ni Umbo-Sauti Maumbo Kimatumizi**

Mchoro 2.3 unabainisha kuwa asili ya lugha ni fonimu yenye maana ambayo ikiungana na fonimu nyingine ya lugha hiyo hujenga silabi na silabi zikiungana hujenga maneno yenye maana na maneno yakiungana hujenga tungo na tungo zikiungana hujenga sentensi kwa lengo la kuwawezesha wanalugha wa lugha kama Kiswahili kuwasiliana na wanajamii wenzao wa lugha hiyo.

### 2.11.2 Kanuni ya Trubetzkoy (1939/1969) ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili

Kanuni ya Trubatzkoy ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili nayo ina nafasi kubwa ya kuongoza uchanganuzi wa idadi ya fonimu katika utafiti huu. Ni kanuni ya kisayansi inayoibua idadi ya fonimu zinazojenga maneno katika lugha za kusemwa na kuandikwa ikiwemo lugha ya Kiswahili. Kwa kuthibitisha ukweli wa kanuni hii namna inavyoibua fonimu za Kiswahili, hebu tuangailie matumizi yake katika jozi zifuatazo:

**Jozi ya Kwanza**

| | | | |
|---|---|---|---|
| [ s | a | w | a ] |
| [ s | a | s | a ] |
| [ s | a | k | a ] |
| [ s | a | b | a ] |
| [ s | a | g | a ] |

**Jozi ya Pili**

| | | | |
|---|---|---|---|
| [ p | i | m | a ] |
| [ l | i | m | a ] |
| [ z | i | m | a ] |
| [ d | i | m | a ] |
| [ h | i | m | a ] |

Baada ya kutumika kanuni ya Nitoe Nikutoe katika jozi ya kwanza zimebaki isharasauti [ w, s, k, b, g ] na katika jozi ya pili zimebaki isharasauti [ p, l, z, d, h ]. Hivyo basi, isharasauti / w, s, k, b, g, p, l, z, d, h / ni fonimu za Kiswahili sanifu. Dhana ya Jozi Sahili, Fischer (1975) ameiita Jozi ya Mlinganuo Finyu kama alivyonukuliwa na Mgullu, (2001:62). Hii ni jozi yenye tofauti ndogo sana ya kifonolojia inayojitokeza katika nyanja za umbo, matamshi na maana baina ya maneno mawili au zaidi.

Kutokana na mifano ya jozi ya kwanza na ya pili za hapo juu, inakubalika kuwa kwa kutumia kanuni ya Nitoe Nikutoe yaani, mtoano wa isharasauti katika Jozi Sahili hupatikana fonimu za Kiswahili sanifu. Kanuni hii inaweza kutumika katika lugha zote zenye maneno, msamiati au leksikoni (Foley na Thompson, 2003:4). Maneno yenye maana msingi wao ni kuundwa kwa isharasauti mojamoja ambazo ndizo fonimu kwa lugha ya kilughawiya katika tawi lake la fonolojia. Muelekeo wa kanuni hii una msingi thabiti wa kuasisiwa na Trubetzkoy (1939) - *Travaux du Cercle Linguistics de Prague* na ndio inayofuatwa katika kuziwasilisha fonimu za Kiswahili sanifu katika utafiti huu pamoja na kuangalia usahihi wa matamshi wa maneno yaliyoundwa na fonimu hizo za Kiswahili sanifu.

## 2.12 Dhana na Sifa ya Jozi Sahili

### a) Dhana ya Jozi Sahili

Jozi Sahili ni maneno mawili au zaidi ya lugha moja yenye kufanana kwa kuwa na isharasauti sawa isipokuwa isharasauti moja tu katika kila neno ambayo huyafanya maneno hayo kuwa na maana tofauti. Isharasauti hizo tofauti ndizo zilizosababisha kuwepo tofauti ya umbo na maana ya maneno hayo katika lugha hiyo (Besha, 2007 na Massamba, 2010). Mfano wa Jozi Sahili katika Kiswahili sanifu kuna maneno: **[ s**abuni na **z**abuni **], [ h**ataki na **h**amaki **], [ s**ema na **h**ema **]**. Kutoka lugha ya Kiingereza, kuna maneno kama **[** ***s**ee* (kuona) na ***b**ee* (nyuki) **]**, **[** ***h**and* (kiganja) na ***l**and* (ardhi) **]**, **[** ***s**oon* (muda si mrefu) na ***m**oon* (baramwezi) **]**. Kutoka lugha ya Kiarabu kuna maneno kama **[** (aliandika) **كتب** na (alichuma) **كسب ]**, **[** (kutokuwa) **لم** na (ngapi) **كم ]**, **[** (ng'ombe) **بكرة** na (ngozi) **بشرة]** Jozi hizi za maneno katika lugha hizo hujuilikana kuwa ni Jozi Sahili kwa kuwa na isharasauti zinazofanana isipokua isharasauti mojamoja tu (isharasauti zilizokozeshwa) kutoka kila neno la jozi hizi kama yanavyobainika hapo katika jozi za mifano ya maneno ya lugha hizo za Kiswahili, Kiingereza na Kiarabu.

### b) Sifa za Jozi Sahili

Ili Jozi Sahili ya maneno itimie kuwa Jozi Sahili lazima iwe na:

ix) Maneno mawili au zaidi kutoka lugha moja.

x) Maneno yenye idadi sawa ya isharasauti isipokuwa isharasauti moja tu katika kila neno.

xi) Maneno yenye kutofautiana kwa isharasauti mbili au zaidi katika kila jozi.

xii) Maneno yenye maana kisemantiki katika lugha hiyo.

xiii) Maneno yenye kuruhusu kipimo cha Nitoe Nikutoe kwa isharasauti zake zote isipokuwa isharasauti moja tu katika kila neno.

### 2.13 Sifa Bainifu za Fonimu

Tafiti zinaonesha kwamba, matamshi sahihi ya fonimu zilizomo katika maneno ya lugha kama Kiswahili, hutegemea sifa bainifu za fonimu hizo. Sifa bainifu za fonimu huufanya ujumbe wa maneno yaliyotamkwa ukubalike na uheshimiwe. Aidha, maneno hayo humfanya mtu asikilize ujumbe kulingana na jinsi ya maneno yalivyotamkwa. Hakuna kanuni mahsusi za matamshi zinazoweza kutumiwa na lugha zote. Lugha nyingi kikiwemo Kiswahili sanifu, huandikwa kwa viashiria vya herufi za alfabeti zenye matamshi maalumu. Mbali na viashiria vya alfabeti za Kilatini, kuna viashiria vya alfabeti za Kigiriki, Kirumi, Kiebrania, Kirusi, Kichina Kihindi na Kiarabu. Kwa kawaida, viashiria vya herufi hizi husimamia neno au sehemu ya neno kimatamshi ili kupata ujumbe uliokusudiwa. Maelezo haya yanakubalika na yana uhusiano wa moja kwa moja na kanuni ya Nitoe Nikutoe inayotumika katika kuzibaini fonimu halisi za Kiswahili sanifu katika utafiti huu. Sababu moja wapo ya malengo ya utafiti huu ni kuhusu suala zima la kufahamu idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

### 2.14 Hitimisho

Katika sura hii imetuonesha kuwa, suala la kutofautiana kwa wataalamu katika idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu lipo kama lilivyobainishwa katika mapitio ya machapisho anuwai katika sura hii. Tathmini inaonesha kuwa, marejeo hayo yamewasilisha ili kuthibitisha tatizo lililokikumba Kiswahili sanifu katika eneo la wataalamu kutofautiana katika idadi ya fonimu na viashiria vyake. Zaidi ya hayo, sura iliona ni vyema kukawa na nadharia na kanuni maalumu kama zilivyobainishwa hapo juu

kuhusiana na taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake ili iwe muongozo wa kuthibibisha uchanganuzi na matokeo ya data za utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inabainisha mbinu maalumu za utafiti zilizotumika katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data ili kuyafikia malengo yaliyokusudiwa ya utafiti huu. Mbinu hizo mahsusi kwa ajili ya utafiti huu zimejumuisha mpangilio wa utafiti, uteuzi wa eneo la utafiti, uteuzi wa idadi pamoja na aina ya Wasailiwa. Aidha, sura imebainisha uteuzi wa vifaa vya kukusanyia data kutoka vyuo vikuu pamoja na mbinu za uchanganuzi wa data zilizokusanywa kutoka kwa Wasailiwa wateule wa utafiti huu.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti kijiografia ni pahali ambapo mtafiti alikwenda kukusanya data. Kwa mujibu wa Bailey (1994), eneo la utafiti ni pahali mahsusi ambapo data za utafiti hukusanywa kwa lengo la kuweza kuyajibu maswali ya utafiti kwa nia ya kuyafanyia kazi malengo mahsusi ya utafiti. Katika mkabala wa uteuzi wa eneo la utafiti huu, limechaguliwa eneo la Zanzibar (Unguja katika Wilaya za Magharibi "A" na "B").

Uteuzi wa eneo la Zanzibar kwa upande mmoja, ulitokana na ukweli kwamba Kiswahili sanifu msingi wake ni lahaja ya Kiunguja-Mjini, moja kati ya lahaja kuu za Zanzibar ambayo takriban Wazanzibari wengi wanaisema na wanaitumia lahaja hiyo katika shughuli zao rasmi na za kawaida. Hivyo, kulikuwa na matumaini makubwa kwamba, data zitakazopatikana katika eneo hili kutokana na usaili wa Hojaji na Mahojiano, zitaambatana na mantiki ya ubora na ukweli halisi wa matumizi sahihi ya Kiswahili sanifu kutokana na utamaduni wa Waswahili wenyewe pamoja na wakaazi wenyeji wa eneo hilo.

Katika eneo hili viliteuliwa vyuo vikuu vinne ambavyo ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kiliopo Beit-ras na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalim Nyerere (MNMA) kiliopo Bububu. Vyuo viwili hivi viko katika Wilaya ya Magharibi “A”. Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU) kiliopo Tunguu na Chuo Kikuu cha Sumait (SU) kiliopo Chukwani. Vyuo hivi viwili vipo wilaya ya Magharibi “B”. taz. Ramani ya Eneo la utafiti, Kiambatanisho cha 7. Vyuo hivyo vimeteuliwa kwa sababu ndivyo vinavyofundisha taaluma ya lughawiya ya Kiswahili na huko SUZA pia kunafundishwa lughawiya za, Kiingerza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania.

Kitaaluma, utafiti huu umewahusisha wanafunzi wa shahada ya kwanza ya Kiswahili-lughawiya wa mwaka wa tatu, wanafunzi wa shahada ya umahiri ya Kiswahili-lughawiya, wahadhiri wanaofundisha taaluma ya fonolojia ya Kiswahili kutoka vyuo vikuu hivyo vilivyotajwa hapo juu na wahadhiri wanaofundisha lughawiya za lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania kutoka SUZA tu. Utafiti huu, kwa upande wa mada hasahasa, umejikita katika kuchunguza vipengele vya sababu na athari za wataalamu zaidi ya 35 kutofautiana katika idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

Hivyo, kulikuwa na matarajio makubwa kuwa, data za Wasailiwa hao zitakuwa za kitaalumu juu ya idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu. Data zilizokusanywa zilijaribu kulinganishwa na idadi ya fonimu na viashiria vyake zilizobuniwa mwaka 1930 na Wazungu na kuweza kuona hali halisi ya idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu cha hivi sasa. Uchunguzi pia ulibaini kuwa baadhi ya Wasailiwa waliokuwemo katika vyuo hivi vinne walitoka sehemu tofauti za Zanzibar na Tanzania kwa jumla. Kitaaluma, utafiti huu ulijikita zaidi katika kuchunguza idadi ya fonimu na viashiria

vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu kulingana na matumizi ya maneno katika nyanja za utamaduni, siasa, uchumi, mazingira, elimu, sayansi na ufundi.

## 3.3 Mpango wa Utafiti

Mpango wa utafiti kwa mujibu wa Ponera (2019: 10-11) yeye ameuita mkabala wa utafiti ambao unafahamika kuwa una mikabala miwili. Mkabala wa kwanza ni wa kitakwimu na mkabala wa pili ni wa kutumia maelezo ya ufafanuzi katika kutafuta maarifa ya kutatua matatizo fulani. Kwa mujibu wa mikabala hiyo ya Ponera mpango wa utafiti ni muongozo wa kuendesha utafiti kwa kiwango cha juu cha udhibiti matatizo yanayoweza kuingilia uhalali wa matokeo ya utafiti na kuonesha jinsi utafiti utakavyofanyika tangu mwanzo hadi mwisho. Mpango wa utafiti ndio unaotoa picha jinsi ya utafiti utakavyofanyika na vipi data zitakavyokusanywa na zitakavyochambuliwa au zitakavyochanganuliwa (Neuman & Robson, 2009 na Kothari, 2004).

Kutokana na dhana hii ya mpango wa utafiti ya akina Neuman & Robson na Kothari, inakubalika kuwa, mpango wa utafiti ndio unaojenga makusudio ya utafiti yanayotokana na suala la utafiti wenyewe. Kwa hali hii utafiti huu, umetumia mikabala miwili yaani, mkabala wa takwimu kwa kipimo cha wingi wa matokeo kwa hali yake pamoja na mkabala wa kimaelezo pamoja na kutoa sababu za matokeo ya maelezo ili kubaini ubora wa matokeo ya wingi wa kipimo. Hii ndio sababu kubwa ya utafiti huu kuchagua vipimo vyote viwili yaani takwimu kwa kuangalia wingi wa matokeo ya Wasailiwa pamoja na maelezo ya kutoa sababu za uoni wao juu ya majibu yao (Creswell, 2009).

## 3.4 Sampuli

Sampuli ni baadhi ya Wasailiwa wanaoteuliwa na kuwa wawakilishi kutoka kundi kubwa la Wasailiwa. Tafiti zimebaini kuwa si rahisi kwa mtafiti kuweza kuwatafiti watu wote wa

jamii anayoitafiti bali huchagua au huteua sampuli tu ya kuwawakilisha jamii nzima (Bryman 2004). Moja kati ya masharti ya utafiti wa kitaalamu ni kuwashirikisha Wasailiwa wanaotumika kutoa taarifa kamili za utafiti ambazo huchambuliwa na kupata matokeo sahihi yanayohusiana na malengo ya utafiti (Mc Dale, 1999). Kwa jumla, utafiti huu uliazimia kuteua sampuli ya Wasailiwa 130. Idadi hii ilikusudiwa kuteuliwa bila ya mpangilio mahsusi kutoka kwenye vikundi vya asili vinavyoitwa klasta. Miongoni mwa vikundi hivyo ni wanafunzi wa Digirii mwaka wa tatu, wanafunzi wa umahiri, wahadhiri wa Kiswahili na wahadhiri wa lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania. Miongoni mwa vikundi hivyo vya sampuli ni kutoka SUZA ilikuwa wapatikane wahadhiri wa Kiswahili 30, wahadhiri wa lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania 20, wanafunzi wa Digrii ya Umahiri 25, wanafunzi wa Digrii mwaka wa tatu 10. Kutoka vyuo vya ZU, SU na MNMA vilipangiwa vitoe jumla ya Wasailiwa 45 miongoni mwao kila chuo kitoe wahadhiri wa Kiswahili 5 na wanafunzi 10 wa Digrii mwaka wa tatu.

### 3.4.1 Usampulishaji

Jumla ya sampuli halisi ya Wasailiwa waliopatikana ni 115 kutoka katika vyuo vikuu vinne vilivyoteuliwa. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) waliteuliwa jumla ya Wasailiwa 70 miongoni mwao ni wahadhiri wa Kiswahili-lughawiya 25, wahadhiri wa lughawiya za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania 15 ambapo kila lugha moja waliteuliwa wahadhiri watatu. Kwa upande wa Wasailiwa wanafunzi waliteuliwa jumla ya Wasailiwa 30 miongini mwao ni wanafunzi wa Digirii ya Kwanza mwaka wa tatu Wasailiwa10 na Wasailiwa wanafunzi wa Digirii ya Umahiri 20. Kutoka Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU), Chuo Kikuu cha Sumait (SU) na Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya

Mwalimu Nyerere (MNMA) waliteuliwa jumla ya Wasailiwa 45 miongoni mwao ni Wasailiwa wahadhiri 15 ambao kila chuo waliteuliwa wahadhiri watano na Wasailiwa wanafunzi 30 ambao, kila chuo waliteuliwa wanafunzi 10.

Sababu ya kutaka kuwa na idadi hiyo na makundi hayo matatu ya wanafunzi wa Digirii wa mwaka wa tatu, wahadhiri wa Kiswahili na wahadhiri wa Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania ni kupata data za Wasailiwa waliowakilisha jamii ya washiriki kutoka vyuo vikuu ambapo ni eneo la wasomi katika taaluma fonolojia ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu uliamua kuwa na idadi mahsusi ya Wasailiwa kutoka kila chuo kupitia njia ya uteuzi wa bahati nasibu. Uteuzi wa bahati nasibu hutoa fursa kwa kila mhojiwa wa utafiti kuwa na nafasi sawa ya kutoa taarifa za utafiti zinazohitajika kulingana na maswali yanayoulizwa. Makundi ya Wasailiwa hao yaliteuliwa kutokana na kwamba, suala la taaluma ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu, linahusiana moja kwa moja na Wasailiwa hao kuliko watu wengine katika jamii ya Wazanzibari. Hivyo, mtafiti aliwahusisha Wasailiwa hao kwa mtazamo huo ili utafiti wake uwe wa ufanisi na uhakika wa data alizozikusanya na kuzichambua. Ufafanuzi wa Wasailiwa waliteuliwa na jinsi walivyopatikana katika vyuo vikuu vilivyoteuliwa ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Nam. 3.1: Sampuli ya Wasailiwawa Usaili wa Hojaji**

| Vyuo Vikuu | Wanafunzi wa Digrii Mwaka 3 | Wanafunzi wa Umahiri | Wahadhiri wa Kswahili | Wahadhiri wa Kigeni | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| The State University of Zanzibar (SUZA) | 10 | 20 | 25 | 15 | 70 |
| Zanzibar University (ZU) | 10 | - | 5 | - | 15 |
| Sumait University (SU) | 10 | - | 5 | - | 15 |
| Mwalimu Nyerere Memorial Academy (MNMA) | 10 | - | 5 | - | 15 |
| Jumla | 40 | 20 | 40 | 15 | 115 |

**Chanzo: Data ya Wasailiwa, 2020**

Jedwali Nam. 3.1 linabainisha sampuli ya jumla ya Wasailiwa 115 walioteuliwa kutoka vyuo vikuu vinne vya SUZA, ZU, SU na MNMA wakiwemo wanafunzi 40 wa Digrii mwaka wa tatu, miongoni mwa hao kila chuo waliteuliwa wanafunzi 10. Wanafunzi 20 wa Digirii ya Umahiri waliteuliwa kutoka SUZA.  Waliteuliwa wahadhiri wa Kiswahili 40 miongoni mwao wahadhiri 25 waliteulwa kutoka SUZA na 15 waliteulwa kutoka vyuo vyengine ambapo 5 walitoka ZU, 5 walitoka SU na 5 walitoka MNMA. Wasailiwa 100 ni wenye taaluma ya fonolojia ya Kiswahili sanifu na Wasailiwa15 wenye taaluma ya fonolojia ya lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania.  Miongoni mwa Wasailiwa hao 15 Wasailiwa 3 wenye taaluma ya fonolojia ya Kiingereza, 3 wenye taaluma ya fonolojia ya Kifaransa, 3 wenye taaluma ya fonolojia ya Kiarabu, 3 wenye taaluma ya fonolojia ya Kireno na 3 wenye taaluma ya fonolojia ya Kihispania. Kati ya Wasailiwa115 Wasailiwa100 waliteuliwa kushiriki kujaza maswali ya usaili wa Hojaji ya

Utafiti huu (Kiambatanisho cha 2) na Wasailiwa 15 wa lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania waliteuliwa kujibu maswali ya usaili wa Mahojiano (Kiambatanisho cha 3). Miongoni mwa Wasailiwa hao kuna Wasailiwa wa jinsi zote mbili yaani, wanaume na wanawake. Wasailiwa hao waliombwa kwanza, kukubali kwa ridhaa zao kujaza usaili wa Hojaji na kujibu usaili wa Mahojiano kwa ajili ya kupata taarifa za utafiti huu kuhusu kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu. Katika hali halisi ya ukusanyaji data nyanjani yaani, vyuoni, jedwali linatubainishia kuwa mtafiti alifanikiwa kuwapata Wasailiwa hao kutoka vyuo vyote vinne vilivyoteuliwa kwa njia ya bahati nasibu na walipatikana kwa wingi.

### 3.4.2 Taarifa za Wasailiwa

Taarifa za Wasailiwa zilizojadiliwa katika utafiti huu ni jinsi, umri na kiwango cha elimu cha kila mhojiwa kama ifuatavyo:

#### a) Jinsi za Wasailiwa

Wakati wa ukusanyaji data kutoka kwa Wasailiwa, mtafiti alikuwa anazingatia uwiano na usawa wa kijinsi. Jambo hili limefanyika ili kupata mawazo ya pande zote mbili za jinsi yaani, jisi ya wanaume na jinsi ya wanawake ili kuondoa dhana ya mfumo dume wa kuhoji aina moja tu ya jinsi ya kiume na kuisababisha kuisemea jinsi nyingine ya kike. Idadi halisi ya jinsi za Wasailiwa imebainishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Nam.3.2: Wasailia Walioteuliwa kwa Kigezo cha Jinsi**

| WasailiwaWanafunzi | Masomo ya Wasailiwa | Wanaume | Wanawake | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| SUZA | Digrii Mwaka 3 | 5 | 5 | 10 |
| ZU | Digrii Mwaka 3 | 5 | 5 | 10 |
| SU | Digrii Mwaka 3 | 5 | 5 | 10 |
| MNMA | Digrii Mwaka 3 | 5 | 5 | 10 |
| SUZA | Umahiri | 13 | 7 | 20 |
| Jumla | | 33 | 27 | 60 |
| Wahadhiri | Lugha | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| SUZA | Kiswahili | 10 | 15 | 25 |
| ZU | Kiswahili | 3 | 2 | 5 |
| SU | Kiswahili | 1 | 4 | 5 |
| MNMA | Kiswahili | 2 | 3 | 5 |
| SUZA | Lugha za Kigeni | 10 | 5 | 15 |
| Jumla | | 26 | 29 | 55 |
| Jumla Kuu | | 59 | 56 | 115 |

**Chanzo: Data za Wasailiwa, 2020**

Jedwali linabainisha aina na jinsi ya Wasailiwa walioshiriki kujaza usaili wa Hojaji na kujibu usaili wa Mahojiano katika utafiti huu kutoka vyuo vinne vilivyoteuliwa. Hojaji ilijazwa jawabu na Mahojiano yalifanyika kuhusu kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu. Jedwali linabainisha kuwa kati ya jinsi hizo, wanaume walikuwa 59 kati ya 115 sawa na asilimia 51.3%) na wanawake walikuwa 56 kati ya 115 sawa na asilimia (48.7%). Hali hii ilimpa faraja mtafiti kwa kupata data ambazo Wasailiwa wake wa jinsi ya kiume na jinsi ya kike walioridhia kushiriki katika kuchangia taarifa za utafiti huu. Kwa hivyo, sababu kuu ya kutumia Wasailiwa wa jinsi zote mbili ni kuweka usawa na kutoa fursa sawa ya kujieleza miongoni mwa wanafunzi

na wahadhiri ili kuondoa upendeleo na kuonekana utafiti umezingatia jinsi moja na kuipuuza jinsi nyingine.

**b) Umri wa Wasailiwa**

Data kutoka eneo la utafiti zinaonesha kuwa Wasailiwa waliohojiwa walikuwa na umri kuanzia miaka 21 hadi 55. Kundi ambalo limechukua idadi kubwa katika utafiti huu ni umri kuanzia miaka 21-29. Kundi hili limekuwa na Wasailiwa wengi kwani utafiti ulilenga wanafunzi wa digrii mwaka wa tatu na wanafunzi wa digirii ya Umahiri. Katika umri huu, vijana wengi wanakuwa vyuo vikuu kusoma Digirii ya Kwanza na wengine Digirii ya Pili (Umahiri). Kundi hili lilikuwa muhimu sana kwa mtafiti kwani ilikuwa rahisi kuona ubora na athari wanaowapata wanafunzi wanaposoma taaluma ya fonimu katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Kundi jingine lilikuwa ni la wahadhiri ambao walikuwa na umri kuanzia miaka 30 hadi 55. Kundi hili lilisaidia kupata data za taaluma ya fonimu za lugha za Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania kwa jumla.

**c) Elimu ya Wasailiwa**

Elimu inamsaidia mtu kuwa na uwelewa wa kuelezea jambo au mambo kwa upana na usahihi zaidi. Katika kuzingatia hilo, mtafiti alitaka kupata watu wenye viwango tofauti vya elimu kuanzia wale wenye Digrii ya Kwanza mpaka Shahada ya Uzamivu. Katika muktadha huo, ndipo mtafiti alipoteua wanafunzi 40 wa Digrii ya Kwanza, mwaka wa tatu na wanafunzi 20 wa shahada ya Umahiri. Aidha, mtafiti aliteua wahadhiri 40 wenye shahada ya Umahiri na wahadhiri 15 wenye shahada ya Uzamivu. Mchanganyiko wa viwango mbalimbali vya elimu ulizingatiwa ili kuona uwiano sawa wa taarifa na maarifa

ya Wasailiwa wa utafiti huu. Kuwatumia Wasailiwa wenye viwango tofauti vya elimu kulimsaidia mtafiti kupata maoni na mitazamo ya viwango tofauti vya watu waliotoa taarifa za utafiti huu hususan kuhusiana katika kuibua sababu na athari za kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika taaluma ya fonolojia ya Kiswahili sanifu.

### 3.5 Mbinu za Ukusanyaji Data

Kwa mujibu wa Massomo na Ngaruko katika Mbogo (2012:91), ukusanyaji data ni kipengele muhimu kwa utafiti wa aina yoyote ile. Ukusanyaji data usiokuwa wa uhakika husababisha kupata matokeo ya utafiti yasiyohalali na yasiyo na ukweli. Mbinu za ukusanyaji data zinazohusiana na uchunguzi, aghlabu hubainika katika njia mbili. Njia ya kutathmini wingi au uchache wa matokeo na njia ya kuchunguza ubora au udhaifu wa matokeo kimantiki. Kama ilivyo kawaida ya utafiti, suala la ukusanyaji data ni la lazima ama kwa njia ya kusoma vitabu, kuchunguza, kupima au kuuliza maswali kupitia usaili. Uzoefu unaonesha kuwa watafiti wengi katika tafiti za kitaaluma ya sayansi ya jamii hutumia njia ya kusoma vitabu na njia ya Hojaji au Mahojiano au huzitumia njia zote hizi kulingana na malengo ya utafiti unaohusika (Blaxter na wenzake 2006:153).

Utafiti huu ulitumia njia mbili za ukusanyaji data; njia ya kwanza ni ya kupitia maandishi kama vile vitabu, makamusi, majarida na mitandao ili kuzikusanya data za kuziunga mkono data za Wasailiwa. Njia ya pili, mtafiti alitumia mbinu ya zana za Hojaji na Mahojiano kwa kuwaomba Wasailiwa kujibu maswali ya Hojaji kwa maandishi na kujibu maswali ya Mahojiano kwa mtindo wa ana kwa ana katika vyuo vilivyoteuliwa. Kwa mujibu wa mbinu hizi inabainika kuwa, utafiti huu ulifanikiwa vizuri kwa uhalali na ukweli katika kuwapata Wasailiwa wengi kutoka vyuo vilivyoteuliwa. Sababu kubwa iliyopelekea uhalali na ukweli wa kupatikana kwa wingi Wasailiwa hao ni usimamizi

mzuri. Mtafiti alichukua juhudi ya kuwaomba baadhi ya wahadhiri wa vyuo hivyo kuwasimamia wanafunzi wao kushiriki kujaza Hojaji (Kiambatanisho cha 2).

Ubora wa data zilizokusanywa kulingana na lengo kuu la utafiti ni kuwapata Wasailiwa wa kutosha katika eneo la utafiti ambao walikuwa ni chachu ya kupata data zilizohitajika kwa ajili ya kuzichunguza na kupata jawabu za uhakika na ukweli ili kuyapima malengo na maswali ya utafiti huu. Pia kwa upande wa ukusanyaji data kwa njia ya Mahojiano, ilimsaidia mtafiti kupata taarifa za papo kwa papo pamoja na kuongeza maswali ambayo hayakuwemo katika Kiambatanisho cha 3 ili kupata taarifa za ziada na za uhakika.

### 3.5.1 Ukusanyaji Data kwa Usaili wa Usaili wa Hojaji

Kwa mujibu wa Massomo na Ngaruko katika Mbogo (2012:91) katika makala yao ya "Data Collection Method," wametoa maana ya *Usaili wa Hojaji* kuwa ni Usaili wa kutumia kifaa cha kukusanyia data ambacho kina maswali yaliyoandikwa na kuwasilishwa kwa Wasailiwa kwa ajili ya kuyajibu kwa mtindo huohuo wa maandishi.

Hojaji inaweza kuwasilishwa kwa njia anuwai kama kuwapelekea Wasailiwa Hojaji hiyo na kuwaelekeza namna ya kuyajibu maswali yake na kuwataka warejeshe majibu baadaye kwa ajili ya kuchanganuliwa. Njia nyingine ni ile ya kuwakusanya Wasailiwa katika kituo kimoja na kuwataka wajibu maswali ya Hojaji hiyo na baadaye kukusanya jawabu zao na kwenda kuzichangnua. Aidha, kuna njia ya kupeperusha Hojaji kwa baruapepe na kuwaelekeza namna ya kuyajibu maswali yake na kuwataka warejeshe majibu baadaye kwa njia hiyohiyo ya baruapepe kwa ajili ya kuchanganuliwa. Mbinu ya Hojaji huwapa uhuru Wasailiwa kujibu maswali wakiwa peke yao bila ya kuonana na mtafiti. Maswali yaliyoulizwa katika usaili wa Hojaji ya Utafiti huu yalifuata utaratibu wa kuyaweka maswali ya uwazi yenye lugha nyepesi inayosomeka kwa urahisi na yanayojibika bila ya

ugumu kwa kufuata maelekezo yake (Alston na Bowles (2007:100-101). Mbinu hii ilitumika kukusanya data kutoka kwa Wasailiwa wanafunzi na wahadhiri wa lughwiya ya Kiswahili. Data zilizopatikana ni za majibu ya maswali kutoka Kiambatanisho cha 2.

### 3.5.2 Ukusanyaji Data kwa Usaili wa Mahojiano

Njia hii ilichaguliwa kutumika katika utafiti huu, kwa Wasailiwa wa lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania ili kupata taarifa za upana kabisa kutokana na uhuru wa Wasailiwa hao katika kujieleza kuhusu taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya lugha zao na katika Kiswahili sanifu. Katika njia hii, mtafiti aliwahoji Wasailiwa watatu kwa kila kikundi cha lugha zao za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania. Usaili wa Mahojiano kwa kila msailiwa moja ulifanyika. Usaili huu pamoja na kuwa uliandaliwa maswali yake maalumu, ulizidisha kuibua maswali zaidi ili kupata taarifa za upana kwa kinachokusudiwa kutafitiwa kwa kila pale ambapo mtafiti alihisi zinahitajika taarifa za ziada. Data zilizopatikana ni za majibu ya maswali kutoka Kiambatanisho cha 3.

### 3.5.3 Ukusanyaji Data kwa Usomaji wa Nyaraka

Usomaji wa nyaraka ni moja kati ya mbinu za utafiti ili kupata data za upili kutoka katika machapisho tangulizi ya taaluma ya lughawiya ya Kiswahili zinazohusiana na utafiti huu. Data za upili katika utafiti huu zimesaidia sana katika kushadidia na kukazia hoja zilizoibuka kutoka katika data za msingi za Wasailiwa wa utafiti huu. Mbinu hii pia ilisaidia sana katika kuimarisha uwasilishaji, uchanganuzi na mjadala wa data za utafiti huu. Kwa kuitumia mbinu hii uwasilishaji na uchanganuzi wa data ulifanyika vyema kama ilivyotokea katika sura ya nne.

### 3.6 Mbinu za Uchanganuzi wa Data

Mbinu za aina mbili zilitumika kuchanganulia data za utafiti huu. Mbinu ya kwanza ni ya ukusanyaji data kwa njia ya Hojaji (Kiambataniho cha 2 na Kiambataniho cha 3) na baadaye kuchunguza kwa tathmini ya asilimia za jawabu za Wasailiwa kwa kutumia vifaa vya majedwali na grafu. Mbinu ya pili ni ya maelezo yaliyotokana na taarifa za vitabuni na mitandaoni na kuzihusisha na data za Hojaji na Mahojiano kwa kuzichanganua kwa kutumia mbinu ya kutathmini ukweli na mantiki za hoja za Wasailiwa zilizojitokeza. Mbinu zote hizo zililenga kupata majibu muwafaka ya tatizo la kutofautiana kwa wataalamu 35 katika idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu kwa kuhusisha vigezo vya sababu, athari na mapendekezo ya Wasailiwa wa utafiti huu.

### 3.7 Uthibitisho wa Data Zilizokusanywa

Data zote zilizokusanywa katika utafiti huu, zinathibitika kuwa ni za kweli kwa sababu zilikusanywa kwa uhakika kutoka kwa Wasailiwa waliopatikana katika vyuo vikuu vinne vilivyoteuliwa. Ubora wa data hizo ni kubainisha kwa kiasi gani utafiti huu ulivyofanikiwa katika kuwapata Wasailiwa waliolengwa kutoka vyuo vikuu hivyo, kwa upande mmoja. Kwa upande wa pili, data zinathibitisha kuwapata kwa wingi Wasailiwa walioteuliwa kutoa taarifa za ukweli na uhakika kwa ajili ya utafiti huu.

### 3.8 Maadili ya Utafiti

Katika taaluma ya utafiti, maadili ni uwajibikaji kitabia kuhusu haki za watu wote tunaokutana nao na kuwashirikisha katika kazi ya utafiti. Uzingatiajiwa malengo ya utafiti na namna ya kuyatumia matokeo ya utafiti kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa jamii.  Lengo la kuzingatia maadili ya utafiti ni kuhakikisha kwamba, mkabala wa utafiti,

vitendo vya utafiti na hatua zote za utafiti hazitakuwa na athari wala udhalilishaji kwa watu wote watakaoshirikishwa katika utafiti unaohusika. Utafiti huu ulihusisha taasisi za serikali na binafsi katika eneo la utafiti ambapo kila sehemu ina taratibu zake. Kabla mtafiti kuanza kazi ya kukusanya data aliomba barua kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ya kumtambulisha sehemu za kufanya utafiti. Mtafiti alitumia barua hiyo kujitambulisha kwa Wasailiwa ili kuwatoa shaka juu ya uhalali wa kuwapo katika eneo hilo kwa ajili ya utafiti huu.

Katika kila chuo kilichoteuliwa, mtafiti alijitambulisha na kuonesha barua ya kibali ili aweze kupata ridhaa ya Wasailiwa wake. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, ni vizuri zaidi Wasailiwa wa utafiti kushiriki kwa ridhaa zao na kuhakikisha usalama na hiyari yao badala ya kulazimishwa (Gilbert, 2008). Kwa hivyo, ili kulinda maadili ya utafiti huu, Wasailiwa waliohusishwa katika utafiti huu ni wale walioridhia kushiriki kwa hiyari zao na kujaza usaili wa Hojaji na kujibu maswali ya usaili wa Mahojiano yaliyoendeshwa na mtafiti mwenyewe na msaada wa wahadhiri wa vyuoni.

Pia, kwa kuwa utafiti huu ulitumia simu ili kurekodi Mahojiano baina ya mtafiti na Wasailiwa, hivyo kabla ya kutumia kifaa hiki, mtafiti aliwajulisha na kuwaomba ridhaa zao Wasailiwa hao. Mtafiti aliwaeleza sababu na umuhimu wa kuwarikodi ambapo hatimaye Wasailiwa hao wote kwa ridhha zao, walikubali kurekodiwa. Vilevile, mtafiti alizingatia suala la usiri na faragha kwa Wasailiwa, ambapo aliwaahidi na kuwahakikishia kwamba, taarifa watakazozitoa zitatumika kwa ajili ya malengo ya utafiti huu peke yake. Kwa kulinda ahadi hii ya usiri aliyoitoa mtafiti kwa Wasailiwa wake, katika matokeo yote ya utafiti huu hakuna ubainishaji wala urejeaji wa majina ya Wasailiwa katika uwasilishaji na uchanganuzi wa data zilizokusanywa. Kwa ufupi, suala la maadili ya utafiti

yalizingatiwa katika mwenwndo mzima wa ufanyaji wa utafiti huu. Mtafiti aliweza kufika maeneo yote ya utafiti kwa kujiamini, kwani alikuwa na barua iliyomtambulisha kwa Wasailiwa na kumruhusu kufanya kazi hiyo katika vyuo vikuu alivyoviteua kufanya utafiti wake.

### 3.9 Hitimisho

Kama ilivyobainika, sura hii ilijadili mbinu anuwai zilizotumika ili kuzipata data za utafiti huu. Pia sura imedokeza juu ya namna data zilivyokusanywa kupitia kwa Wasailiwa mahsusi ambao ni wanafunzi na wahadhiri walioteuliwa kwa idadi maalumu kutoka katika vyuo vyao. Uteuzi wa Wasailiwa hao, ulitokana na sababu zilizokwishaelezwa hapo awali. Pia mbinu ya kuteua Wasailiwa kwa njia ya bahati nasibu na kuwaomba kuyajibu maswali ya Hojaji na Mahojiano ilitumika. Pamoja na mbinu ya uteuzi wa Wasailiwa, sura hii imetubainishia mbinu zilizotumika katika kuzichanganua data zilizokusanywa. Zaidi ya hayo, sura hii imetubainishia zana zilizotumika kwa kuzipata data zilizokusanywa kwa mintaarafu ya kubainisha idadi halisi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchanganuzi wa data zilizokusanywa katika utafiti huu. Data hizo zimetokana na tatizo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza sababu na athari za kutofautiana kwa wataalamu zaidi ya 35 katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

Uwasilishaji na changanuzi wa data za utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Lyons (1968) isemayo: Lugha ni Umbo-Sauti Maumbo Kimatumizi iliyoshirikiana na Kanuni ya Trubetzkoy (1939/1969) ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili. Nadharia na kanuni hiyo kwa pamoja, ndizo zilizoongoza uwasilishaji na uchanganuzi wa data katika utafiti huu. Mtafiti ameweza kuwasilisha na kuchanganua data za utafiti huu kwa nia ya kuchunguza kilichowafanya wataalamu watafautiane. Pia utafiti ulitaka kubaini sababu na athari za kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Hatimaye, utafiti huu ulitaka kuibua mapendekezo ya njia za kutatua tatizo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

## 4.2 Uwasilishaji na Uchanganuzi wa Data

Kwa ujumla, utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi matatu ambapo lengo la kwanza lililenga kuchunguza sababu zilizowafanya wataalamu zaidi ya 35 kutofautiana katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Lengo la pili, lilikusudia kudhihirisha athari za wa wataalamu kutofautiana katika

uwasilishaji wao wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Lengo la tatu lilitaka kupendekeza njia za kurekebisha tatiazo la kutofautiana kwa wataalamu katika idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

Uchanganuzi wa data uliofanywa katika sehemu hii unahusu data zilizokusanywa nyanjani yaani, Chuo Kikuu cha SUZA kiliopo Beitras, wilaya ya Maghribi ‘‘A’’ Chuo Kikuu cha MNMA kiliopo Bububu wilaya ya Maghribi ‘‘A’’, Chuo Kikuu cha SU kiliopo Chukwani wilaya ya Maghribi ‘‘B’’ na Chuo Kikuu cha ZU kiliopo Tunguu wilaya ya Maghribi ‘‘B’’. Malengo mhsusi hayo yalifanyiwa maswali manne yaliyotakiwa yajibiwe na Wasailiwa katika usaili wa Hojaji (Kiambatanisho cha 2). Pia kulikuwa na maswali manne yaliyotakiwa yajibiwe na Wasailiwa wa usaili wa Mahojiano (Kiambatanisho cha 3). Katika uchanganuzi huu, yametumika majedwali na grafu kwa ajili ya kubainisha kwa uwazi uchanganuzi wa data hizo kwa upande wa kupima wingi wa majibu ya Wasailiwa kisilimia. Kwa upande wa pili, palichunguzwa hoja za Wasailiwa kulingana na mantiki na ukweli wa majibu yao waliyoyatoa. Baadhi ya majibu hayo yalihusishwa na nadharia za kanuni za Kiswahili sanifu pamoja na maoni ya wataalamu katika mapitio ya vitabu, majarida na mitandao mbalimbali ili kuyathibitisha ubora wake.

Hatimaye, mtafiti alitoa mwelekeo unaokubalika katika mnasaba wa taaluma ya fonolojia ya Kiswahili sanifu kulingana na uchanganuzi wa data zilivyobainisha ukweli uliopatikana katika kuyafanyia kazi malengo mahsusi ya utafiti huu. Katika uchanganuzi wa usaili wa Hojaji (Kiambatanisho cha 2) Wasailiwa wanafunzi wa Digirii mwaka wa 3, wanafunzi wa umahiri na wahadhiri wa Kiswahili-lughawiya kwa pamoja walijibu maswali manne. Katika uchanganuzi wa usaili wa Majadiliano, Wasailiwa wahadhiri wa lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania waliopo SUZA wao pia

walijibu maswali manne ambapo maswali matatu ni yalayale walioulizwa Wasailiwa wenzao nayo ni kama yanavyoonekana katika Kiambatanisho cha 3. Uchanganuzi halisi wa data zilizokusanywa ni kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Swali la 1 la Usaili wa Hojaji na Mahojiano kuhusu Sababu za Wataalamu Kutofautiana katika Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake

Katika swali hili ulifanyika uwasilishaji na uchanganuzi wa data kuhusu lengo mahsusi la kwanza la utafiti huu. Lengo hilo limechunguza sababu za wataalamu zaidi ya 35 kutofautiana katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu. Ili kufikia lengo hili mtafiti aliunda swali mahsusi la kwanza lililouliza, Ni sababu zipi zilizowafanya wataalamu kutofautiana katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu? Data zilizotumika kujibu swali hili zilitoka kwa Wasailiwa wa usaili wa Hojaji na usaili wa Mahojiano. Majibu yaliyotolewa na Wasailiwa katika kujibu swali hilo yalikuwa kama yanavyoonekana katika Grafu Nam. 4.1 na Grafu Nam. 2 hapo chini:




| | Sababu ya 1 | Sababu ya 2 | Sababu ya 3 | Sababu ya 4 | Sababu ya 5 | Sababu ya 6 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Digirii mwk 3 | 1 | 4 | 8 | 25 | 1 | 1 | 40 |
| Umahiri | 0 | 3 | 7 | 10 | 0 | 0 | 20 |
| Wahadhiri | 1 | 3 | 11 | 20 | 4 | 1 | 40 |
| Jumla | 2 | 10 | 26 | 55 | 5 | 2 | 100 |

Digirii mwk 3 Umahiri Wahadhiri

**Chanzo: Data ya Wasailiwa, 2020**

**Grafu Nam 4.1: Majibu ya Wasailiwa wa Hojaji kuhusu Sababu za Wataalamu Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake**

Sababu ya 1: Tafauti ya viwango vya wataalamu katika taaluma ya fonolojia ya Kiswahili sanifu.

Sababu ya 2: Usanifishaji wa Kiswahili kufanywa na wataalamu wageni yaani, Wazungu ambao waliathiriwa na taaluma za lugha zao.

Sababu ya 3: Wataalamu kuwa huru katika maandishi yao bila ya kusimamiwa na jopo moja la wahariri katika taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake.

Sababu ya 4: Wataalamu kutozingatia kanuni ya kisayansi inazowasilisha idadi ya fonimu na viashiria vyake.

Sababu ya 5: Wataalamu kuathiriwa na mikabala ya fonimu za lugha nyingine za Kiingereza, Kiarabu na Kibantu.

Sababu ya 6: Tofauti za marejeo waliorejea wataalamu walipowasilisha idadi ya fonimu na viashiria vyake.

Grafu linaonesha sababu sita zilizofikiriwa zimewafanya wataalamu zaidi ya 35 kutofautiana katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Sababu ya Wataalamu kutozingatia kanuni ya kisayansi inayowasilisha idadi ya fonimu na viashiria vyake, imetolewa na Wasailiwa 55 sawa na asilimia (55%). Idadi hii ni ya kiwango cha juu kuliko zote na kila kikundi cha Wasailiwa kimeikubali sababu hii kwa idadi kubwa kuliko sababu nyingine. Wasailiwa wanafunzi mwaka watatu 25 kati ya 40 sawa na asilimia (62.5%) wameitoa sababu hii. Wasailiwa wanafunzi wa umahiri 10 kati ya 20 sawa na asilimia (50%) wameitoa sababu hii. Wasailiwa wahadhiri 20 kati ya 40 sawa na asilimia (50%) nao wameitoa sababu hii. Sababu ya Wataalamu kuwa huru katika maandishi yao bila ya kusimamiwa na jopo moja la wahariri katika taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake imetolewa na Wasailiwa 26 sawa na asilimia 26%. Sababu ya usanifishaji wa Kiswahili kufanywa na wataalamu wageni yaani, Wazungu ambao waliathiriwa na lugha zao imetolewa na Wasailiwa 10 sawa na asilimia 10%. Sababu za Tafauti ya viwango tafauti vya wataalamu katika taaluma ya fonimu za

Kiswahili sanifu na Tofauti za marejeo waliorejea wataalamu walipowasilisha idadi ya fonimu na viashiria vyake, kila moja imetolewa na Wasailiwa 2 sawa na asilimia 2%. Hatimaye sababu ya Wataalamu kuathiriwa na mikabala ya fonimu za lugha nyingine za Kiingereza, Kiarabu na Kibantu imetolewa na Wasailiwa 5 sawa na asilimia 5%.

Kwa jumla, sababu zote hizo sita, zinakubalika kwani kila sababu moja kwa kiasi fulani imechangia kuhusu tatizo la kutofautiana kwa wataalamu katika uwasilishaji wao wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Sababu ya Wataalamu kuathiriwa na mikabala ya fonimu na viashiria vya lugha ya Kiingereza, Kiarabu na lugha za Kibantu, sababu hii inaungwa mkono na Batibo (1980:11) alipotanabahisha kwamba, fonolojia ya Kiswahili imeathiriwa sana na lugha nyingine. Hii imetokana na sababu watu wengi wanaoitumia lugha ya Kiswahili wana lugha zao za kwanza yaani lugha mama na Kiswahili ni lugha yao ya pili au ya kigeni walioisoma baadaye. Sababu hizi tunaweza kuzigawa katika sehemu mbili: zile zinazotokana na lugha nyingine za Kibantu na zile zinazotokana na lugha zisizo za Kibantu. Batibo hapa kwa mawazo yake hayo, anasisitiza kuwa lugha ya Kiswahili imepata athari za lugha nyingine kama za Kibantu au za kigeni kama Kiingereza na Kiarabu. Utafiti huu unakubaliana na hoja hii kwani historia inatubainishia kuwa Waingereza ndio wa kwanza waliochangia usanifishaji wa Kiswahili katika miaka ya 1925 hadi 1930. Kwa upande wa pili utafiti uliliuliza swali hilihili kwa Wasailiwa 15 wa lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania. Wasailiwa hao pia walitakiwa kutoa sababu zilizowafanya wataalamu zaidi ya 35 wa Kiswahili sanifu kubainisha idadi tofautitofauti za fonimu na viashiria vyake. Swali hili liliulizwa ili kuona mkabala wao kwa kulifanyia kazi lengo na swali la kwanza la utafiti huu. Jawabu za Wasailiwa hao katika usaili wa Mahojiano ni kama linavyoonekana katika grafu lifuatalo:




| | Sababu ya 1 | Sababu ya 2 | Sababu ya 3 | Sababu ya 4 | Sababu ya 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Wasailiwa wa Kiingereza | 3 | 2 | 3 | 1 | 3 |
| Wasailiwa wa Kifaransa | 2 | 1 | 2 | 1 | 2 |
| Wasailiwa wa Kiarabu | 3 | 3 | 3 | 2 | 3 |
| Wasailiwa wa Kireno | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 |
| Wasailiwa wa Kihispania | 2 | 2 | 3 | 1 | 2 |
| Jumla | 13 | 11 | 14 | 8 | 10 |

**Grafu Nam. 4.2: Majibu ya Wasailiwa wa Mahojiano kuhusu Sababu za Wataalamu Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake**

**Chanzo: Data ya Wasailiwa, 2020**

Sababu ya 1: Wataalamu kutobainisha kanuni walioitumia katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake.

Sababu ya 2: Wataalamu kutofanya utafiti wa kina kwa wazungumzaji na wajuzi wa fonolojia ya Kiswahili sanifu.

Sababu ya 3: Wataalamu kuwa huru kuandika kazi zao bila ya kupitiwa na jopo mahsusi la wataalamu wa idadi ya fonimu na viashiria vyake.

Sababu ya 4: Wataalamu kutoshirikiana kwa kubadilishana mawazo kuhusu idadi ya fonimu na viashiria vya Kiswahili sanifu.

Sababu ya 5: Usanifishaji wa Kiswahili kukosa kupitiwa upya tangu 1930 hadi leo na kubaini kasoro zilizopo.

Grafu linaonesha sababu tano za tatizo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Kwa mujibu wa utafiti huu sababu hizi zote zinakubalika kwani kila sababu moja imekubaliwa na Wasailiwa zaidi ya nusu. Sababu ya Wataalamu kuwa huru kuandika kazi zao bila ya kupitiwa na jopo mahsusi la wataalamu, imetolewa na Wasailiwa wengi kuliko nyingine yaani, Wasailiwa 14 kati ya 15 sawa na asilimia 93.3%. Sababu hii imefuatiwa na sababu ya Wataalamu kutobainisha kanuni waliotumia katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake iliyotolewa na Wasailiwa 13 sawa na asilimia 87.3%. Uzoefu pia unaonesha kuwa jamii ya wasomi wa somo la Kiswahili-lughawiya ndio inayokumbana na taathira za sababu hizi yaani, wanafunzi, wahadhiri na wataalamu wenyewe kwa jumla. Sababu ya Wataalamu kutofanya utafiti wa kina kwa wazungumzaji na wajuzi wa Kiswahili sanifu imetolewa na Wasailiwa 11 sawa na asilimia 73.3%. Tukichunguza hapa namna Wasailiwa wa Hojaji na Wasailiwa wa Mahojiano tunabaini kwamba, mawazo yao yanafanana sana yaani sababu za Wataalamu kutobainisha kanuni, Usanifishaji wa Kiswahili kufanywa na

wageni, Wataalamu kuwa huru na Wataalamu kuathiriwa na mikabala ya lugha nyingine zote sababu hizi zimeainisha na Wasailiwa wa Hojaji na Mahojiano. Sababu hizo zinahitaji kufanyiwa kazi ili kuepusha mkabala mbaya wa tatizo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Wasailiwa hawa wametafautiana katika sababu ya Tafauti ya viwango tafauti vya wataalamu katika taaluma ya fonimu katika fonolojia ya Kiswahili sanifu iliyowasilishwa na Wasailiwa wa Hojaji tu na sababu ya Wataalamu kutoshirikiana kwa kubadilishana mawazo kuhusu idadi ya fonimu za Kiswahili sanifu iliyowasilishwa na Wasailiwa wa Mahojiano tu.

Pamoja na sababu hizo zilizoibuliwa na Wasailiwa wa utafiti huu, uchunguzi pia unaonesha kuwa, sababu zifuatazo zimechangia wataalamu hao zaidi ya 35 kutofautiana katika uwasilisha wa idadi ya fonimu idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu:

i. Baadhi ya wataalamu kuidharau na kutoifuata sera ya lugha ya kudhibiti maandishi ya taaluma za Kiswahili sanifu.

ii. Kuwepo kwa yombo vingi vinavyosimamia lugha kama KAKAMA, BAKITA, BAKIZA badala ya kuwepo chombo kimoja cha kusimamia maandishi ya Kiswahili sanifu kikamilifu.

iii. Mvutano kati ya wataalamu wazawa wa Kiswahili na wataalamu wasio wazawa wa Kiswahili sanifu katika taaluma ya idadi ya fonimu na matamshi yake sahihi na fasaha.

### 4.2.2 Swali la 2 la Hojaji kuhusu Isharasauti Ambatano Ng'ong'o na Mpumuo kama ni Fonimu au si Fonimu

Swali la 2 la usaili wa Hojaji liliwataka Wasailiwa wabainishe ukubalifu wao kwa hoja za kifonolojia kama isharsauti ambatano ng'ong'o [ mb, nd, ng, nj] na isharsauti mpumuo [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] ni fonimu au si fonimu. Majibu yaliyotolewa na Wasailiwa wa Hojaji katika kujibu swali hilo ni kama yalivyo katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Nam. 4.1: Isharasauti Ambatano Ng'ong'o na Mpumuo ni Fonimu au si fonimu**

| Vyuo Vikuu | Wanaf. Digrii 3 | | Wanaf. Umahiri | | Wahadhiri | | Jumla (100%) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ndio | Hapana | Ndio | Hapana | Ndio | Hapana | Ndio | Hapana |
| SUZA | 9 | 1 | 13 | 7 | 23 | 2 | 45 (45%) | 10 (10%) |
| SU | 7 | 4 | - | - | 4 | 0 | 11 (11%) | 4 (4%) |
| ZU | 8 | 1 | - | - | 4 | 2 | 12 (80%) | 3 (3%) |
| MNMA | 5 | 5 | - | - | 3 | 2 | 8 (53.3%) | 7 (7%) |
| Jumla | 29 | 11 | 13 | 7 | 34 | 6 | 76 (76%) | 24 (24%) |

**Chanzo: Data za Wasailiwa, 2020**

Katika jedwali hilo, tunabaini kwamba Wasailiwa 76 sawa na asilimia (76%) wamekubali kuwa isharasauti ambatano ng'ong'o [ mb, nd, ng, nj ] na isharasauti mpumuo [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] ni fonimu katika Kiswahili sanifu. Wasailiwa 24 sawa na asilimia (24%) wao wamekanusha kuwa isharasauti hizo si fonimu. Ukichunguza katika kila kundi la Wasailiwa kati ya wanafunzi wa Digrii mwaka 3, wanafunzi wa Umahiri na wahadhiri wa Kiswahili, waliokubali kuwa isharasauti ambatano ng'ong'o [ mb, nd, ng, nj ] na isharasauti mpumuo [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] ni fonimu ni wengi kuliko waliokataa kuwa isharasauti hizo si fonimu. Pamoja na waliokubali kuwa wengi utafiti huu haukutosheka

na jawabu hilo ulitaka kubaini hoja za kifonolojia za waliokubali kuwa isharasauti hizo ni fonimu ili wathibitishe jawabu lao.

#### 4.2.2.1 Hoja za Isharasauti Ambatano Ng'ong'o na Mpumuo kama ni Fonimu au si Fonimu

Uchanganuzi katika sehemu hii unahusu swali la 2 katika usaili wa Hojaji lililowataka Wasailiwa kutoa hoja za kifonolojia za jawabu zao za swali la 2. Kama tulivyoona katika jedwali 4.2 la hapo juu, Wasailiwa waligawika pande mbili za waliokubali na waliokataa. Waliokubali ni Wasailiwa 76 sawa na asilimia (76%) kuwa isharasauti ambatano ng'ong'o [ mb, nd, ng, nj ] na isharasauti mpumuo [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] ni fonimu. Waliokataa ni Wasailiwa 24 sawa (24%) kuwa isharasauti ambatano ng'ong'o [ mb, nd, ng, nj ] na isharasauti mpumuo [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] si fonimu. Kwa upande wa waliokubali hoja zao katika kujibu swali hilo zilikuwa kama zilivyowasilishwa katika Grafu 4.3 hapa chini:




| | Hoja ya 1 | Hoja ya 2 | Hoja ya 3 | Hoja ya 4 | Hoja ya 5 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanafunzi wa Mwk. 3 | 1 | 6 | 8 | 5 | 3 | 23 |
| Wanafunzi wa Umahiri | 5 | 5 | 0 | 0 | 6 | 16 |
| Wahadhiri wa Kiawahili | 9 | 7 | 0 | 0 | 21 | 37 |
| Jumla | 15 | 18 | 8 | 5 | 30 | 76 |

**Chanzo: Data za Wasailiwa, 2020**

**Grafu Nam. 4.3: Hoja za Wasailiwa Waliokubali Isharasauti Ambatano na Mpumuo ni Fonimu**

Hoja ya 1: Isharasauti [ mb, nd, ng, nj ] na [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] zinatumika kuunda maneno katika lugha ya Kiswahili sanifu

Hoja ya 2: Isharasauti [ mb, nd, ng, nj ] na [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] zinabadilisha maana katika maneno ya Kiswahili sanifu.

Hoja ya 3: Isharasauti [ mb, nd, ng, nj ] na [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] ni katika makundi ya nazali na mpumuo.

Hoja ya 4: Isharasauti [ mb, nd, ng, nj ] na [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] ni katika kundi la sauti ambatano.

Hoja ya 5: Isharasauti [ mb, nd, ng, nj ] na [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] zimepatikana kwa mbinu ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili za maneno ya Kiswahili sanifu.

Grafu linabainisha hoja tano za jumla za Wasailiwa waliokubali kuwa isharasauti ambatano ng'ong'o [ mb, nd, ng, nj ] na isharasauti mpumuo [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] ni fonimu. Kati ya hoja hizo tano, hoja mbilli za Isharasauti hizo zinatumika kuunda maneno katika lugha ya Kiswahili sanifu na Isharasauti hizo zinabadilisha maana katika maneno ya Kiswahili sanifu, si za kifonolojia. Sababu ya Isharasauti hizo zimepatikana kwa mbinu ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili za maneno ya Kiswahili sanifu, hoja hii inakubalika sana kuwa ni ya kifonolojia na pia ni ya kisayansi. Kwa mkabala wa muongozo wa kanuni ya utafiti huu, sababu ya isharasauti hizo zimepatikana kwa mbinu ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili za maneno ya Kiswahili sanifu iliyobainishwa na Wasailiwa wengi kuliko zilizobaki, ndio hasa inayokubalika zaidi kuwa ni sababu ya kifonolojia na kisayansi kuliko hizo nyingine.

Kwa upande wa Wasailiwa waliokataa kuwa, isharasauti ambatano ng'ong'o [ mb, nd, ng, nj ] na isharasauti mpumuo [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] si fonimu, hoja zao ni kama zinavyobainika katika Grafu lifuatalo:




**Chanzo: Data za Utafiti, 2020**

**Grafu Nam.4.4: Hoja za Waliokataa kwamba Isharasauti Ambatano na Mpumuo si Fonimu**

Hoja ya 1: Isharasauti [ mb, nd, ng, nj ] na [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] hazikuwekwa katika jedwali la konsonanti za Kiswahili.

Hoja ya 2: Isharasauti [ mb, nd, ng, nj ] na [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] hazijapata mashiko na zimebainishwa na wataalamu wachache tu.

Hoja ya 3: Isharasauti [ mb, nd, ng, nj ] na [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] bado zina mjadala kwa wataalamu wa fonolojia ya Kiswahili sanifu.

Hoja ya 4: Isharasauti [mb, nd, ng, nj] si fonimu na isharasauti [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] ni alofoni katika Kiswahili sanifu.

Grafu linabainisha hoja nne za Wasailiwa kuhusu isharasauti [ mb, nd, ng, nj ] na [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] kuwa si fonimu. Hoja hizo bado hazioneshi kuwa ni za kifonolojia wala si za kisayansi. Hoja hizo zote zina upungufu na inadhaniwa kuwa, pengine ndio sababu mojawapo iliyowafanya hata hao wataalamu zaidi ya 35 kuweza kutofautiana na kuona kuwa baadhi ya wataalamu ama wameziwacha au wameziepuka baadhi ya fonimu kwa kutokuwa na kanuni ya kisayansi ya kuwasilisha idadi halisi ya fonimu za Kiswahili sanifu. Kwa kweli haijuilikani wataalamu hao wametumia kanuni gani katika uwasilishaji wao wa idadi ya fonimu walizoziwasilisha. Wataalamu hao wote ukimtoa Nchimbi (2008) hawakuonesha kigezo au kanuni walioitumia hadi wakawasilisha idadi zao hizo. Nchimbi alionesha kigezo alichokitumia ambacho ni cha Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili.

Pamoja na hali hiyo, inaonesha kuwa, baadhi ya fonimu za Kiswahili sanifu zimeepukwa kubainishwa na baadhi ya wataalamu hao ama kwa makusudi au kwa kutofanya utafiti wa kina. Khamisi, (2005:5) ametanabahisha juu ya hali hiyo aliposema kwamba, inaonekana wazi kuwa idadi ya sauti ambazo zinapatikana katika lahaja za lugha zenye asili moja na Kiswahili sanifu zenye kuhitaji juhudi kubwa zaidi kujifunza kuzitamka ama zimeepukwa katika Kiswahili sanifu cha leo au zimerahisishwa kwa namna fulanifulani. Mathalan, toni

ambayo ni tabia moja ya lugha nyingi zenye asili moja na lugha ya Kiswahili sanifu na ambayo bado inapatikana katika lahaja kadha za Kiswahili sanifu, imetolewa katika Kiswahili sanifu cha sasa. Hali ya kuziepuka baadhi ya sauti hapa, ni kwa sababu ya kuwarahisishia watu wengine kujifunza Kiswahili sanifu lakini kila lugha lazima ieleze jinsi fonimu zake zinavyotamkwa na wazawa wake. Khamisi kwa maoni yake hayo, anathibitisha kuwa Kiswahili sanifu hakikuzingatia mlingano wa sauti za lahaja za Kiswahili sanifu bali zimeepukwa na matokeo yake ni kulazimishwa kutokuwa na toni katika Kiswahili sanifu kipya ambacho yeye amekiita Kiswahili sanifu cha sasa. Hivyo utafiti huu ulichunguza hali hiyo kwa Wasailiwa wenyewe na kupata toni sahihi kulingana na lugha yao kama itakavyobainika huko mbele katika sura hii.

### 4.1.3 Swali la 2 la Mahojiano kuhusu Idadi na Aina ya Fonimu za Lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania

Wasailiwa walitakiwa kubainisha jumla ya fonimu, idadi ya konsonanti na idadi ya irabu za lugha wanazozifundisha huko SUZA zikiwemo: Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu Kireno na Kihispania. Lengo la swali hili kwa Wasailiwa hawa ni kutaka kulikazia lengo la kwanza la utafiti huu ili kuona kama suala la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake pia lipo katika lugha hizi maarufu za kimataifa kama lilivyobainika katika Kiswahili sanifu? Jawabu ya swali hilo ni kama linavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Nam. 4.2: Idadi na Aina ya Fonimu za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania**

| Lugha | Idadi ya Wasailiwa | Idadi ya na Aina ya Fonimu | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Jumla ya Fonimu | Fonimu Konsonanti | Fonimu Irabu |
| Kiingereza | 3 (100%) | 44/45 | 24/25 | 20 |
| Kifaransa | 3 (100%) | 33/34 | 19/20 | 13 |
| Kiarabu | 3 (100%) | 36/37 | 29/30 | 7 |
| Kireno | 3 (100%) | 31/32 | 2324 | 8 |
| Kihispania | 3 (100%) | 23/24 | 18/19 | 5 |

**Chanzo: Data za Wasailiwa, 2020**

Jedwali linabainisha namna Wasailiwa wa lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania walivyobainisha idadi ya fonimu na aina zake kwa lugha zao wanazozisomesha hapo SUZA walipotakiwa wazibainishe. Kila Kikundi cha Wasailiwa kilitoa jawabu za aina moja kuhusu idadi na aina za fonimu za lugha zao kama ilivyobainishwa hapo juu bila ya kutofautiana kwa kila kikundi. Kwa kila kikundi kilibainisha tofauti ya fonimu moja ya konsonanti lakini katika irabu wote walikubaliana kwa idadi moja kwa kila lugha. Idadi ya fonimu na viashiria vya lugha hizo zimebainishwa kwa uwazi na wataalamu kumikumi kwa kila lugha. taz. Kiambatanisho cha 5.

Kwa bahati data hizi za idadi na aina za fonimu za lugha hizi zinawiyana sana na idadi na aina za fonimu zilizobainishwa na wataalamu wa lugha hizo katika Kiambatanisho cha 5. Bado tofauti inayobainika hapa ni ndogo sana. Hii ni kuthbitisha kuwa bado idadi ya fonimu za lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania, hazijatofautiana sana kama ilivyobainka kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

Kuhusu lugha ya Kifaransa Wasailiwa wake wote watatu, hawakubagua kati ya irabu za kawaida na irabu za ving’ong’o kama zilivyobinishwa na wataalamu katika Kiambatanisho cha 5. Kuhusu Kiarabu Wasailiwa wake wametofautiana kidogo na wataalamu kwa kubainisha irabu saba za fat-ha au fat’hataani, kasra au kasrataani, dhuma au dhumataani na sukun (irabu fupi) na irabu [ aa, ii, uu] (irabu refu) zinazotumika katika lugha hiyo ambazo wataalamu 10 wote hawakuzibainisha kabisa. Irabu saba walizozibainisha Wasailiwa wa Kiarabu ni kama zilivyo katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Nam. 4.3: Irabu za Kiarabu**

| Fonimu Irabu za Kiarabu | Kiotografia | Kifonetiki |
|---|---|---|
| Fat’hatu fupi / ـَ / au Fat-haten / ـً / | a au an | a au $a^n$ |
| Fat’hatu refu / اء / | aa | a: |
| Kasratu fupi / ـِ / au Kasrataani / ـٍ / | i au in | ɪ au $ɪ^n$ |
| Kasratu refu / ء ي / | ii | ɪ: |
| Dhuma fupi / ـُ / au Dhumataani / ‘’ / | a au un | ʊ au $ʊ^n$ |
| Dhumatu refu / أ و / | uu | ʊ: |
| Sukuun / ـْ / | m au n | ’ |

**Chanzo: Data za Wasailiwa, 2022**

Jedwali linaonesha irabu saba zinazopatikana katika Kiarabu kama zilivyoelezwa na Wasailiwa wote watatu wakati wa usaili wa Mahojiano huko nyanjani.

### 4.2.4 Uthibitisho wa Kanuni ya Kisayansi ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili Inavyobainisha Idadi ya Fonimu za Kiswahili sanifu

Uthibitisho wa ubainishaji wa idadi ya fonimu za Kiswahili sanifu kwa kutumia kanuni ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili za maneno ni kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jozi Sahili i): | [ d | a | i ] |
| | [ h | a | i ] |
| | [ n | a | i ] |
| | [ l | a | i ] |
| | [ r | a | i ] |

Katika jozi ya (i) hapo juu, tunabaini kuwa [ a, i ] katika jozi hiyo zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ d, h, n, l, r ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jozi Sahili ii): | [ b | a | a ] |
| | [ j | a | a ] |
| | [ f | a | a ] |
| | [ v | a | a ] |
| | [ k | a | a ] |

Katika Jozi Sahili (ii) hapo juu, tunabaini kuwa isharasauti [ a, a ] katika jozi hiyo zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ b, j, f, v, k ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Jozi Sahili iii): | [ t | u | w | a ] |
| | [ t | u | p | a ] |
| | [ t | u | m | a ] |
| | [ t | u | n | a ] |
| | [ t | u | t | a ] |

Katika Jozi Sahili (iii) hapo juu, tunaona kuwa isharasauti [ t, u, a ] katika jozi hiyo zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ w, p, m, n, t ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Jozi Sahili ya iv: | [ h | a | w | a ] |
| | [ h | a | y | a ] |
| | [ h | a | b | a ] |
| | [ h | a | s | a ] |
| | [ h | a | m | a ] |

Isharasauti [ h, a, a ] katika jozi hiyozinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ w, y, b, s, m ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

**Tanbihi:**

Isharasauti **[ w ]** na **[ y ]** ambazo ni viyeyusho au vilainisho wataalamu wameziita **nusu irabu** kwa kanuni moja tu ya kukaribiana kimatamshi na irabu **[ u ]** na **[ i ]**. Nadhani kwa mujibu wa utafiti huu isharasauti hizi si vyema kuziita nusu irabu au nusu konsonanti, bali ni konsonanti kamili kwa ushahidi ufuatao:

*a)* Isharasauti **[ w ]** na **[ y ]** zimewekwa katika kundi la konsonanti yaani, vipasuo, vipasuo kwamizi, vikwamizi, ving'ong'o, vitambaza, vimadende na viyeyusho.

b) Isharasauti **[ w ]** na **[ y ]** hazikuwekwa katika kundi la irabu yaani, irabu za juu, au nusu juu au kati au nusu chini au chini na wala hazitamkwi mbele wala nyuma ya ulimi kama zinavyotamkwa irabu.

c) Isharasauti **[ w ]** inatamkwa kwa mzuio mwembamba kwenye midomo na isharasauti **[ y ]** inatamkwa kwa mzuio mwembamba kwenye kaakaa gumu.

d) Sifa bainifu za isharasauti **[ w ]** na **[ y ]** ni kikonsonanti yaani, **[ w ]** kiyeyusho ghuna cha midomo wakati **[ y ]** ni kiyeyusho ghuna cha kaakaa gumu.

e) Isharasauti **[ w ]** na **[ y ]** zinakubali kufuatiwa na irabu katika ujenzi wa maneno kwa kufuata kanuni ya konsonanti na irabu kama ka**wa**, **we**ngi, ka**wi**a, **wo**te, **ya**ngu, **ye**tu, mo**yo** na hu**yu.** Kwa ushahidi huu utafiti huu unaona kuwa aina za isharasauti (fonimu) katika Kiswahili sanifu ni mbili tu, yaani konsonanti na irabu nusu irabu inakosa mashiko kutokana na ushahidi wa hapo juu.

Jozi Sahili ya v:

[ ch o k a ]
[ sh o k a ]
[ ny o k a ]

Katika jozi hiyo tunabaini kuwa isharasauti [ o, k, a ] katika jozi hiyozinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ ʧ, ʃ, ɲ ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

Jozi Sahili ya vi:

[ r i th l]
[ r i dh l ]
[ r i ng l ]

Katika Jozi Sahili (v) tunabaini kuwa isharasauti [ r, i, i ] katika jozi hiyo zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ θ, ð, ɠ ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

Jozi Sahili ya vii:

| | | | |
|---|---|---|---|
| [ kh | i | n | i ] |
| [ ch | i | n | i ] |

Isharasauti [ i, n, i ] katika jozi hiyozinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ x, ʧ ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

Jozi Sahili ya viii:

| | | | |
|---|---|---|---|
| [ p | u | nj | a ] |
| [ p | u | ng | a ] |
| [ p | u | mb | a ] |
| [ p | u | nd | a ] |

Isharasauti [ p, u, a ] katika jozi hiyo zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ ή, ɠ, ꞵ, ɗ ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

Jozi Sahili ya ix:

| | | | |
|---|---|---|---|
| [ k | u | mv | ɪ ] |
| [ k | u | mb | ɪ ] |
| [ k | u | nd | ɪ ] |

Isharasauti [ k, u, i ] katika jozi hiyozinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ ɱ, ꞵ, ɠ ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

| Jozi ya Sahili ya x: | [ gh | a | l | a ] |
|---|---|---|---|---|
| | [ nd | a | l | a ] |

Isharasauti [ a, l, a ] katika jozi hiyo zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ ɣ, ɗ ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

| Jozi Sahili ya xi: | [ p | a | t | a ] |
|---|---|---|---|---|
| | [ $p^h$ | a | t | a ] |
| | [ t | a | t | a ] |
| | [ $t^h$ | a | t | a ] |
| | [ k | a | t | a ] |
| | [ $k^h$ | a | t | a] |
| | [ ch | a | t | a ] |
| | [ $ch^h$ | a | t | a ] |

Isarasauti [ a, t, a ] zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ p, $p^h$, t, $t^h$, k, $k^h$, ʧ, $ʧ^h$ ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

**Tanbihi**

Isharasauti [ p, t, k, ʧ ] hutamkwa bila ya mpumuo katika maneno [ paa, taa, kaa, chaa ] na isharasauti [ $p^h$, $t^h$, $k^h$ , $ʧ^h$ ] hutamkwa kwa mpumuo katika maneno [paa, taa, kaa, chaa]. Mpumuo wa matamshi na bila ya mpumuo wa matamshi ndio unaobadilisha maana za maneno hayo kama ilivyokwisha elezwa hapo kabla.

| Jozi ya Sahili ya xii: | [ ch | a | ng | a ] |
|---|---|---|---|---|
| | [ sh | a | ng | a ] |

Isharasauti [ a, ng, a ] katika jozi hiyo zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ ʧ, ʃ ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

Jozi Sahili ya xiii:

| | | | |
|---|---|---|---|
| [ ch | a | l | i ] |
| [ sh | a | l | i ] |
| [ gh | a | l | i ] |

Isharasauti [ a, l, i ] katika jozi hiyo zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ ʧ, ʃ, ɣ ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

Jozi Sahili ya xiv

| | | | |
|---|---|---|---|
| [ ny | e | k | a ] |
| [ fy | e | k | a ] |
| [ ch | e | k | a] |

Isharasauti [ e, k, a ] katika jozi hiyo zinatoana katika kila neno na kubakia isharasauti [ ɲ, ɦ, ʧ ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

Jozi Sahili ya xv

| | | |
|---|---|---|
| [ m | ch | i ] |
| [ n | ch | i ] |

Isharasauti [ ch, i ] katika jozi hiyo zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ m, n ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

**Tanbihi**

Hapa isharasauti [ m, n ] zilikosa kufuatiwa na irabu za wazi na kusababisha kutamkwa kwa mzuio wa alasauti zake na kutoa sauti ya irabu fiche. Irabu fiche hizo hazina kiwakilishi cha kimaandishi bali alama yake ni kapa ambayo ni [ ø ].

Jozi Sahili ya xvi:

| | | |
|---|---|---|
| [ p | a | a ] |
| [ p | e | a ] |
| [ p | i | a ] |
| [ p | o | a ] |
| [ p | u | a ] |

Isharasauti [ p, a ] katika jozi hiyo zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ aː, ɛː, ɪː, ɔː, ʊː ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

Jozi Sahili ya xvii:

| | | | |
|---|---|---|---|
| [ p | aa | z | a ] |
| [ p | oo | z | a ] |
| [ p | uu | z | a ] |

Isharasauti [ p, z, a ] katika jozi hiyo zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ aː, ɔː, ʊː ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

Jozi Sahili ya xviii):

| | | |
|---|---|---|
| [ m | t | ee ] |
| [ m | t | ii ] |
| [ m | t | aa ] |

Isharasauti [ m, t ] zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti [ ɛː, ɪː, aː ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu.

Kwa mujibu wa BAKIZA, (2010) irabu hizo zimeainishwa kwa alama za kifonetiki zifuatazo: [ aː ɛː ɪː ɔː ʊː ].

Jozi Sahili ya xix): [ ˈl ai ]

[ ˈl eo ]

[ ˈl ia ]

[ ˈl oa ]

[ ˈl au ]

Isharasauti [ l ] zinatoana katika kila neno na kuzibakisha isharasauti ambatano [ aɪ, ɛɔ, ɪa, ɔa, aʊ ] ambazo hazikutoana na zinakubalika kuwa ni fonimu irabu ambatano za Kiswahili sanifu.

**Tanbihi**

Irabu refu, kimaandishi ya kiotografia zinabainika kuwa ni mbili lakini kimatamshi ni irabu moja tu ambazo hutamkwa kwa muda mrefu zaidi kuliko zinavyotamkwa irabu fupi. Hii ndio sababu ya kuitwa irabu refu yaani, kimatamshi na sio kimaandishi. Pia irabu fiche imeitwa hivyo kwa kuwa imefichika yaani, inadhihiri kimatamshi lakini haidhihirishwa kimaandishi kama zilivyodhihiri kimatamshi na kimaandishi irabu fupi [ a, ɛ, ɪ, ɔ, ʊ ].

Uchunguzi unaonesha kuwa, irabu fupi hutamkwa kwa mwangi wa alifu au mwangi wa hamza yaani, irabu ikitokea mwanzo wa neno hutamkwa tofauti na inapotokea kati au mwisho wa neno. Irabu zikisimama mwanzo wa neno kama: [ **a**ti, **e**ti, **i**ta, **o**ta, **u**ti ] basi irabu [ a, e, i, o, u ] zilizotokea mwanzo mwa maneno hayo zinatoa sauti kali yaani hamza. Irabu hizohizo zikifuatia baada ya konsonanti au irabu nyenzao, hutamkwa kwa sauti laini ya muachilio yaani alifu ya uyeyusho (Nchimbi, 1996).

Hali hii imesababishwa na athari ya lugha ya Kiarabu ndani ya lugha ya Kiswahili yaani, irabu ikitokea mwanzo wa neno na ikafuatiwa na konsonanti au irabu nyingine hutamkwa kwa mwangi wa irabu ya hamza. Mfano: [ **A**li, **A**sha, **a**hsante, **a**hlan, **a**mbari, **a**u, **E**she,

**e**nda, **e**ka, **e**mbe, **e**lekea, **I**ssa, **i**nda, **i**ba, **i**la, **i**tika, **o**gopa, **O**thman, **o**mbwe, **u**mbo, **o**sha, **U**ssi, **u**staadh, **u**dhia, **u**laji, **u**nga ] lakini irabu ikitokea baada ya irabu nyingine hutamkwa kwa toni moja ya irabu ya alifu kutokana na muambatano wa irabu mbili zenye sifa bainifu tofauti (*diphthong*). Mfano: [ k**ua**, ak**ae**, n**ai**, p**ao,** l**au,** anguk**ia**, mchuk**ue**, h**io,** kw**ao,** sah**au** ].

Kila irabu ina utamkwaji wake ambao ni tofauti na utamkwaji wa irabu nyingine. Kuna tofauti kati ya irabu refu yaani irabu zinazovutwa kama [ a:, e:, i:, o:, u: ] na irabu fupi yaani irabu zisizovutwa kama [ a, e, i, o, u, ø ]. Suala la irabu tano tu kwa lugha kama ya Kiswahili ni kuonesha kutofanywa kwa utafiti wa ndani kwani baadhi ya lugha za kimataifa zina irabu nyingi zikijumuika na zile irabu fupi, irabu refu, irabu fiche na irabu ambatano kama [ ao, au, ea, ei, ie, ia, oa, ou, ua, uo ].

Irabu ambatano ni maarufu katika lugha za kimataifa kama Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Kwa mujibu wa Collins & Mees, (2008:213-22, lugha hizi zina irabu zaidi ya tano zikizijumuisha na hizo irabu ambatano ambazo Waingereza wao wameziita kwa jina la *diphthong***.** Hata Kiswahili nacho kinabainika kuwa na irabu ambatano katika maneno kama: amtak**ae,** haf**ai,** mwenz**ao,** dhar**au,** pot**ea,** hal**ei,** l**eo,** sik**ia,** mtil**ie,** sik**io,** k**iu,** ok**oa,** mt**oe,** h**oi,** ma**ua,** mchuk**ue,** hak**ui** na h**uo** lakini suala hili bado lina mjadala na linahitaji uchunguzi zaidi wa kisayansi. Uchunguzi unaonesha kuwa, irabu hizo kimaandishi ya kiotografia ni mbili lakini kimatamshi ya kifonetiki ni mwangi mmoja unaochangana kiimbo cha irabu zote mbili. Kutokana na mfumo huo wa utamkaji wa irabu ambatano hizo, utafiti huu unakubaliana na lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kireno kwamba, lugha ya Kiswahili nayo inazo irabu ambatano.

#### 4.2.4.1 Matokeo ya Matumizi ya Kanuni ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili

Kutokana na uchanganuzi wa fonimu kwa kutumia kanuni ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili za maneno ya Kiswahili sanifu, tumepata idadi ya fonimu 47 za msingi zilizogawika kiasili katika makundi mawili makuu ambayo ni:

Kundi la kwanza kuna fonimu konsonanti hafifu: / p, $p^h$, t, $t^h$, k, $k^h$, ʧ, $ʧ^h$, f, ɦ, θ, s, ʃ, x, h / na kundi la pili ni fonimu konsonanti ghuna: / b, ð, d, g, ɟ, ɓ, ɗ, ʛ, ή, l, m, n, ɱ, ɲ, ŋ, ɣ, r, v, z, j, w ] na kundi la tatu la fonimu irabu ghuna: / a, ɛ, ɪ, ɔ, ʊ, ø, a:, ɛ: ɪ:, ɔ:, ʊ: / ambapo jumla ya fonimu hizi zimegawika tena katika makundi yafuatayo:

i) Fonimu za konsonanti **vipasuo**: / p, $p^h$, b, t, $t^h$, d, k, $k^h$, g /.

ii) Fonimu za konsonanti **vikwamizi** ambazo ni / f, ɦ, v, θ, ð, s, z, ʃ, X, ɣ, h /.

iii) Fonimu za konsonanti **vipasuo-kwamizi:** / $ʧ^h$, $ʧ^h$, ɟ /.

Fonimu za konsonanti **ving'ong'o:** / m, n, ɱ, ɓ, ɗ, ŋ, ή, ɲ, ʛ/.

v) Fonimu za konsonanti **kitambaza:** / l /.

vi) Fonimu za konsonanti **kimadende:** / r /.

vii) Fonimu za konsonanti **viyeyusho:** / w, j /.

viii) Fonimu za **irabu fupi:** / a, ɛ, ɪ, ɔ, ʊ, ø /.

ix) Fonimu za **irabu refu:** / a: ɛ: ɪ: ɔ: ʊ: /.

x) Fonimu za irabu ambatano / aɪ, ɛɔ, ɪa, ɔa, aʊ /.

Fonimu konsonanti zote hizo zinaweza kuwekwa katika jedwali na fonimu irabu zote hizo zinaweza kuwekwa katika mchoro kama ifuatavyo:

**Jedwali Nam. 4.4: Fonimu Konsonanti za Kiswahili sanifu**

| Makundi ya Fonimu | Mwahali mwa Kutamkia | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Midomo | Mdomo - Meno | Meno - Ulimi | Ufizi - Ulimi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | Glota |
| **Vipasuo** | p $p^h$ b | | | t $t^h$ d | | k $k^h$ g | |
| **Vikwamizi** | | f ﬁ v | θ ð | s z | ʃ | x ɣ | h |
| **Vipasuokwamizi** | | | | | ʧ $ʧ^h$ ɟ | | |
| **Ving'ong'o** | m ɓ | ɱ | | n ɗ | ɲ ή | ŋ ɠ | |
| **Vitambaza** | | | | l | | | |
| **Vimadende** | | | | r | | | |
| **Viyeyusho** | w | | | | j | | |

**Chanzo: Data za Utafiti, 2020**

Katika jedwali hapo juu, tunabaini kuwa jumla ya fonimu konsonanti zilizopatikana kutokana na uchanganuzi wa kanuni ya kisayansi ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili ya maneno ya Kiswahili. Jedwali pia linabainisha aina za fonimu kama: vipasuo na vipasuo kwamizi zina sauti hafifu na ghuna na fonimu konsonanti za ving'ong'o, vitambaza, vimadende na viyeyusho zote hizo zina sauti ghuna. Aidha jedwali linabainisha fonimu konsonanti na mwahali mwao mwa kutamkiwa kulingana na makundi yao yanayohusika. Kuna fonimu zilizowekewa kipawa cha **[ $^h$ ]** ni fonimu za mpumuo na fonimu zisizo na kipawa cha **[ $^h$ ]** ni fonimu za bila ya mpumuo. Fonimu g'ong'o nazo ziko za aina mbili

yaani, fonimu ng’ong’o sahili yaani, asilia kama / **m** / na / **n** / ambazo ndizo zinazosababisha kutokea kwa irabu fiche yaani, / **-’** / na fonimu ng’ong’o ambatano ambazo ni / ꞵ, ɖ, ɠ, ή, ɲ, ŋ, ɱ /.

Kuhusu fonimu irabu, nazo ziko katika makundi mawili ya fonimu irabu fupi wazi / a, ɛ, ɪ, ɔ, ʊ, -’ / na fonimu irabu refu wazi / a:, ɛ:, ɪ:, ɔ:, ʊ: / kama zinavyobainika katika mchoro ufuatao:




**Mchoro Nam. 4.1: Fonimu Irabu za Kiswahili Sanifu**

**Chanzo: Data za Utafiti, 2020**

Katika mchoro wa hapo juu tunabaini jumla ya fonimu irabu wazi 10 na sehemu zao za kutamkiwa kulingana na ama mbele au nyuma ya ulimi (juu au nusu juu au kati au nusu chini au chini). Jedwali Nam. 4.3 na Mchoro Nam. 4.1 hapo juu, ni kuonesha fonimu za

Kiswahili sanifu katika makundi yake na mwahali mwao mwa kutamkiwa kwa mujibu wa sifa bainifu zao. Fonimu hizo zimejumuisha konsonanti na irabu ambazo nazo zimegawika katika makundi matano ya fonimu za konsonanti sahili, fonimu za konsonanti ambatano, fonimu za konsonanti mpumuo, fonimu za irabu fupi na fonimu za irabu refu. Jumla ya fonimu hizo ndizo zinazotumika kuunda maneno yanayotumika katika mazungumzo na maandishi ya Kiswahili sanifu ambacho asili yake ni lahaja ya Kiunguja Mjini. Kauli hii inaungwa mkono na Nchimbi (1996:25) alipohoji kwamba uthibitisho wa asili ya fonnimu hizo zinatokana na matumizi yake na wasemaji wenye asili ya Kiswahili katika kutofautisha maneno. Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili ya Jakobson, (1978) na kwa mujibu wa nadharia ya fonolojia iliyojadiliwa na Wanaskuli wa Prague ikiongozwa na Turbetzkoy pamoja na Jakobson imedaiwa kwamba, fonimu ni kipashio cha chini kabisa cha lugha chenye uwezo wa kubadilisha umbo na maana katika neno la lugha.

Hoja hiyo ya Nchimbi haina doa wala toa bali ni sahihi na inatuthibitishia kuwa, Waswahili wazalia ndio wenye kutamka idadi maalumu na sahihi ya fonimu za lugha ya Kiswahili zinazotokana na lahaja iliyosanifiwa ya Kiunguja Mjini. Fonimu hizo zina haja ya kuchunguzwa, kubainika na kukubalika na wazawa na wataalamu pamoja na wasomi wa fonolojia ya Kiswahili sanifu.

Matokeo haya ya kuchunguza fomimu za Kiswahili sanifu yanathibitisha kuwa, kila lugha ina idadi mahsusi ya fonimu zake yaani, fonimu zikijumuisha konsonanti na irabu ambazo ndizo msingi wa lugha.  Fonimu hizo ndizo zinazounda maneno na maneno huunda tungo na hatimaye tungo huunda sentensi kama ilivyokwishaelezwa hapo awali. Ukweli huu pia unaungwa mkono na Foley na Thomson (2003:4) waliposema kwamba, lugha huunda jumla ya sauti mojamoja zinazoitwa fonimu. Kila lugha ina mfumo wa kilughawiya wa

kuunda kikundi cha fonimu zake za kipekee. Mfumo wa fonimu hizo, hutofautiana kutoka lugha moja hadi lugha nyingine. (TAKIKI). Foley na Thompson wanasisitiza kuwa kila lugha ikiwemo lugha ya Kiswahili ina idadi mahsusi ya fonimu zake na upekee wa mpangilio wa fonimu hizo katika kuunda maneno ya lugha yake ambao ni tofauti na fonimu za lugha nyingine yoyote.

**Tanbihi**

Jambo la kuzingatia hapa ni kwamba, uchanganuzi kuhusu fonimu hapo juu, hauna dhamira ya kuonesha idadi ya fonimu za Kiswahili sanifu, bali ni kuthibitisha kuwa Kanuni ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili ina uwezo wa kuwasilisha idadi ya fonimu za Kiswahili sanifu. Suala la idadi kamili ya Fonimu za Kiswahili sanifu na viashiria vyake linahitaji mikakati maalumu kama utafiti huu utakavyopendekeza katika sura ya sita ya tasnifu hii.

Hali hii ya kuwepo kwa kutofautiana katika fonolojia ya Kiswahili sanifu na kuweza kufanyiwa masahihisho inathibitishwa na kutolewa muongozo na Simala (2004:39) aliposema kwamba, wazalendo wa lugha ya Kiswahili sanifu yaani, wazawa wanadai kuwa matatizo yanayoikumba lugha hii ni lazima kutazamwa na kueleweka kuwa ni masuala ya kijamii. Hivyo basi, pana haja ya dharura kuhakikisha kuwa, Kiswahili sanifu kinapewa hadhi yake katika jukwaa la lugha za Kiafrika na zile za ulimwengu.

Katika maelezo hayo, Simala anasisitiza kuwa, Kiswahili sanifu ni chombo cha jamii basi hakikosi kuwa na matatizo. Lakini kila yanapogundulikana matatizo basi, yasiachiwe ila yahakikishwe kuwa, yanachunguzwa na yanafanyiwa masahihisho yake, ili Kiswahili sanifu kiendelee kuwa na hadhi ya kitaifa na kimataifa. Sasa kinachojitokeza kwa wengi

wa wasemaji au wazungumzaji wa Kiswahili sanifu ni kutokuwa weledi na mahiri wa taaluma za sarufi, lughawiya na utamaduni wa Kiswahili katika mazingira ya Waswahili wazawa wenyewe. Ukilinganisha kwa mfano kati ya watu wenye asili ya pwanipwani mwa upwa wa Afrika Mashariki na wale walio nnje ya Upwa wa Afrika Mashariki, utagundua kwamba wale wa nnje ya Afrika Mashariki wengi wao, Kiswahili ni lugha yao ama ya pili au ya kigeni. Lakini hao wa pwanpwani wengi wao Kiswahili ni lugha yao mama yaani, lugha yao ya uzawa. Hivyo, inakadiriwa kuwa, wengi wa wanaozua kutofautiana katika matamshi ya baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu kati ya makundi haya mawili, wanazua kwa kutoielewa vyema lugha hii. Lakini kwa kuwa wamo katika mawasiliano, basi kwao wao, kuzua tofauti za aina hiyo sio tatizo, almuradi tu matamshi au maandishi yao yanafahamika basi kwao wao ni sawa tu. Uzoefu unaonesha kuwa, wazungumzaji wanaotoka nje ya Upwa wa Afrika Mashariki wana Kiswahili sanifu tu wakati wale wasemaji wenye asili ya Afrika Mashariki, wana Kiswahili sanifu na fasaha. Maneno haya yanathibitishwa na Mhina, (1970:55) alipokiri kwa kusema kwamba, mwandishi: Sheikh Muhammed Saleh Farsy ambaye ni Muunguja mwenye ujuzi mkubwa wa lugha hii, wote twasadiki kuwa Unguja ndiko kwenye makao makuu ya Kiswahili safi kitumiwacho na wengi hapa Afrika Mashariki. Usafi wa Kiswahili hicho twaweza kuuona jinsi unavyojitokeza katika maandishi ya mtaalamu huyu.

Mhina hapa anatuhakikishia kuwa watu wa Unguja ndio wenye kusema Kiswahili safi yaani fasaha. Ushahidi unatokana na yeye mwenyewe pia ameteleza kwa pale aliposema *wote twasadiki*. Tungo hii ilipaswa iwe *sote twasadiki* ndio sahihi na fasaha kwa wenyewe wazawa wa Kiswahili.

### 4.2.5 Uchunguzi wa Zaida wa Utafiti kuhusu Aina za Fonimu za Kiswahili sanifu

#### a) Fonimu Silabi Funge $ m $ na $ n $

Kimsingi, silabi ni isharasauti zinazotamkwa kwa mwangi mmoja wa sauti wa ama konsonanti na irabu au konsonanti pekee au irabu pekee. Isharasauti [ m, n, b, f ] huwa ni silabi funge kwa kufuatiwa na irabu fiche katika maneno kama **m**tu, **m**zigo, ali**m**sema, **m**buni, **n**ke, **n**ta, **n**cha ka**b**la, la**b**da ha**f**la, gha**f**la. Katika maneno hayo isharasauti [ **m, n, b, f ]** zinatoa mwangi wa sauti ya pekee na kupata jina la silabi funge zenye irabu fiche. Kwa ufafanuzi huo wa dhana ya silabi funge inadhihirika kuwa, hakuna isharasauti pekee inayoweza kutamkika bila ya sauti hiyo kuwa ni silabi funge inayofuatiwa na irabu fiche (Polome, 1967).

Akina Benard (2000:56), Khamis (2011:24) na Nchimbi (2008:41) wao wameibainisha isharasauti silabi **$ m $** na **$ n $** kuwa ni fonimu katika maneno kama:

| **Matamshi** | **Maandishi** | **Fonimu Silabi** |
|---|---|---|
| m’ba | mba | m’ |
| m’baazi (mti) | mbaazi | m’ |
| m’buni | mbuni | m’ |
| m’bono (mti) | mbono | m’ |
| m’buyu | mbuyu | m’ |
| m’boga (mmea) | mboga | m’ |
| n’zuri | nzuri | n’ |
| n’ zio | nzio | n’ |
| n’cha | ncha | n’ |
| n’zi | nzi | n’ |
| n’ke | nke | n’ |
| kab’la | kabla | b’ |

| | | |
|---|---|---|
| lab’da | labda | b’ |
| haf’la | hafla | f’ |
| ghaf’la | ghafla | f’ |

Isharasauti **[ m, n, b, f ]** katika maneno hayo ni fonimu konsonanti silabi funge za Kiswahili sanifu. Fonimu **/ m /, / n /, / b /** na **/ f /** zinahitaji kupambanuliwa kwa kutamkwa kwa sauti au toni ya pekee bila ya kuunganishwa na konsonanti **[ b, n, z, ch, k, l, d, l ]** zinazozifuatia. Hali hii inachangia kutofautiana kwa uwakilishwaji wa maandishi sahihi ya isharasauti kutokana na matamshi yake fasaha. Ni vyema kwa maneno hayo silabi funge ya $ m $ na $ n $ zikbainishwa kimaandishi kwa kuwekewa alama ya koma juu ( **’** ) ili kutofautisha kati ya maneno kama mbaazi (mti) na mbaazi (nafaka), mboga (mmea) na mboga (majaini).

**Tanbihi:**

Kutokana na isharasauti **[ m ]** na **[ n ]** kuwa ni fonimu konsonanti za silabi funge, silabi funge hizi hufuatiwa na irabu fiche ambayo inadhihiri kimatamshi lakini haidhihiri kimaandishi. Irabu kama hii inapatikana katika lugha ya Kiarabu na inadhihiri kimatamshi na kimaandishi kwa kiashiria cha **[ ᵔ ]** au **[ o ]**. Katika mkabala huu inabainika kuwa hata lugha ya Kiswahili nayo ina irabu hiyo ambayo inadhihirishwa kimatamshi lakini haidhihirishwi kimaandishi. Irabu fiche katika Kiswahili hutokea katika maneno kama **m**kate, **n**ta, **m**ba, **n**zi, **n**nje, **n**zio, **m**zo**,** **m**moja na **nk**e. Kwa uthibitisho huu, ni dhahiri kwamba, irabu fupi za Kiswahili kimatamshi na kimaandishi ni sita badala ya tano ambazo zinawakilishwa kwa viashiria vya kiotografia vya [ a, e, i, o, u, − ] na viashiria vya kifonetiki vya [ a, ε, ɪ, ɔ, ʊ, ø ].

**b) Kutozibainisha Kimaandishi Fonimu Funge /m/ na / n / katika Maneno ya Kiswahili sanifu**

Uchunguzi unaonesha matatizo ya kuzidondosha baadhi ya fonimu kimaandishi kutokana na matamshi yake sahihi na kusababisha kutofautiana kati ya matamshi na maandishi ya maneno. Mfano wa kuzidondosha fonimu silabi ni kama ifuatavyo:

| **Matamshi** | **Maandishi** | **Kutozibainisha Kimaandishi** |
|---|---|---|
| mmbu | mbu | m |
| mmbwa | mbwa | m |
| nnje | nje | n |
| nnjoo | njoo | n |
| nnge | nge | n |
| nngwe | ngwe | n |

Uchunguzi unaonesha kwamba, matatizo ya matamshi na maandishi ya fonimu hizo yamesababishwa na usanifishaji wa Kiswahili ulipofanywa na Wazungu tangu mwaka 1930. Pamoja na hilo pia uchunguzi unabaini kuwa makosa kama hayo hufanywa na wazungumzaji wasio wazawa wa Kiswahili ama kwa kutofahamu au kwa kudharau au kwa wigo tu (Khamisi, 2005, Mhina, 1970 na Ager, 2014).

**c) Irabu fupi na Irabu Refu katika Kiswahili sanifu**

Irabu refu kimaandishi ya kiotografia zinabainika kuwa ni mbili lakini kimatamshi ni irabu moja tu ambazo hutamkwa kwa muda mrefu zaidi kuliko zinavyotamkwa zile irabu fupi.

Hii ndiyo sababu ya kuitwa irabu refu yaani, kimatamshi na sio kimaandishi. Pia irabu fiche imeitwa hivyo kwa kuwa imefichika haikudhahiri kama zilivyo irabu fupi nyengine.

Uchunguzi unaonesha kuwa, irabu fupi hutamkwa kwa mwangi wa alifu au mwangi wa hamza yaani, irabu ikitokea mwanzo wa neno hutamkwa tofauti na inapotokea kati au mwisho wa neno. Irabu zikisimama mwanzo wa neno kama: **[** ***a****ti,* ***e****ti,* ***i****ta,* ***o****ta,* ***u****ti* **].** Irabu **[ a, e, i, o, u ]** zilizotokea mwanzo mwa maneno hayo zinatoa sauti kali yaani hamza. Irabu hizohizo zikifuatia baada ya konsonanti au irabu nyenzao, hutamkwa kwa sauti laini ya muachilio yaani alifu ya uyeyusho (Nchimbi, (1996).

Hali hii imesababishwa na athari ya lugha ya Kiarabu ndani ya lugha ya Kiswahili yaani, irabu ikitokea mwanzo wa neno na ikafuatiwa na konsonanti au irabu nyenginehutamkwa kwa mwangi wa irabu ya hamza. Mfano: [ **A**li, **A**sha, **a**hsante, **a**hlan, **a**mbari, **a**u, **E**she, **e**nda, **e**ka, **e**mbe, **e**lekea, **I**ssa, **i**nda, **i**ba, **i**la, **i**tika, **o**gopa, Othman, **o**mbwe, **u**mbo, **o**sha, **U**ssi, **u**staadh, **u**dhia, **u**laji, **u**nga] lakini irabu ikitokea baada ya konsonanti hutamkwa kwa irabu ya alifu. Mfano: [ ak**ae**, na**i**, pa**o,** a**u,** anguk**ia**, mchuk**ue**, h**oi,** t**oa,** kw**ao,** sah**au,** p**ua,** mpand**ie,** suk**uo,** t**ui** ].

Kila irabu ina utamkwaji wake ambao ni tofauti na utamkwaji wa irabu nyingine. Kuna tofauti kati ya irabu refu yaani irabu zinazovutwa kama [ a:, e:, i:, o:, u: ] na irabu fupi yaani irabu zisizovutwa kama [ a, e, i, o, u, ø ]. Suala la irabu tano tu kwa lugha kama ya Kiswahili ni kuonesha kutofanywa kwa utafiti wa ndani kwani baadhi ya lugha za Kimataifa zina irabu nyingi zikijumuika na zile irabu refu, irabu fiche na irabu ambatano kama [ ao, au, ea, ei, ie, ia, oa, ou, ui, uo ].

Irabu ambatano ni maarufu katika lugha za kimataifa kama Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Kwa mujibu wa Collins & Mees, (2008:213-22, lugha hizi zina irabu zaidi ya tano zikijumuishwa na hizo irabu ambatano ambazo Waingereza wao wanaziita *diphthong***.** Hata Kiswahili nacho kinabainika kuwa na irabu ambatano katika maneno kama: amtak**ae,** haf**ai,** mwenz**ao,** dhar**au,** pot**ea,** hal**ei,** l**eo,** sik**ia,** mtil**ie,** sik**io,** k**iu,** ok**oa,** mt**oe,** h**oi,** ma**ua,** mchuk**ue,** p**ua,** hak**ui** na h**uo.** Uchunguzi unaonesha kuwa, irabu hizo kimaandishi ya kiotografia ni mbili lakini kimatamshi ya kifonetiki ni mwangi mmoja unaochangana kiimbo cha irabu zote mbili. Kutokana na mfumo huo wa utamkaji wa irabu ambatano hizo, Utafiti huu unakubaliana na lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kireno kwamba na lugha ya Kiswahili nayo inazo irabu ambatano kama [ ae, ai, ao, au, ea, ei, eo, ia, ie, io, iu, oa, oe, oi, ua, ui, uo ].

**d) Upungufu katika Utamkaji wa Fonimu za Kiswahili Sanifu**

Ukiachilia mbali kutofautiana katika idadi ya fonimu na viashiria vyake, utafiti huu pia umebaini upungufu wa utamkaji wa fonimu kwa baadhi ya wataalamu katika maneno ya Kiswahili sanifu. Suala hili la upungufu wa utamkaji wa fonimu katika maneno ya Kiswahili sanifu limejadiliwa na Kihore na wenzake, (2004) kwamba, Kiswahili kina baadhi ya maneno yanayotamkwa kinyume na idadi ya fonimu zake. Lakini akina Mgullu (2001:79) na Khamis (2011: xiv-xv) wao wanahoji kuwa, Waswahili wazalia wenyewe huyatamka maneno ya Kiswahili sawasawa kulingana na idadi ya fonimu zake katika neno yaani, umbo la neno ndio msingi wa utamkaji wa fonimu zake (Ligami, 2002:136, Chomsky & Halle, 1968). Kwa mnasaba huu, suala la makossa katika utamkaji wa fonimu za neno ni jambo linalohitaji kutanabahishwa katika Kiswahili sanifu. Hii ni kwa sababu jukumu kuu la lugha sanifu yoyote ile ni kujaribu kuondoa tofauti za utamkaji kwa

kuwafanya wasemaji au wazungumzaji wake wawe na njia moja ya utamkaji wa maneno ya lugha hiyo kwa usahihi kulingana na idadi mahsusi ya fonimu za lugha hiyo.

Mifano ya kutofautiana katika matamshi au maandishi ya fonimu katika maneno ya Kiswahili sanifu ni kama ifuatavyo:

| **Matamshi au Maandishi Pungufu** | **Matamshi au Maandishi Sahihi** |
|---|---|
| Mmo**m**onyoko | Mmo**ng'**onyoko, |
| Mu**m**unya | Mu**ng'**unya |
| **M**kanda | **U**kanda |
| M**z**iramu | M**l**izamu au m**r**izamu |
| m**l**o**l**ongo | M**d**o**r**ongo, |
| **Li**ngine au **le**ngine | **J**ingine au **je**ngine |
| Let**a** | Let**e** |
| Ma**kh**aribi au ma**h**aribi | Ma**gh**aribi, |
| H**au**po | H**u**po, |
| H**au**endi | hw**e**ndi |
| H**e**ba | H**ai**ba |
| Mwana**u**me | Mwana**m**me |
| **Hairisha** au **gh**airisha | A**kh**irisha au **ah**irisha |
| **Kh**afla au **gh**afla (Shughili Fulani) | **H**afla |
| Kiambatanisho | Kiambat**ani**sho |
| Kusta**h**afu | Kusta**a**fu |
| Mak**a**zi | Mak**aa**zi |
| **Mw**uguzi | **M**u**u**guzi |
| M**i**da | M**u**da, |
| **Ma**saa | **S**aa |

| | |
|---|---|
| Mka**r**imani | Mka**l**imani |
| Na**wa**shukuru au na**wa**shukuruni | Na**ku**shukuruni |
| S**into**fahamu | S**uita**fahamu |
| **U**mauti | **M**auti, |
| Ur**o**da | Ur**e**da |
| **V**ema | **Vy**ema, |
| **A**fisi **U**tofauti | **O**fisi na Tofauti |

### 4.2.6 Swali la 3 la Hojaji: Athari za Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na Viashiria Vyake

Katika sehemu hii utafiti ulichanganua na kuwasilisha data kuhusu lengo mahsusi la pili la utafiti huu. Lengo hilo lilitaka kudhihirisha athari za kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Ili kufikia lengo hili mtafiti aliunda swali mahsusi la 2 katika utafiti huu lililouliza, Kuna athari gani za kutofautiana kwa wataalamu katika idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu? Data zilizotumika kujibu swali hilo, zilikusanywa kwa kutumia usaili wa Hojaji na Mahojiano (Kiambatanisho cha 2 na Kiambatanisho cha 3).

Majibu yaliyotolewa na Wasailiwa katika kulijibu swali hilo kuhusu athari wa kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake kwa wanafunzi na wahadhiri wa fonolojia ya Kiswahili sanifu yalikuwa kama ifuatavyo:




| | Athari ya 1 | Athari ya 2 | Athari ya 3 | Athari ya 4 | Athari ya 5 | Athari ya 6 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanafunzi wa Mwk. 3 | 16 | 3 | 0 | 0 | 3 | 18 | 40 |
| Wanafunzi wa Umahiri | 15 | 1 | 0 | 0 | 3 | 1 | 20 |
| Wahadhiri wa Kiswahili | 20 | 5 | 4 | 6 | 4 | 1 | 40 |
| Jumla | 51 | 9 | 4 | 6 | 10 | 20 | 100 |



**Chanzo: Data za Wasailiwa, 2020**

**Grafu Nam. 4.5: Majibu ya Wasailiwa wa Hojaji kuhusu Athari za Kutofautiana Idadi ya Fonimu na Viashiria vyake**

Athari ya 1: Kuzusha mkanganyiko na ubabaifu wa kutoifahamu ni ipi idadi sahihi kati ya 27, 28, 29, 30, 31, 32, 33, 34, 35, 36, 37, 38, 40, 41, 42, 45, 58.

Athari ya 2: Kujenga migongano na mizozo baina ya wataalamu katika taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake.

Athari ya 3: Kuonesha mbaguano wa wataalamu kwa kutokuwa na idadi linganifu ya fonimu na viashiria vyake.

Athari ya 4: Kiswahili sanifu kukosa idadi sahihi ya fonimu na viashiria vyake.

Athari ya 5: Kuibua mikabala mingi na kila mmoja kujiona yuko sahihi katika taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake.

Athari ya 6: Kuwavunja moyo wanafunzi kuchagua somo la lughawiya kwa kutokana na kutokubaliana kwa wataalamu wake.

Grafu linabainisha namna Wasailiwa walivyoibua aina sita za athari za kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Athari hizo pia nazo zinakubalika kuwa ndizo zinaowakabili wanafunzi, wahadhiri na wasomi wa fonolojia ya Kiswahili sanifu, hususan katika taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake. Athari ya kuzusha mkanganyiko na ubabaifu wa kutoifahamu ni ipi idadi sahihi kati ya 27, 28, 29, 30, 31, 32, 33, 34, 35, 36, 37, 38, 40, 41, 42, 45, 58 imeonekana na Wasailiwa wengi kuliko athari nyengine yaani, Wasailiwa 51 sawa na asilimia (51%). Athari ya kuwavunja moyo wanafunzi kuchagua somo la Kiswahili-lughawiya kutokana na kutokubaliana kwa wataalamu wake imeelezwa na Wasailiwa 20 sawa na asilimia (20%). Athari nne zilizobaki zimebainishwa kwa kiwango cha chini ya jumla ya Wasailiwa yaani chini ya 10. Utafiti huu unakubaliana na athari zote hizo kuwa zinachangia kudhoofisha ustawi wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Zaidi ya athari hizo zilizobainishwa na Wasailiwa, utafiti huu pia umebaini athari nyingine kama:

i) Vyombo vinavyosimamia Kiswahili snafu kama KAKAMA, BAKITA NA BAKIZA kutokaa kufanya kazi yao vyema kwa kutosimamia suala la idadi ya fonimu na viashiria katika Kiswahili sanifu.

ii) Kiswahili kutofautiana na lugha nyingine za kimataifa kama Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania ambazo wataalamu wao wamelingana sana katika ubainishhaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika lugha zao.

iii) Viashiria vya fonimu kutokuwa mahsusi kwa kila fonimu moja na badala yake kila muandishi kuamua kutumia viashiria vyake kinyume na lugha maarufu za kimataifa kama Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania ambazo pia wataalamu wao wote wamelingana vyema tu.

#### 4.2.6.1 Swali la 3 la Mahojiano: Athari za Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na Viashiria Vyake

Swali hili pia waliulzwa wasailiwa wa Mahojiano na jawabu zao zilikuwa kama zinavyobainika katika grafu lifuatalo:




| | Athari ya 1 | Athari ya 2 | Athari ya 3 | Athari ya 4 | Athari ya 5 | Athari ya 6 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wasailiwa wa Kiingereza | 3 | 2 | 3 | 3 | 0 | 2 |
| Wasailiwa wa Kifaransa | 3 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Wasailiwa wa Kireno | 3 | 2 | 2 | 1 | 3 | 3 |
| Wasailiwa wa Kiarabu | 3 | 3 | 3 | 3 | 0 | 0 |
| Wasailiwa wa Kihispania | 2 | 2 | 3 | 2 | 0 | 0 |
| Jumla | 12 | 11 | 10 | 13 | 3 | 2 |

**Chanzo: Data za Wasailiwa, 2020**

**Grafu Nam. 4.6: Majibu ya Wasailiwa wa Mahojiano kuhusu Athari za Kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake**

Athari ya 1: Wataalamu kuibua mikabala mingi na kila mmoja kujiona yuko sahihi katika taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake.

Athari ya 2: Kiswahili sanifu kukosa idadi sahihi ya fonimu na viashiria vyake.

Athari ya 3: Wanafunzi wa umahiri na uzamivu kulikwepa somo la Lughawiya kwa kukosa udhibiti na kukimbilia somo la Fasihi.

Athari ya 4: Kuzusha ubabaifu na kuchanganyikiwa katika kutoifahamu ni ipi idadi sahihi kati ya 27, 28, 29, 30, 31, 32, 33, 34, 35, 36, 37, 38, 40, 41, 42, 45, 58.

Athari ya 5: Kudharaulika kwa Kiswahili kwa kukosa msimamo mmoja wa idadi ya fonimu na viashiria vyake.

Athari ya 6: Kiswahili sanifu kukosa mkabala mmoja wa idadi halisi ya fonimu na viashiria vyake.

Grafu linaonesha athari sita ziliobainishwa kwa jumla na Wasailiwa wa lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania. Athari ya Kuzusha ubabaifu na mkanganyiko wa kutoifahamu ni ipi idadi sahihi kati ya 27, 28, 29, 30, 31, 32, 33, 34, 35, 36, 37, 38, 40, 41, 42, 45, 58 imekubaliwa na Wasailiwa 13 sawa na asiimia (87%). Athari ya Wataalamu kuibua mikabala mingi na kila mmoja kujiona yuko sahihi katika taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake imebainishaji Wasailiwa 12 sawa na asiimia 80%. Sababu ya Kuwepo kwa vyombo vingi vya kusimamia Kiswahili sanifu kama KAKAMA, BAKITA, BAKIZA badala ya chombo kimoja tu imeoneshwa na Wasailiwa 11 sawa na asilimia (73%) na sababu ya Kiswahili sanifu kutokuwa na jopo moja la wataalamu lenye msimamo mmoja wa kuyapitia maandishi ya wataalamu imeoneshwa na Wasailiwa 10 sawa na asilimia (67%). Athari hizo zinkifanya Kiswahili sanifu kudharaulika mbele ya lugha sanifu za kimataifa kama Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania kwa Kiswahili kwa kukosa msimamo mmoja wa idadi ya fonimu na viashiria vyake.

Pamoja na hali hiyo, athari zote hizo zilizotolewa na Wasailiwa wa Hojaji na Mahojiano ufatiti huu unazinakubalika katika na zinafikiriwa pengine ndizo zilizosababisha kutofautiana kwa wataalamu katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu

Kutokana na wa uchanganuzi huo wa sababu na athari za kutofautiana kwa wataalamu katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu, utafiti huu umeweza kuibua matatizo sasa tuangalie mapendekezo ya kurekebisha matatizo hayo kwa majibu ya swali la nne kutoka kwa Wasailiwa wa Hojaji na Mahojiano.

### 4.2.7 Swali la 4 la Hojaji Kuhusu Mapendekezo ya Nini Kifanyike ili Kurekebisha Tatizo la Kuhitalifiana

Wasailiwawa 15 wa lugha za lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania walitakiwa watoe mapendekezo yao kuhusu nini kifanyike ili kupunguza au kuondoa sababu na athari ya kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Majibu ya Wasailiwa hao ni kama yafuatayo:




| | Pendekezo la 1 | Pendekezo la 2 | Pendekezo la 3 | Pendekezo la 4 | Pendekezo la 5 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanafunzi wa Mwk.3 | 10 | 20 | 0 | 5 | 5 | 40 |
| Wanafunzi wa Umahiri | 2 | 10 | 8 | 0 | 0 | 20 |
| Wahadhiri wa Kiswahili | 13 | 15 | 7 | 5 | 0 | 40 |
| Jumla | 25 | 45 | 15 | 10 | 5 | 100 |

**Chanzo: Data za Wasailiwa, 2020**

**Grafu Nam. 4.7: Mapendekezo ya Wasailiwa wa Hojaji kuhusu Nini Kifanyike ili Kurekebisha Tatizo la Kutofautiana kwa Idadi ya Fonimu na viashiria vyake**

Pendekezo la 1: Ufanyike utafiti wa kina kwa kutumia vigezo vya kisayansi ili kupata idadi halisi ya fonimu za Kiswahili sanifu.

Pendekezo la 2: Wataalamu watumie kanuni ya kisayansi katika fonolojia ya Kiswahili katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake.

Pendekezo la 3: Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA) iandae Warsha kwa wataalamu ili wachunguze idadi halisi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

Pendekezo la 4: Itumike nadharia teule ya kisayansi kwa wataalamu wanaobainisha idadi ya fonimu na viashiria vyake.

Pendekezo la 5: Mabaraza ya Kiswahili yaweke udhibiti wa kuyathibitisha maandishi ya taaluma ya fonolojia ya Kiswahili sanifu.

Grafu linabainisha mapendekezo matano yaliyotolewa na Wasailiwa. Pendekezo la Wataalamu watumie kanuni ya kisayansi katika fonolojia ya Kiswahili katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake limependekezwa na Wasailiwa 45 sawa na asilimia (45%). Pendekezo hili limefuatiwa na pendekezo la Ufanyike utafiti wa kina kwa kutumia vigezo vya kisayansi ili kupata idadi halisi ya fonimu za Kiswahili sanifu lililopendekezwa na Wasailiwa 25 sawa na asilimia (25%). Mapendekezo matatu yaliyobaki yamependekezwa na Wasailiwa wachache yaani, asilimia 15%, 10% na 5% kwa kila moja. Kwa mujibu wa utafiti huu, mapendekezo haya yote yanakubalika na kama yatafanyiwa kazi huenda suala la kutofautiana kwa ubainishaji wa idadi ya fonimu na vishiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu likapungua au likaondoka kabisa.

#### 4.2.7.1 Swali la 4 la Mahojiano Kuhusu Mapendekezo ya Nini Kifanyike ili Kurekebisha Tatizo la Kuhitalifiana

Swali hili pia waliulzwa wasailiwa wa Mahojiano na jawabu zao zilikuwa kama zinavyobainika katika grafu lifuatalo:




| | Pendekezo la 1 | Pendekezo la 2 | Pendekezo la 3 | Pendekezo la 4 | Pendekezo la 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Wasailiwa wa Kiingereza | 3 | 2 | 3 | 3 | 2 |
| Wasailiwa wa Kifaransa | 2 | 1 | 2 | 1 | 2 |
| Wasailiwa wa Kiarabu | 3 | 3 | 2 | 2 | 3 |
| Wasailiwa wa Kireno | 3 | 2 | 3 | 2 | 3 |
| Wasailiwa wa Kihispania | 2 | 1 | 2 | 2 | 2 |
| Jumla | 13 | 9 | 12 | 10 | 12 |

Wasailiwa wa Kiingereza, Wasailiwa wa Kifaransa, Wasailiwa wa Kiarabu, Wasailiwa wa Kireno, Wasailiwa wa Kihispania, Jumla

**Chanzo: Data za Wasailiwa, 2020**

**Grafu Nam. 4.8: Mapendekezo ya Wasailiwa wa Mahojiano kuhusu Nini Kifanyike ili Kurekebisha Tatizo la Kutofautiana**

Pendekezo la 1: Kamisheni na mabaraza ya Kiswahili yashirikiane katika kusimamia maandishi ya taaluma za Kiswahili sanifu.

Pendekezo la 2: KAKAMA iandae jopo la wataalamu weledi wakae na kudurusu Sera ya Kiswahili na usanifishaji wake ili kudhibiti idadi moja ya fonimu na viashiria vyake.

Pendekezo la 3: Wataalamu waoneshe nadharia au kanuni iliyowaongoza wanapowasilisha idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

Pendekezo la 4: Utafiti wa idadi ya fonimu na viashiria vyake ufanyike kwa kusikia matamshi ya sauti za wazungumzaji badala ya maandishi ya wataalamu.

Pendekezo la 5: Mabaraza ya Kiswahili yatoe ithibati ya kazi zote zinazoandikwa katika taaluma za lughawiya ya Kiswahili sanifu.

Grafu linabainisha mapendekezo matano yaliyotolewa na Wasailiwa. Mapendekezo matatu yamekubaliwa na Wasailiwa kwa kiwango kikubwa cha Wasailiwa. Mapendekezo hayo ni Kamisheni na mabaraza ya Kiswahili yashirikiane katika kusimamia maandishi ya taaluma za Kiswahili sanifu limekubaliwa na Wasailiwa13 sawa na asilimia (87%). Wataalamu waoneshe nadharia au kanuni iliyowaongoza wanapowasilisha idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu limekubaliwa na Wasailiwa 12 sawa na asilimia (80%). Mabaraza ya Kiswahili yatoe ithibati ya kazi zote zinazoandikwa katika taaluma za lughawiya ya Kiswahili sanifu nalo limekubaliwa na Wasailiwa 12 sawa na asilimia (80%). Mapendekezo mawili yamekubaliwa kwa kiwango cha zaidi ya nusu ya jumla ya Wasailiwa. Pendekezo la KAKAMA iandae jopo la wataalamu weledi wakae na kudurusu sera ya Kiswahili na usanifishaji ili kudhibiti idadi ya moja ya fonimu na

viashiria vyake limekubaliwa na Wasailiwa tisa sawa na asilimia (60%). Pendekezo la Utafiti wa idadi ya fonimu na viashiria vyake ufanyike kwa kusikia matamshi ya sauti za wazungumzaji badala ya maandishi ya wataalamu Wasailiwa10 sawa na asilimia (67%). Kwa matokeo haya utafiti huu unayakubali mapendekezo yote haya kwa kuwa, kila pendekezo moja limekubaliwa na zaidi ya nusu ya Wasailiwa. Pia mapendekezo hayo yana mantiki ya kuondosha tatizo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonnolojia ya Kiswahili sanifu.

### 4.2.8 Kulingana kwa Uwasilishaji na Uchanaganuzi wa Data za Hojaji na Majadiliano

Kutokana na uchanaganuzi wa data za usaili wa Hojaji na usaili wa Majadiliano utafiti huu umebaini kwamba wahojiwa wa Hojaji na Majadiliano kwa maswali 3 yaani, swali la 1, swali la 3 na swali la 4 majibu yao yamelingana sana tafauti ni lugha tu. Lakini wote wamebainika kuwa na mtazamo wa aina moja kuhusu tatizo la wataalamu kutofautiana katika idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Ushahidi wa hayo umeonekana wazwazi katika uchanganuzi na uwasilishaji wa taarifa za utafiti huu.

## 4.3 Hitimisho

Sura hii imechanganua na kujadili na kuwasilisha data za Wasailiwa zilizokusanywa kutoka uwandani, yaani vyuo vikuu vine vya Zanzibar. Uchanganuzi huo ulitumia usaili wa Hojaji (Kiambatanisho cha 2) na usaili wa Mahojiano (Kiambatanisho cha 3). Maswali ya Hojaji na ya Mahojiano yalilenga kujibu malengo matatu ya utafiti huu yaani, kutaka kufahamu sababu, athari na mapendekezo ya suala la wataalamu zaidi ya 35 kutofautiana katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahi

sanifu. Kwa upande wa pili, sura imebainisha mchango wa utafiti kuhusu idadi yay a fonimu za Kiswahili sanifu. Zaidi ya hayo sura imeonesha nini kifanyike ili katika suala la sababu na athari za kutofautiana kwa wataalamu zaidi ya 35 katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake lipungue au liondoke kabisa.

# SURA YA TANO

# MATOKEO, MJADALA NA MCHANGO WA UTAFITI

## 5.1 Utangulizi

Matokeo ya Utafiti huu, yamelenga kutafiti, kukusanya na kuchambua data, kuhakiki na kufafanua sababu na athari za kutofautiana kwa wataalamu zaidi ya 35 katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Matokeo ya utafiti huu yalilenga katika kusaidia kuondoa tatizo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake ili kukiweka Kiswahili sanifu katika mkabala na mustakbali mpya wa idadi halisi ya fonimu na viashiria vyake mahsusi. Hali hii ya kuwepo kwa kutofautiana katika Kiswahili sanifu na kuweza kufanyiwa utafiti ili kutoa masahihisho, inathibitishwa na kutolewa muongozo na Simala (2004:39) alipoelekeza kwamba, wazalendo wa lugha kama Kiswahili sanifu wanadai kuwa matatizo yanayoikumba lugha yao ni lazima kutazamwe na kueleweka kuwa ni masuala ya kijamii. Hivyo basi, pana haja ya dharura kuhakikisha kwamba Kiswahili sanifu kinapewa hadhi yake katika jukwaa la lugha za Kiafrika na zile za ulimwengu.

Katika maelezo hayo, Simala anasisitiza kuwa, Kiswahili sanifu ni chombo cha jamii basi hakikosi matatizo. Lakini kila yanapogundulikana hayo matatizo basi, yasiachiwe ila yahakikishwe kuwa, yanachunguzwa na yanafanyiwa masahihisho yake, ili Kiswahili sanifu kiendelee kuwa na hadhi zaidi katika majukwaa ya kitaifa na kimataifa. Sura hii imelenga kuweka bayana matokeo mjadala na mchango wa yaliyoibuka kutokana na uchanganuzi wa data zilizokusanywa kwa nia ya kuyapatia majibu sahihi malengo mahsusi ya utafiti huu. Katika kipengele cha matokeo, mtafiti amewasilisha na kuyajadili

kwa ufupi matokeo ya utafiti. Kipengele cha mchango wa utafiti kinabainisha mambo mapya ya kitaaluma yaliyoibuliwa na utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu ni kama yafuatavyo:

## 5.2 Matokeo ya Utafiti kwa Jumla

Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kulingana na malengo mahsusi ya utafiti huu kama ifuatavyo:

### 5.2.1 Matokeo ya Lengo Mahsusi la Kwanza

Matokeo ya lengo mahsusi la Kwanza yaliyopatikana kwa majibu ya Wasailiwa katika swali namba 1 la usaili wa Hojaji na swali namba 1 la usaili wa Majadiliano. Swali lilitaka kufahamu ni sababu gani zilizowafanya wataalamu zaidi ya 35 kutofautiana katika idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Utafiti ulibaini jumla ya sababu 14 ambazo zilitolewa na Wasailiwa. Miongoni mwake sababu sita zilibainishwa na Wasailiwa wa usaili wa Hojaji iliyojazwa majibu, sababu tano zilibainishwa na Wasailiwa wa usaili wa Mahojiano na sababu 3 zimewasilishwa na mtafiti. Jumla ya sababu hizo kama inavyobainika hapa chini:

i) Tafauti ya viwango tafauti vya wataalamu katika taaluma ya fonimu katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

ii) Usanifishaji wa Kiswahili kufanywa na wataalamu wageni yaani, Wazungu ambao waliathiriwa na taaluma za lugha zao.

iii) Wataalamu kuwa huru katika maandishi yao bila ya kusimamiwa na jopo moja la wahariri katika taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake.

iv) Wataalamu kutozingatia kanuni ya kisayansi inazowasilisha idadi ya fonimu na viashiria vyake.

v) Wataalamu kuathiriwa na mikabala ya fonimu za lugha nyingine za Kiingereza, Kiarabu na Kibantu.

vi) Tofauti za marejeo waliorejea wataalamu walipowasilisha idadi ya fonimu na viashiria vyake.

vii) Wataalamu kutobainisha kanuni waliotumia katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake.

viii) Wataalamu kutofanya utafiti wa kina kwa wazungumzaji na wajuzi wa Kiswahili sanifu.

ix) Wataalamu kuwa huru kuandika kazi zao bila ya kupitiwa na jopo moja la wataalamu.

x) Wataalamu kutoshirikiana kwa kubadilishana mawazo kuhusu idadi ya fonimu za Kiswahili sanifu.

xi) Usanifishaji wa Kiswahili kukosa kupitiwa upya tangu 1930 hadi leo na kubaini kasoro zilizopo.

xii) Baadhi ya wataalamu kuidharau na kutoifuata sera ya lugha ya kudhibiti maandishi ya taaluma za Kiswahili sanifu.

xiii) Kuwepo kwa yombo vingi vinavyosimamia lugha kama KAKAMA, BAKITA, BAKIZA badala ya kuwepo chombo kimoja cha kusimamia maandishi ya Kiswahili sanifu kikamilifu.

xiv) Mvutano kati ya wataalamu wazawa wa Kiswahili na wataalamu wasio wazawa wa Kiswahili sanifu katika taaluma ya idadi ya fonimu na matamshi yake sahihi na fasaha.

Sababu hizi kama zilivyoelezwa kwa mujibu wa utafiti huu ndizo zinazofikiririwa kwamba zilizowafanya wataalamu zaidi ya 35 kutofautiana katika idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Baadhi ya sababu hizi kama ya Wataalamu kuathiriwa na mikabala ya fonimu za lugha nyingine za Kiingereza, Kiarabu na Kibantu, pia imezungumziwa na Batibo (1980). Sababu ya Usanifishaji wa Kiswahili kufanywa na wataalamu wageni yaani, Wazungu ambao waliathiriwa na taaluma za lugha zao pia nayo imezungumziwa na Mbaabu (2007). Hivyo utafiti huu unakubaliana kikamilifu na sababu hizo. Matokeo ya suali la 2 la Hojaji kuhusu Isharasauti Ambatano Ng'ong'o [ mb, nd, ng, nj ] na isharasauti mpumuo na [ $p^h$, $t^h$, $k^h$, $ch^h$ ] zimebainika kuwa ni fonimu za Kiswahili sanifu kutokana na kupatikana kwa kanuni ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili za maneno ya Kiswahili.

Matokeo ya swali la 2 la Mahojiano kuhusu idadi na aina ya fonimu za lugha zaKiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania imebainika kuwa Wasailiwa wa lugha hizo wa kila somo wamewasilisha idadi ya aina moja fonimu konsonanti na irabu. Kwa kila somo Wasailiwa wake wameonesha tofauti ya konsonanti moja na kutokuwa na tofauti yoyote katika idadi ya irabu kwa kila lugha. Matokeo hayo yalithibitisha kwa tatizo kuwa tatizo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika lugha hizo ni dogo mno, kiasi kwamba halifanani kabisa na tatizo lilopo katika Kiswahili sanifu.

### 5.2.3 Matokeo ya Lengo Mahsusi la Pili

Katika kujibu lengo mahsusi la Pili, Wasailiwa walitakiwa bainishe athari za kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu. Matokeo yameibua athari 15 miongoni mwao athari sita zilibainishwa na Wasailiwa wa Hojaji, athari sita zilizowasilishwa na Wasailiwa wa Mahojiano na athari tatu zimchangiwa na mtafiti. Athari hizo ni:

i) Kuzusha mkanganyiko na ubabaifu wa kutoifahamu ni ipi idadi sahihi kati ya 27, 28, 29, 30, 31, 32, 33, 34, 35, 36, 37, 38, 40, 41, 42, 45, 58.

ii) Kujenga migongano na mizozo baina ya wataalamu katika taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake.

iii) Kuonesha mbaguano wa wataalamu kwa kutokuwa na idadi linganifu ya fonimu na viashiria vyake.

iv) Kiswahili sanifu kukosa idadi sahihi ya fonimu na viashiria vyake.

Kuibua mikabala mingi na kila mmoja kujiona yuko sahihi katika taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake.

vi) Kuwavunja moyo wanafunzi kuchagua somo la lughawiya kwa kutokana na kutokubaliana kwa wataalamu wake.

vii) Wataalamu kuibua mikabala mingi na kila mmoja kujiona yuko sahihi katika taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake.

viii) Kiswahili sanifu kukosa idadi sahihi ya fonimu na viashiria vyake.

ix) Wanafunzi wa umahiri na uzamivu kulikwepa somo la Lughawiya kwa kukosa udhibiti na kukimbilia somo la Fasihi.

x) Kuzusha ubabaifu na kuchanganyikiwa katika kutoifahamu ni ipi idadi sahihi kati ya 27, 28, 29, 30, 31, 32, 33, 34, 35, 36, 37, 38, 40, 41, 42, 45, 58.

xi) Kudharaulika kwa Kiswahili kwa kukosa msimamo mmoja wa idadi ya fonimu na viashiria vyake.

xii) Kiswahili sanifu kukosa mkabala mmoja wa idadi halisi ya fonimu na viashiria vyake.

xiii) BAKIZA kutokaa kufanya kazi yao vyema kwa kutosimamia suala la idadi ya fonimu na viashiria katika Kiswahili sanifu.

xiv) Kiswahili kutofautiana na lugha nyingine za kimataifa kama Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania ambazo wataalamu wao wamelingana sana katika ubainishhaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika lugha zao.

xv) Viashiria vya fonimu kutokuwa mahsusi kwa kila fonimu moja na badala yake kila muandishi kuamua kutumia viashiria vyake kinyume na lugha maarufu za kimataifa kimataifa kama Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania ambazo pia wataalamu wao wote wamelingana vyema tu.

Athari hizi ndizo zinazofikiriwa kuwa zinaathiri taaluma ya idadi ya fonimu *na viashiria* vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Kila athari moja ukiiangalia ina mantiki ya kuwasukuma wataaalamu kuweza kupwekeka kimtazamo wake katika taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake. Kati ya athari hizo 15, utafiti huu unakubaliana zaidi na athari za: Kuzusha mkanganyiko na ubabaifu wa kutoifahamu ni ipi idadi sahihi kati ya 27, 28, 29, 30, 31, 32, 33, 34, 35, 36, 37, 38, 40, 41, 42, 45, 58. Kiswahili sanifu kukosa idadi sahihi ya fonimu na viashiria vyake. Wataalamu kuibua mikabala mingi na kila

mmoja kujiona yuko sahihi katika taaluma ya idadi ya fonimu na viashiria vyake. Kuwavunja moyo wanafunzi kuchagua somo la lughawiya kwa kutokana na kutokubaliana kwa wataalamu wake. Kwa bahati athari hizi kama ilivyoelezwa hapo awali, pia zinawaathiri hata wahadhiri na wanataaluma wa vyuoni na kufikia uamuzi wa kulikimbia somo hili kwa kuliona halina mkabala mmoja wa kitaaluma.

### 5.2.4 Matokeo ya Lengo Mahsusi la Tatu

Kwa kullifanyia kazi lengo mahsusi la Tatu, Wasailiwa walitakiwa watoe mapendekezo ya kurekebisha tatizo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Matokeo yameibua mapendekezo tisa yaliyowasilishwa na Wasailiwa wa Usaili wa Hojaji na Mahojiano. Mapendekezo hayo ni:

i) Ufanyike utafiti wa kina kwa kutumia vigezo vya kisayansi ili kupata idadi halisi ya fonimu za Kiswahili sanifu.

ii) Wataalamu watumie kanuni ya kisayansi katika fonolojia ya Kiswahili katika uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake.

iii) Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA) iandae Warsha kwa wataalamu ili wachunguze idadi halisi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

iv) Itumike nadharia teule ya kisayansi kwa wataalamu wanaobainisha idadi ya fonimu na viashiria vyake.

v) Mabaraza ya Kiswahili yaweke udhibiti wa kuyathibitisha maandishi ya taaluma ya fonolojia ya Kiswahili sanifu. Kamisheni na mabaraza ya Kiswahili yashirikiane katika kusimamia maandishi ya taaluma za Kiswahili sanifu.

vi) KAKAMA iandae jopo la wataalamu weledi wakae na kudurusu Sera ya Kiswahili na usanifishaji wake ili kudhibiti idadi ya moja ya fonimu na viashiria vyake.

vii) Wataalamu waoneshe nadharia au kanuni iliyowaongoza wanapowasilisha idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu.

viii) Utafiti wa idadi ya fonimu na viashiria vyake ufanyike kwa kusikia matamshi ya sauti za wazungumzaji badala ya maandishi ya wataalamu.

ix) Mabaraza ya Kiswahili yatoe ithibati ya kazi zote zinazoandikwa katika taaluma za lughawiya ya Kiswahili sanifu.

Mapendekezo haya kila moja lina nafasi yake ya kuchangia kurekebisha tatizo la wataalamu kutofautiana katika idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojiia ya Kiswahili sanifu. Kwa ujumla, matokeo ya utafiti huu yamesaidia kufikia hitimisho na kuliziba pengo kuhusu suala la wataalamu zaidi ya 35 kutofautiana katika idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

## 5.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umeibua mchango ufuatao:

1. Kwa kuitumia mwongozo wa kanuni ya kisayansi ya Nitoe Nikutoe katika Jozi Sahili utafiti huu umebaini idadi ya fonimu 47 za Kiswahili sanifu zilizogawika kama ifuatavyo:

i) Fonimu za konsonanti vipasuo ni 9: / p, $p^h$, b, t, $t^h$, d, k, $k^h$, g /.

ii) Fonimu za konsonanti vikwamizi ni 11: / f, ﬁ, v, θ, ð, s, z, ʃ, X, ɣ, h /.

iii) Fonimu za konsonanti vipasuo-kwamizi ni 3: / $ʧ^h$, $ʧ^h$, ɟ /.

Fonimu za konsonanti ving'ong'o ni 9: / m, n, ɱ, ɓ, ɗ, ŋ, ή, ɲ, ʄ/.

v) Fonimu za konsonanti kitambaza ni 1: / l /.

vi) Fonimu za konsonanti kimadende ni 1: / r /.

vii) Fonimu za konsonanti viyeyusho ni 2: / w, j /.

viii) Fonimu za irabu fupi ni 6: / a, ɛ, ɪ, ɔ, ʊ, -' /.

ix) Fonimu za irabu refu ni 5: / a: ɛ: ɪ: ɔ: ʊ: /.

2. Isharasauti **[ m, n, b, f ]** ni fonimu silabi funge za Kiswahili sanifu na zinahitaji kubainishwa kimaandishi kwa koma juu ( ' ) katika maneno kama: m'baazi (mti), ili litafautike na mbaazi (nafaka), m'boga (mmea), ili litafautike na mboga ( majani), m'buni (mti), ili litafautike na mbuni (ndege), m'buyu (mti) ili litafautike na mbuyu (nafaka).

3. Kufuatana kwa isharasauti ng'ong'o mbili za **[ mm ]** na **[ nn ]** kimatamshi na kimaandishi si makosa kwa maneno ya Kisawhili sanifu kama **nn**je**, nn**ge**, nn**joo**, mmbu, mm**bwa kwani tayari yapo maneno **nn**e na **mm**oja ambayo yanatumika kimatamshi na kimaandishi.

4. Fonimu **/ w /** na **/ j /** ziko katika kundi la konsonanti viyeyusho na haziko katika kundi la irabu kama zinavyoitwa nusu irabu kutokana na sifa bainifu zao (taz. 4.2.4 Jozi ya iv na Tanbihi).

5. Kiswahili kina irabu fiche ambayo kiuhalisia irabu hiyo inadhihirishwa kimatamshi lakini haidhihirishwi kimaandishi kwa maneno kama: **As**kari, **lab**da, **kas**kazi, **kab**la, **m**moja**, m**kate, **m**zo, **m**ba, **n**ta, **n**zi, **n**zio, **nk**e na **n**nj*e*.

6. Kiswahili nacho kina fonimu irabu ambatano ambazo Waingereza wao wameziita *diphthong* ambazo ni: / ɪa, ɛɔ, aɪ, ɔa / katika maneno ( lia, leo, lai, loan a lau.

Mchango huo uliotokana na utafiti huu umeibua taaluma ambayo tangu wataalamu wa mwanzo wa taaluma ya lughawiya ya Kiswahili sanifu, akina Johnson (1939), Ashton (1944) na Krum (1940) hadi wataalamu wa sasa akina Khamisi ((2005)), Massamba (2012) na TATAKI & BAKITA, (2013) bado hawakuyawasilisha mambo hayo katika taaluma ya fonoloija ya Kiswahili sanifu. Hivyo, machango huo unafikiriwa, kusaidia katika kukiweka Kiswahili sanifu katika mkabala na mustakbali mpya wa idadi ya fonimu na viashiria vyake pamoja na fonimu zilizoibuliwa ambazo zilikuwa zina mushkeli kwa baadhi ya wataalamu na kusababisha kutofautiana kwa wataalamu kama ilivyoelezwa hapo awali.

## 5.4 Hitimisho

Katika sura hii utafiti umeeleza matokeo ya utafiti kulingana na majibu ya malengo na maswali yake matatu ya utafiti huu. Pamoja na matokeo hayo, utafiti pia umegundua mchango wa ziada wa kilichokusudiwa kutafitiwa. Mchango huo ulioibuliwa umekusudiwa kusaidia ama kupunguza au kuondoa tatizo la kutofautiana kwa wataalamu zaidi ya 35 katika mfumo mzima wa uwasilishaji wa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

## SURA YA SITA

## HITIMISHO, MAPENDEKEZO NA MAONI

### 6.1 Utangulizi

Sura hii imeongoza kuangalia hitimisho la jumla la matokeo ya utafiti huu. Kisha, kuelezea kuhusu mapendekezo ya ama kupunguza au kuondoa suala zima la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Hatimaye kutoa maoni kwa wataalamu wa Kiswahili hasahasa wanafonolojia wa Kiswahili sanifu.

### 6.2 Hitimisho

Utafiti huu ulilenga kutafiti, kukusanya na kuchanganua data za tatizo la kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Matokeo haya yalitokana na data zilizochanganuliwa na kushereheshwa pamoja na uthibitisho wa uchanganuzi wa maswali manne ya usaili wa Hojaji na maswali manne ya usaili wa Mahojiano. Matokeo ya utafiti huu yalizingatia zaidi malengo ya sababu, athari na mapenekezo ya nini kifanyike ili kusawazisha tatizo la wataalamu wa lughawiya ya Kiswahili sanifu katika suala la idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Utafiti kwa jumla, umetuthibitishia kuwa usanifishaji wa Kiswahili uliofanywa hapo zamani yaani, mwaka 1930 na Wazungu ulikuwa na kasoro katika idadi ya fonimu na viashiria vyake.

Kwa kweli tatizo la wataalamu kutofautiana katika idadi ya fonimu na viashiria vyake katika lugha moja ya Kiswahili sanifu ni suala linalowachanganya na kuwababaisha wanataaluma na wahadhiri pale wanaopkutana nalo katika mafunzo ya darasani kwa kutofahamu waidhibiti idadi gani ipi au ya mtaalamu yupi. Dhamira yao ya kufahamiana

na kuwasiliana inaweza kuwa na makosa fulani ya kisarufi au kilughawiya. Lakini wataalamu wanaopokubaliana kwa idadi sawa ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu, wataibua kanuni sahihi itayowongoza watumiaji wa Kiswahili sanifu, kusema na kuandika maneno sahihi kwa kutumia fonimu mahsusi za lugha hii.

Hali hii inahitajika sana katika Kiswahili sanifu kwa sababu hali ya kutofautiana katika idadi ya fonimu na viashiria vyake, ina athari kubwa sana kwa wasomi wa fonolojia ya lugha hii. Wasomaji, ambao wengi wao hawana kisomo cha kutosha, wanachukulia lugha ya maandishi kama lugha sahihi, sanifu na yenye usahihi wakati kumbe matamshi ya kusemwa au kuzungumzwa ndio msingi wa usahihi na ufasaha wa lugha kama ilivyokwisha elezwa hapo awali. Kuhifadhi, kulinda na kutetea usahihi wa lugha kama nguzo ya utamaduni wa Kiswahili sanifu ni jukumu la wanalughwiya wote wakiwemo wataalamu wasemaji, wazungumzaji na hata watumizi wa lugha hii ya Kiswahili.

## 6.3 Mapendekezo

Baada ya kubaini kuwa ni kweli kuna kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu, utafiti huu umependekeza yafuatayo ili kuwe na idadi halisi ya fonimu na viashiria vyake mahsusi katika Kiswahili sanifu:

i) Viashiria vya fonimu ambatano ng’ong’o kama [ mb, nd, ng na nj ] pamoja na irabu zote ni vyema viwakilishwe kwa viashiria vya kifonetiki badala ya kiotografia ili kuwe na usambamba wa viashiria hivyo na kutowababaisha watumizi wake.

ii) Kila fonimu moja ya Kiswahili sanifu iwe na kiashiria kimoja tu cha kifonetiki kinacholingana na kiashiria cha Alfabeti za Kifonetiki za Kimataifa (AKIKI) ili kuondoa utaratibu wa fonimu moja kuwa na vishiria vingi.

iii) KAKAMA iandae warsha ya kuipitia, kuimarisha na kuisimamia sera ya lugha ya Kiswahili pamoja na suala la kuupitia upya usanifishaji wa Kiswahili sanifu ili kuihifadhi lugha hii kwa kuwa na idadi mahsusi ya fonimu na viashiria vyake badala ya kuruhusu kila mmoja kuwa na idadi na viashiria vyake binafsi.

iv) Imefikia wakati sasa Kiswahili sanifu kiwe na chombo kimoja tu cha juu kabisa cha kukisimamia na kukiimarisha Kiswahili katika sera na usanifu wake ili Kiswahili nacho kipate hadhi zaidi ya kuwa lugha sanifu, lugha rasmi na lugha ya taifa kwa Tanzania na Afrika Mashariki na lugha ya kimataifa duniani kote.

v) Mabaraza ya Afrika Mashariki yanayokuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili sanifu, chini mwamvuli wa KAKAMA yawezeshwe kikamilifu kifedha yaweze kukaa pamoja na kujadili mikakati na mielekeo ya kuondosha tatizo la idadi ya fonimu na viashiria vyake katika Kiswahili sanifu ili khatma ya Kiswahili sanifu iwe ya hadhi ya juu zaidi.

vi) Utafiti huu uwahamasishe na uwashawishi watafiti wa fonolojia ya Kiswahili sanifu kuendeleza tafiti za taaluma ya fonimu na viashiria vyake ili kuziba mapengo mengine yaliyoachwa katika utafiti huu.

vii) Pamoja na ukamilifu wa matokeo ya utafiti huu yalivyofikiwa, kwa vile suala la utafiti ni la kudumu, Mtafiti wa kazi hii anapendekeza watokee watafiti wengine

wauendeleze utafiti huu kwa pale palipofikiwa kwa njia ya kuimarisha matokeo yaliyopo na kukiweka Kiswahili sanifu katika mazingira ya kutafitiwa kisayansi.

## 6.4 Maoni ya Mtafiti

Kwanza, idadi, ya fonimu 47 na viashiria vya kifonetiki vilivyopendekezwa katika utafiti huu, izingatiwe na umoja wa wataalumu wa fonolojia ya Kiswahili sanifu wa Afrika Mashariki. Pili, Idadi hiyo iwe ni chachu na muongozo wa pamoja kwa wataalamu kwa nia ya kupunguza au kuondoa kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu. Tatu, mapendekezo yaliyotolewa kwa jamii zilizokusudiwa yazingatiwe kikamilifu na yapangiwe utatekelezaji wake, kwa nguvu za pamoja ya vyombo vinavyohusika. Nne, kama maoni haya yatafanyiwa kazi na vyombo vinavyohusika, bila shaka kuna matarajio makubwa ya kupunguza kama si kuondoa kabisa matatizo ya kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu.

Maoni haya yanaungwa mkono na Achebe (1958) katika riwaya yake ya *Things Fall Apart* alipohoji kwamba mtu anayewaalika jamaa zake kwenye sherehe, hafanyi hivyo kwa ajili ya kuwaokoa na njaa. Waalikwa wote wana vyakula vyao majumbani kwao. Tunapokusanyika usiku wa mbaamwezi katika ardhi ya kijiji chetu, siyo kwa sababu ya mbaamwezi. Kila mmoja wetu angeweza kuiona mbaamwezi akiwa nyumbani kwake bali tunakusanyika kwa sababu ni jambo zuri kwa jamaa kukusanyika pamoja. Kwa hiyo tuendelee na umoja wetu ili tufurahie nguvu ya kuwa pamoja. Tukitabasamu haina maana kwamba hatuna matatizo isipokuwa tuna nguvu ya kushinda matatizo yetu. Peke yako unaweza kutabasamu lakini mkiwa pamoja mnaweza kucheka. Ukiwa peke yako unaweza kufurahi lakini mkiwa pamoja mnaweza kushereheka. Ukiwa peke yako unaweza kutamka

lakini mkiwa pamoja mnaweza kuongea. Tuendeleze mambo yetu ambayo yanaweza kutuunganisha pamoja kuliko kuwa na mambo yanayotusababisha kutengana.

Chinua Chebe hapa anasisitiza kuwa mambo yetu yawe ya kijamii au kitaaluma yanahitaji muunganiko na makubaliano ya pamoja kwa taratibu na kanuni zinazokubalika na wote ili kuepusha kutolingana na kutofautiana kunakoleta kufarakana na kusambaratika kwa nguvu ya pamoja. Nami nafungia ripoti ya utafiti huu kwa kumuunga mkono Achebe kwa kunukuu usemi wa wahenga wa Kiswahili unaosema, ‘‘Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu’’.

Hatimaye mtafiti anahitimisha maoni yake kwa kusema kwamba utafiti huu wa taaluma ya sayansi ya jamii, uchukuliwe kama ni juhudi mojawapo tu ya mtafiti kulitafiti tatizo la wataalamu kutofautiana kwa idadi ya fonimu na viashiria vyake katika fonolojia ya Kiswahili sanifu, sio kwamba umekamilisha taaluma hii. Kuna matatizo mengine mengi ambayo yanahitaji kuchunguzwa katika taaluma ya fonimu za Kiswahili sanifu. Hivyo, watokee watafiti wengine waendelee kuyachunguzwa ili fonolojia ya Kiswahili sanifu izidi kuwa na mkabala imara na thibitifu duniani kama zilivyo fonolojia za lugha tatu maarufu za kimataifa za Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu.

## MAREJEO


Abdulhamid, S. (2003). *Taysiiru rahni fii tajwiid al-Kur-an*. Shibra Alkhiima: Daaru Atakwaa.

Abdutawaab, R. (1997). *Almadkhuli ila ilmu al-Arabiya.* Kuwait: Islamic Foundation Ltd.

Abry, D. & Veldeman, J. (2007). *La phonetique*. Paris: CLE International.

Akidah, M. A. (2013). Phonological and semantic change in language borrowing:

Akyüa, A. (2002). *Exercises D' oral en contexte.* Français: Hachette

Ali, U. M. (2009). *Tafsiri ya buluughu al-maraam.* Mombasa: Al-hikma for Authorship & Translation.

Alston, M. & Bowles, W. (2007). *Research for social workers: An introduction to methods 2nd edition.* London: Routledge, Tylor & Francis Group.

Anderson, S. (1985). Phonology in the twentieth cenntury. Theories of rules and theories of representations. Chicago and London: The Chicago University Press.

Anderson, T. (1956 -57). *Mordern Spanish: A Project of modern language association.* New York & Burlingame: Hartcourt. Brace & World.

Angongo, J. (1983). ‘‘Fonimu za Kiswahili’’ katika *TUKI*: Dar-es- Salaam: TUKI.

Ashton, E. O. (1944). *Swahili grammar including intonation*. London: Longman Group.

Aswani, F. O. (1995). Fonolojia ya silabi za Kiswahili sanifu na za Kimarama*:* Uchunguzi linganishi. Tasnifu ya Uzamili ya Falsafa ya Kiswahili sanifu. Eldoret: Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapshwa)

Azevedo, M. (2005). *Portuguese a linguistic introduction* Cambridge: Ersity Press

Bailey, K. D. (1994). *Methods of social research.* Belmont: Wadsworth.

Bakhressa, S. K. (1999). *Kamusi ya maana na matumizi*. Nairobi: Oxford University Press.

BAKITA (1994). *Mwongozo kwa waandishi wa Kiswahili sanifu*. Chapa ya Kwanza. Dar es Salaam: BAKITA na Dar es Salaam University.

BAKITA (1998). *Kiswahili sanifu na sahihi.* Dar es Salaam: Baraza la Kiswahili sanifu la Taifa.

BAKITA (2004). Kiswahili sanifu na utandawazi. Toleo la Tano. Dar es Salaam: BAKITA.

BAKITA (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn publishers Limited.

BAKITA na TATAKI (2013). *Mwongozo kwa wataalamu wa Kiswahili sanifu*. Toleo la Pili. Dar es Salaam: BAKITA.

BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili fasaha.* Nairobi: Oxford University Press.

Batibo, H. M. (1980). Je Fonolojia ya Kiswahili ni ya Kibantu? Makala iliyowasilishwa katika Semina Iringa (Haijachapishwa).

Bauer, L. (2008). *The linguistics student's Handbook*. Edingbergh: Edingbergh University Press.

Besha, R. (1994). *Utangulizi wa lugha na isimu*. Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam University Press.

Besha, R. M. (2007). Utangulizi wa lugha na isimu. Dar es Salaam, Macmillan Aidan Ltd.

Black, W. (2016). *The handbook of Portugues linguistic*. Oxford: John Willey & Sons Ltd.

Blaxter, L. (2006). *How to research Third Edition*. England: Open University Press.

Bloomfield, B. W. (1931). *Sarufi ya Kisawhili*. London: The Sheldon Press.

Borobio, V. (2002). *Curso de espanol para extranjeros.* Spain: Instituto Cervantes.

Brandão de Carvalho, J., Nguyen, N. na Wauquier, S. (2010) *Comprendre la phonnologie.* Paris: Presses Universitaires de France.

Bryman, A. (2004). *Social research methods.* New York: Oxford University Press.

Burns, N and Grove, S. (2003). *The practice of nursing research conduct, critique and utilization* ($4^{th}$ ed), Philadelphia: Pennsylvania Publishers

Cappelle, G. na Menand, R. (2009). *TAX I Methode de Francais*. Paris: hachette Francais Langue Etrangere.

Chaliac, L.& Motron, A. C. (2004). Phonetique progressive DU Français: CLE International.

Chaliac, L.& Motron, A. C. (2006). *Phonetique rogressive DU Français*: CLE International.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Choge, S. (2009). Undestanding Kiswahili vowels. *Journal of Pan African Studies*. Vol. 2 p. 4-7 Nairobi: Nairobi University Press.

Christiane, A. M. (1971). *Baltaxe. principles of phonology* Los Angeles: University of CaliforniaPress.

Collins, B. & Mees, I. M. (2008). Practical phonetics and phonology Second Edition a Source Book for Students. London: Routledge Tylor & Francis Group.

Confied, D. L. (1981). *Spanish in the pronounciation in the America*. London: The University of Chicago.

Conha, E. (2005). Portugues self-taught (thimm's system) with phonetic pronounciation. New Delhi: david Mckay Company Publishers.

Cordoso, H. C, Baxter, A. N. & Nunes M. P. (2012). *Ibro-Asian creoles*; *comparative* Amsterdam: John Begammins Publishing Company.

Creswell, J. (2009). Research design qualitative, quantitative, anda mixed methods approaches (3rdEd). SAGE Publications. Inc.

Darwesh, A. (2009). A phonological semantic approach to Arabic teminology. Melbourne: Whites Cop P+Y Ltd.

David, D. (2005). *How many consonant sounds are there in English?* Singapore: National Institute of Education.

Delgado, M. M. R. (1988). *Ouvir falar. Introducao a fonetica doPortugues*. Ed. Lisboa: Caminho.

Duhne, E. E., Emilsson, E., Montoya, T. M., Rio, R, (1997). *Pido la palabra.* Mexico: Universidad Nacional Autónoma de México.

Easy Spanish Phrase Book **(**1994). *Spanish language material*. New York: Dover Publishcations Inc.

Edinburgh University Press (2005). *Key thinkers in linguistics and the philosophy of language.* Edinburgh: Edinburgh University Press.

Espada, F. (2006). Manualde fonetica exercicios e explicacoe. Lisboa-Porto: Lidel.

Finch, G. (2003). *How to study of linguistics. A guide to understanding language* (Second Edition) Great Bitain: Palgrave Macmillan.

Firth, J. (1957). *Papers in linguistics* 1934 – 51. London: London University Press.

Fischer, M. (1975). *Trends ni phonological theory*. Copenhagen: Akademisk Forlag.

Fishman, J. (1971). Advances in the sociology of languageI. The Hague. Mouton.

Foley, J. & Thompson, L. (2003). *Language learning: A lifelong process*. London: Arnold.

Gilbert, N. (2008). *Researching social life.* London: SAGE Publications Ltd.

Gromova, N. V. (2008). *The Swahili language in contemporary*in Swahili Forum 15.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili.*Nairobi: Oxford University Press.

Halle, M. (1959). *Sound pettern of Russian*. The Hague: Mouton.

Harris, Z. S. (1951). *Methods of structural linguistics*. Chicago, University of Chicago Press.

Haugen, E. (1966). Dialect, language, nation. American Anthropologist 68: 922-35.

Hélène, H. (2012). La morphologie forme et sens des mots du français. Paris: Armnd Colin.

Jakobson, R. & Morris Halle (1971). *Fundermentals of language*. The Hague: Mouton.

Jama Masjid (1950). *The adaab of reciting the Holly Qur'an.* Delhi: IMA Publishers Pvt. Ltd

Johnson, F. (1939). *A standard Swahili-English dictionary*, Nairobi, Oxford University Press.

Johnson, F. (1939). *A standard English-Swahili dictionary*, Nairobi: Oxford University Press.

Jones, D. (1957). *An outline of English phonetics*. Cambridge, Cambridge University Press.

Jonguero, R. (2001). *Vamos aprender Portugues*. Lisbon: Alicerce Editorial Lda.

Joseph, G. (2004). Makosa ya mara kwa mara ya finyanzo kwenye maandishi ya Kiswahili sanifu. K. Mtesigwa na M. Mwinyi (Wahariri) katika *Lugha Yetu*. *39*. Kur.74-76. Dar-es-Salaam: BAKITA.

Journal of education and research, 1(4), kur. 1-20.

Juma, H. K. (2017). Tathmini ya mitaala ya ufundishaji wa Kiswahili sekandari katika matumizi ya nadharia nchini Tanzania. Katika *KISWAHILI*: Jarida la Taasisi ya Uchunguzi. Juz. 80: Kur. 1-16. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Juma, H. K. na Mushi, C. (2019, Disemba 19-21). Dhima za Kiswahili sanifu katika maendeleo ya fasihi na isimu. Makala elekezi ilyowasilishwa katika Kongamano la BAKIZA lililofanyika Zanzibar. (Haijachapishwa).

Kadeghe, M. (2005). *Phology, semantics and stylistics*. Dar-es-Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Karim, C. R. (2004). *Arabic linguistic introduction.* New York: Cambridge University Press.

Katamba, F. (1989). *An introduction to phonology*. London: Longman.

Kess, A. (2014). *The Arabic language*. Manchester. Edinberg University Press.

Khalid, A. (1977). *The liberation of Swahili from European apropriation.* Nairobi: East African Litereture Bureau.

Khamis, A. (2005). Athari za nadharia na kanuni za uandishi wa matamshi ya baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu. N. Ogechi, N. Shitemi, K. Simala (Wahariri)

katika *Nadharia ya Taaluma ya Kiswahili na lugha za kiafrika*. kur .175-184 Eldoret: Moi Universty Press.

Khamis, A. (2010, Machi 20). Makosa ya Kiswahili sanifu yanayofanywa na umma wa watanzania na sababu zake katika mawasiliano sahih**.** Makala iliyowasilishwa kwenye Kongamano la Chawakama katika Ukumbi wa Chuo Kikuu cha St. John Dodoma. (Haijachapishwa).

Khamis, A. (2011). *Uchanganuzi wa Kiswahili fasaha.* Zanzibar: University College of Education Press.

Khamis, S. A. (1984). Urban versus rural Swahili (A study of Pemba varieties*)*. Tasnifu ya Shahada ya Tatu ya Falsafa ya Chuo Kikuu Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Khamisi, A. M. (2005). Kiswahili ikiwa ni lugha ya kimataifa. katika *Lugha ya Kiswahili.* Dares Salaam: TUKI.

Kihore Y. M. (1996). *OFC 003 Kiswahili sanifu.* Dar es Salaam: Open University of Tanzania.

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B., na Msanjila, Y. P, (2000). *Sarufi miundo ya Kiswahili sanifu (SAMIKISA).* Dar es Salaam: TUKI.

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B. na Msanjila, Y. P. (2001). Isimujamii sekondari na vyuo, Dar es Salaam: Taasisi ya Kuchunguza Kiswahili.

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B. na Msanjila, Y. P. (2001). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu.* (SAMAKISA) Dar es Salaam: TUKI.

King'ei, G. K. na Musau, M. (2002). *Matatizo wa Kiswahili sanifu.* Nairobi: Didaxis.

Kipacha, A. (2010). *Sarufi ya Kiswahili sanifu*. Dares Salaam: Open University of Tanzania.

Kirkeby, W. A. (2002). *English-Swahili dictionary*. *Dar es Salaam*: Kirkeby Publishing Company.

Kiswahili sanifu. *Journal of ZAP Chancery*, Eldoret: Moi University

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: methods and techniques*. 2nd Edn. New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Krapf, J. L. (1885). Kiswahili sanifu language with special reference to the Kinika. Tubingen.

Krauss, M. E. (1992). The world's languages in crisis. Language 68 (1). 4-10.

Krum, B. (1940). *Words of oriental origin in Swahili.* London: The Sheldon Press.

Kutub Khana (673). *Juzuu Amma*. Mombasa: Ishayatu-ul-Islam.

KVDA PLAZA.

Lekule, S. (2013). Bubujiko la maarifa katika *chomboz.blogspot.com*.17 March, 2013

Ligami, P. (2002). Ujuzi na utendji katika lugha ya Kiswahili sanifu*:* Umuhimu wa Utafiti. katika *Utafiti wa Kiswahili*. Kur.136-139. Eldoret: Moi University Press.

Lodhi, A. Y. (1976). *Notes on Swahili phonology* (Handout) Upsala: Upsala University.

Lodhi, A.Y. (1976). *Notes on Swahili phonology. (Handout).* Upsala: Upsala University.

Lodhi, A.Y. (2000). Oriental influences in Swahili: A study in language and culture conacts. Upsala: Enlanders Grafic System.

Lodhi, A.Y. na Otterbrandt, T. (1987). *Kortfattad Swahili-Svensk Svensk-Swahili Ordbok.* Motala Tryck: Motala Grafiska.

Lyons, J. (1968). *An introduction to theoratical linguistics.* London: Cambridge University Press.

Macpherson, I. R. (1975). *Spanish phonology: Descriptive and historical*. New York: Manchester University Press. Burnes & Noble Books.

Madeira, E., LdaPei, M. & Gaynor, F. (1954) *A dictionary of linguistics.* New York: Philosophical Library Publication.

Madumulla, J. na Kihore, Y. M. (2005). Wahariri**.** *Kiswahili sanifu Juzuu 68.* Dar es Salaam: TUKI.

Maganga, C. (1979). *Fonolojia ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Maganga, C. (1984). *Misingi ya fonetiki matamshi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Maganga, C. (1991). A study of the morphophonology of standard Swahili, Kipemba, Kitumbatu and Kimakunduchi *Tasnifu ya Shahada ya Tatu ya Falsafa.* University of Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

Maganga, C. (1997). *Historia ya Kiswahili.* Dar-es-Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Maria, M., Mira, H. & Andrea de, E. (2000). *The phonology of portuguese*. Oxford:

Mario, A. P. & Frank, G. (1954). *A dictionary of linguistics.* New York: Philosophical Library.

Maro, B. (2013, Mei 7). Maneno yatumiwayo vibaya. katika *Nipashe* - *Jungu letu* Nam. 057744 la Jumaane, uk. 2.

Martinent, A. (1973). *Morphonemics.* New York: Holt, Renehert and Winston.

Massamba, D. P. B. (2002). Historia ya Kiswahili sanifu 50 Bk hadi 1500 BK. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Massamba, D.P.B. (1996). *Phonological theory: History and development*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya isimu na falsafa ya lugha*. Dares Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).

Massamba, D.P.B. (2012). *Misingi ya fonolojia.* Dares Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI).

Mathooko, P. M. (2007). *Isimu jamii misingi ya nadharia*. Nairobi: Bird Printers & Stationers.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya lugha, isimu na nadharia kwa sekondari, vyuo na vyuo vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers Ltd.

Mayoka, J. M. (2007, Novemba 12-15). Umuhimu wa Kiswahili sanifu na sahihi katika vyombo vya habari na elimu. Makala iliyotolewa katika Kongamano la kimataifa la Idhaa za Kimataifa Duniani lililofanyika Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

Mbaabu, I. (1985). *Sarufi ya Kiswahili. Nairobi,* Kenya Publishing & Book Marketing Co. Ltd.

Mbaabu, I. (2007). Historia ya usanifishaji wa Kiswahili sanifu. Dar es Salaam: TUKI.

Mbogo, S., Kitula, M., Gimbi, A., Ngaruko, D., Massomo, S., Kizoza, J. et. al. (2012) *Reseach methodology*. Dar es Salaam: Open University of Tanzania.

Mbonde, J. M. (1976). (Mhariri). *Uandishi wa insha Tanzania*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Mbunda, F. L. (1976). *Mwalimu wa lugha ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Mc Dale, S. A. (1999). *Wrriting a dissertation proposal*. Washington: The George Washington Universty Press.

Menand, R. (2009). *Le nonvean taxi 1. Methode de Francais.* France: Hachette Francais Langue Etrangere.

Menand, R. (2009). *Le nonvean taxi 2. Methode de Francais.* Paris: Hachette Francais Langue Etrangere.

Menand, R. and Johnson, A. (2010). *Le nonvean taxi 3. Methode de Francais.* Paris: Hachette Francais Langue Etrangere.

Mfaume, G. (1985). *Misingi ya isimu ya lugha ya Kiswahili sanifu.* Dar-es-Salaam: Utamaduni Publishers.

Mgullu, R. (2001). Mtalaa wa isimu: Fonetiki, fonolijia na mofolojia ya Kiswahili. Nairobi: Longman Publishers.

Mhina, G. A. (1970). *Kiswahili sanifu na maendeleo.* London: Thomas Nelson and Sons Ltd.

Mlacha, S. A. K. (2004). Kiswahili sanifu katika kanda ya Afrika mashariki. Dar es Salaam: TUKI.

Mmallavi, A. P. W. (1977). *Lugha katika jamii.* Dar es Salaam: East African Publishing House.

Mohamed, A. M. (2011). *Comprehensive swahili-english dictionary.* Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mohammed, A. M. (1972). Maendelezo ya maandalizi ya Kiswahili sanifu katika *Lugha Yetu*. Toleo la 5 kur. 1- 13. Dar es Salaam: BAKITA.

Mohammed, A. M. (1986). *Sarufi mpya*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Mohochi, S. (2005, Julai 6-7). Twahubiri maji tukinywa mvinyo? Mielekeo ya wasomi na viongozi kuhusu lugha ya Kiswahili sanifu. Makala ya Semina (Haijachapishwa).

Msanjila, Y. P. (2005). Hali ya Kiswahili sanifu katika shule za sekondari Tanzania*: Udhalilishaji wa Lugha ya Taifa.* Makala ya Semina (Haijachapishwa).

Msanjila, Y. P., Massamba, D.P.B., na Kihore, Y. M. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili* Dar-es-Salaam: Taasisi ya KuchunguzaKiswahili.

Mtesigwa, P. C. K. (2007, Novemba 12). Kiswahili sanifu kwa ushirikiano na mshikamano: Haja ya matumizi sahihi ya Kiswahili sanifu katika Vyombo vya Habari. Makala iliyotolewa katika Kongamano la kimataifa la idhaa za kimataifa duniani lililofanyika Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

Mutahi, K. (1990*). Introduction to language skills in Swahili*. Nairobi: University of Nairobi.

